ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango/Jimbo la Donge
10. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana,

		Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake

40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 27 Februari, 2018

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe Mwenyekiti, (Shehe Hamad Mattar) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya uwasilishaji wa Kauli ya Serikali kuhusu Hoja Binafsi ya Mjumbe kuhusu kuweka Miundombinu bora kwa watu wenye Ulemavu katika majengo, barabara, makaazi maeneo ya kupumzikia na maeneo mengine. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya Uwasilishwaji wa Kauli ya Serikali kuhusu Maombi ya wananchi wa Kisakasaka Zanzibar kuhusu namna wanavyoweza kufaidika kutokana na machinjio ya wanyama yaliyopo kwenye maeneo yao. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Ripoti ya Mapendekezo ya muelekeo wa Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2018/2019. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajei

Mhe. Bahati Khamis Kombo (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuweka hati mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Ripoti ya Mapendekezo ya Muelekeo wa Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2018/2019. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

TAARIFA ZA SERIKALI

Hoja Binafsi ya Mjumbe Kuweka Miundombinu Bora kwa Watu Wenye Ulemavu katika Majengo, Barabara, Makaazi, Maeneo ya Kupumzikia na Maeneo Mengine

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante. Sasa namwita Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Usafirishaji, ili aweze kutoa taarifa vizuri. Karibuni sana Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha rasmi taarifa ya serikali kuhusu utekelezaji wa maazimio ya Hoja Binafsi ya Mjumbe kuhusu kuweka Miundombinu Bora kwa Watu wenye Ulemavu katika majengo, barabara, makaazi, maeneo ya kupumzikia na maeneo mengine**.**

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukuwa kukushukuru wewe kwa kunipatia fursa hii adhimu wa kuwasilisha taarifa ya serikali kuhusu utekelezaji wa maazimo ya Hoja

Binafsi ya Mjumbe kuhusu kuweka miundombinu bora kwa watu wenye ulemavu katika majengo barabara, maakazi, maeneo ya kupumzikia na maeneo mengine.

Napenda pia kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mhe. Mohamed Said Mohamed Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kupitia Jimbo la Mpendae kwa kuwasilisha hoja hii, chini ya Kanuni ya 27(1) (n), 27(3), 49(1) na 50 za Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2016. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kupitia Hoja ya Mjumbe, Baraza lako Tukufu lilipitisha maazimio yafuatayo:

Kwanza, serikali kutekeleza kikamilifu na kwa vitendo masharti ya Kifungu cha 12 na 13 cha Sheria ya Watu Wenye Ulemavu yaani, (Haki na Fursa) Namba 9/2006 ambayo, imetungwa na Baraza la Wawakilishi pamoja na masharti mengine sambamba na vifungu hivyo.

Pili, kutungwa kwa kanuni na kuweka viwango na miongozo kwa watu wenye ulemavu, kuwawezesha kufikia vyombo vya usafiri wa umma, vituo vya vyombo hivyo, sehemu za kusimama, huduma, majengo ya umma, vituo vya michezo na sehemu za burudani.

Tatu, wamiliki wote wa majengo yaliyopo ambayo hayana miundombinu rafiki ya kuwezesha watu wenye walemavu kuyafikia wabanwe na serikali kama sheria hii inavyoagiza, wafanye marekebisho ya miundombinu hiyo, ili watu wenye ulemavu waweze kuyafikia.

Nne, serikali iwatake wasanifu majengo, wahandisi wa ujenzi na watu wengine wanaohusika na usanifu na ujenzi wa majengo kuzingatia masharti ya Sheria ya Watu Wenye Ulemavu wanapoanza kuandaa michoro na kuhakikisha majengo mapya yanakuwa na miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu. Aidha, serikali isitowe kibali kwa ujenzi wo wote mpya usiozingatia masharti ya sheria ya kuwa na miundombinu rafiki kwa walemavu.

Tano, ukaguzi maalumu ufanywe na serikali katika kuhakikisha kuwa majengo na ujenzi wo wote unafanyika kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Watu Wenye Ulemavu yanayotaka kuwepo kwa miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu.

Utekekelezaji wa Maazimio ya Hoja Binafsi ya Mjumbe

Mhe. Mwenyekiti, Baada ya kutoa maelezo hayo, kwa ruhusa yako, na kwa kuzingatia taratibu za Baraza lako tukufu sasa naomba kuwasilisha hatua zilizochukuliwa na serikali juu ya utekelezaji wa maazimio ya Hoja ya Mjumbe kuhusu kuweka miundombinu bora kwa watu wenye ulemavu katika majengo, barabara, makaazi, maeneo ya kupumzikia na maeneo mengine kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hatua kwa hatua tayari imeshaanza kutekeleza kwa vitendo masharti ya kifungu cha 12 na 13 cha Sheria ya Watu Wenye Ulemavu (Haki na Fursa) Namba 9 mwaka 2006, kwa kuweka miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu katika maeneo ya usafirishaji na majengo mbalimbali kama ifuatavyo:

Usafiri wa Baharini

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji suala la kuweka miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu limepewa kipaumbele na tayari mambo yafuatayo yameshafanyika:

Kwa upande wa gati ya abiria, wizara kupitia Shirika la Bandari imeweka njia maalumu, kwa ajili ya kupita watu wenye ulemavu katika sehemu ya kuingilia na kutokea bandarini. Aidha, katika maeneo ya gati ya abiria kuna viti maalum kwa ajili ya kuwahudumia watu wenye ulemavu wanaosafiri na wanaoingia nchini. Vilevile, upande wa gati ya mizigo, shirika limeweka njia maalum za kuingia na kutokea watu wenye ulemavu.

Meli nyingi zinazotoa huduma ya kusafirisha abiria zina miundombinu rafiki ya watu wenye ulemavu kama vile "*ramp*" ambapo watu wenye ulemavu huingia na kutoka melini bila ya usumbufu. Aidha, kwa meli zetu za serikali nalo suala hili limepewa kipaumbele ambapo watu wenye mahitaji maalum kabla ya kuingia kwenye meli husaidiwa kwa vifaa maalum yaani *wheel chairs* na ndani ya meli mazingira ni rafiki ikiwemo sehemu maalum zilizotengwa kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum ikiwemo watu wenye ulemavu.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kupitia Shirika la Bandari imeweka mikakati mbalimbali ya kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanapata haki na fursa ipasavyo. Miongoni mwa mikakati hiyo ni :

(i) Kuhakikisha njia za mawasiliano baina ya wenye meli na bandari zinaendelea kuimarishwa kwa ajili ya kutoa huduma kwa watu wenye ulemavu;

(ii) Kuendelea kuimarisha mashirikiano baina ya wafanyabiashara walemavu na Bandari kwa kupewa kipaumbele kwenye shughuli za kuingiza na kutoa mizigo bandarini;

(iii) Kuhakikisha miradi yote inayotekelezwa bandarini ina miundombinu bora kwa watu wenye ulemavu hasa majengo ya shirika.

Usafiri wa Anga

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa usafiri wa anga, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji tayari imeshaweka miundombinu katika maeneo yaliyoimarishwa ikiwemo eneo la kuondoka abiria wanaotoka ndani na nje ya nchi yaani *Domestic and International Departure* kwa kuwawezesha watu wenye ulemavu kusafiri bila ya usumbufu. Aidha, kwa upande wa jengo jipya la abiria *Terminal II* suala la kuweka miundombinu kwa watu wenye ulemavu limezingatiwa kwa kiasi kikubwa kwa kuweka huduma ya "*lift*" itakayowawezesha watu wenye ulemavu kufika katika maeneo yote ya jengo na kiwanja kwa urahisi zaidi.

Usafiri wa Barabara

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa usafiri wa barabara, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji tayari imeshaanza kuchukua hatua ya kuweka miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na uwekaji wa alama za barabarani hasa kwenye maeneo wanayokatisha waendao kwa miguu yaani *zebra crossing* kwa barabara ya Mwanakwerekwe – Fuoni. Aidha kwenye mradi wa ujenzi wa Barabara ya Bububu – Mahonda-Kinyasini hadi Mkokotoni, Pale, Kiongele, Matemwe, Muyuni na Fuoni–Kombeni suala la kuweka miundombinu na alama mbalimbali zikiwemo za watu wenye ulemavu limezingatiwa.

Kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018, Serikali kupitia Mfuko wa Barabara imetenga fedha kwa ajili ya kuweka alama 40 zote zikiwa ni za watu wenye ulemavu. Aidha, Wahandisi wa Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara tayari wameshawasiliana na Idara ya Watu Wenye Ulemavu, ili kupata ushauri kuhusu maeneo na aina ya alama zinazohitajika kuwekwa.

Hatahivyo, serikali inatoa angalizo kuwa mtu yeyote atakayeonekana anahujumu alama zilizowekwa barabarani atachukuliwa hatua za kisheria. Hivyo basi, naomba kila mwananchi awe mlinzi wa mwenzake na kutoa taarifa sehemu inayohusika kwa anaehujumu au kutotii alama zinazowekwa barabarani.

Vilevile, serikali kupitia wizara inayohusika na masuala ya usafirishaji imetoa kipaumbele kwa watu wenye ulemavu kwa kupata huduma bora za usafiri wa barabarani kwa kutayarisha kadi maalum katika kanuni za gari za biashara kwa ajili ya Watu wenye Ulemavu zitakazowasaidia kupata usafiri wa umma kwa kulipa nusu nauli.

Mhe. Mwenyekiti, wizara itaendelea kuweka miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu wa aina tofauti katika sekta ya usafirishaji, ili na wao waweze kupata huduma za usafiri kwa urahisi katika maeneo mbali mbali ikiwemo usafiri wa barabara, baharini na usafiri wa anga.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa majengo ya makaazi wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kupitia Wakala wa Majengo Zanzibar kwa kushirikiana na Idara ya Watu wenye Ulemavu pamoja na wataalamu wengine wa fani ya ujenzi walishiriki katika kutayarisha muongozo yaani "*Building Standards*" za majengo ambazo zitatumika kuwezesha majengo na maeneo mengine yaliyotajwa kuwa na mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu.

Muongozo huo umekamilika na Idara ya Watu Wenye Ulemavu imeshawasiliana na kuwasilisha kwa wadau mbalimbali kuhusu marekebisho yake yameshafanyika na kwa sasa tuko katika hatua za kukamilisha katika kikao cha Makatibu Wakuu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya muongozo huo kukamilika, katika kusimamia utekelezaji wake, serikali itatoa vitabu vya muongozo kwa wataalamu wote wanaohusika na utayarishaji ramani za majengo na viwanja vya burudani ambapo watawajibika kuufuata muongozo huo. Wajenzi wote wa majengo ya makaazi, maofisi au majengo yanayokusudiwa kutoa huduma kwa jamii watalazimika kufuata muongozo huo, ili tuweze kuwa na majengo yenye mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu. *(Makofi)*
Kwa upande wa utekelezaji na usimamizi wa muongozo huo, taasisi zinazotoa vibali vya ujenzi kama vile *DCU* na Halmashauri za Wilaya zitatakiwa kuhakikisha kuwa

Muongozo unatekelezwa kikamilifu. Vile vile, bodi zinazohusika na usimamizi wa ujenzi kama vile Bodi ya Wakandarasi na Bodi ya Usajili ya Wataalamu wa Ujenzi watapaswa kusimamia Muongozo huo na kuhakikisha viwango vinavyowekwa katika Muongozo huo zinafuatwa kikamilifu katika utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kupitia Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo inatoa maelelekezo na kuwataka wataalamu wote wa ujenzi wakiwemo wasanifu majengo, wahandisi wa ujenzi na watu wengine wanaohusika na usanifu na ujenzi wa majengo kuzingatia masharti ya Sheria ya Watu wenye Ulemavu wanapoanza kuandaa michoro yaani, *design stage* na kuhakikisha majengo mapya yanakuwa na miundombinu rafiki kwa Watu wenye Ulemavu.

Hatahivyo, wizara kupitia Bodi ya Usajili, Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo imeanza kuchukua hatua za kuangalia uwepo wa miundombinu rafiki ya watu wenye ulemavu kwenye michoro inayowasilishwa katika bodi, kwa ajili ya usajili wa miradi kabla ya kuanza ujenzi na wakati wa kufanya ukaguzi wa jengo kipindi cha ujenzi unapokuwa ujenzi unaendelea.

Shirika la Nyumba likiwa ni miongoni mwa taasisi zinazomiliki nyumba za kuishi na biashara hapa Zanzibar, itaweka umuhimu katika miradi yake mipya ya majengo ya biashara na makaazi kwa kuweka miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu itakayowezesha watu wenye ulemavu kutumia majengo yake bila ya usumbufu kwa kuhusisha ujenzi wa "*lift*", vyoo na huduma nyengine zitakazoweza kutumiwa na watu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa majengo yote ya zamani ambayo yamejengwa kabla ya kupitishwa sheria hii itakuwa ni gharama kubwa sana juu ya matengenezo ya kuweka miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu. Hatahivyo, baada ya kukamilika kwa muongozo wa uwekaji wa viwango vya majengo vitakavyotumika kuwezesha majengo na maeneo mengine kuwa na mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu, serikali itahakikisha majengo yote mapya yatakayojengwa baada ya kupitishwa sheria hii yatalazimika kuwa na miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu kwa kuzingatia sera, sheria na muongozo uliowekwa.

Hitimisho

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia, nachukuwa nafasi hii tena kwa kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii. Aidha nampongeza sana Mhe. Mohamed Said Mohamed, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Mpendae kwa kuwasilisha hoja binafsi kwa lengo la kuishauri serikali kuimarisha huduma zake kwa kuweka miundombinu bora kwa watu wenye mahitaji maalum ikiwemo watu wenye ulemavu. (*Makofi*)

Vilevile, nawashukuru wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kunivumilia na kunisikiliza kwa umakini wakati nikiwasilisha taarifa hii. Mhe. Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wako wote waipokee taarifa hii. *(Makofi)*
Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, Waheshimiwa Wajumbe taarifa tumeisikia na tumeipokea na kwa mujibu wetu wa kanuni yetu ya 44 kifungu (3) kinasema Mwenyekiti wa kamati au Mjumbe mwengine alieidhinishwa na kamati amepewa nafasi ya kutoa maoni kwa niaba ya kamati kuhusiana na taarifa hiyo ya serikali.

Kwahivyo, namwita Mwenyekiti wa Kamati kama ana maoni yoyote ya Mawasiliano aweze kuja kutoa maoni yake. Ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano): Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kunipa nafasi hii kwa kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa kutumia kanuni ya 44 (3) kama inavyoeleza kanuni zetu za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, nasikitika sana kusema kwamba Afisi yako haikuitendea haki kamati yangu ya Ardhi na Mawasiliano. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni zetu taarifa yoyote inayotoka serikalini inatakiwa Katibu wa Baraza au Spika wa Baraza la Wawakilishi taarifa ile aiwasilishe kwa kamati na kamati iweze kujadili na kuichambua halafu ije itoe maoni kwenye Baraza la Wawakilishi. (*Makofi*)

Kwahiyo, kwa kutetea heshima ya Waheshimiwa Wajumbe wa kamati walionichagua kama Mwenyekiti naomba kiti chako Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii leo tuakhirishe ili uiagize kamati yako ikae ipitie halafu ije itoe maoni. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, itakuwa sio haki mimi kama Mwenyekiti nikatoa maoni ya kamati bila ya kuwashirikisha wenzangu. (*Makofi*)

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ripoti zinazokuja hapa kuna Ahadi za Serikali lakini vile vile kuna *commitment* ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kusimamia serikali katika yale ambayo iliyoyaahidi. Sasa Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kwamba ilikuwa ni hoja binafsi, lakini kwa kuwa ripoti iliyojibiwa imejibiwa na serikali mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, kama ulivyosoma kanuni ya 44 (3) basi ni vyema tuitendee haki ripoti hii ili tutakachokishauri Mhe. Waziri na yeye aje aridhike na ule ushauri wa kamati.

Mhe. Mwenyekiti, naomba tena kiti chako kwa heshima kubwa ili kulinda kanuni zetu, basi naomba Mhe. Mwenyekiti, hii ripoti tuipokee halafu ikabidhi kamati yako ifanyie kazi na tunakuahidi kesho tukijaaliwa au jioni tunaweza tukakaa na kamati tukaweza kuiwasilisha ili sasa serikali iende ikaifanyie kazi. Mhe. Mwenyekiti, naomba muongozo wako. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano. Mimi ningekushauri kwa vile wewe ni Mwenyekiti na hoja imeshasikilikana Baraza au uongozi wa Baraza umeshasikia ni vyema wewe uchukue fursa hii kutoa maoni yako, hivyo kama kuiwakilisha kamati na baadae tuweze kutoa hoja wananchi Wajumbe waweze kuichangia kama utaridhika na hili. Nakuomba sana ufanye hivi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako bila ya kukiuka kanuni ya 44 (3) nikisema hapa ninaweza kutoa mchango wangu kama Mwakilishi wa

Jimbo la Shaurimoyo. Lakini sitoweza kutoa maoni kwa niaba ya kamati. Sasa kama utanikubalia nitoe maoni yangu kama Mwakilishi wa kawaida nitatoa maoni yangu, lakini sitotoa maoni kwa niaba ya kamati na huo ndio utaratibu wetu wa Baraza. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe nimekuona lakini na hii kanuni inasema wewe utoe kwa niaba ya Wajumbe sio lazima kwamba Wajumbe wote wakae waijadili hii kamati. Wewe kanuni imekupa nafasi kwa niaba ya Wajumbe. (*Makofi*)

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana na nikupongeze sana kwa kiti chako kuwa makini sana. Lakini kuendelea kumwambiwa Mjumbe atoe maoni kwa mujibu wa kamati tutakuwa tunavunja kanuni yetu hiyo hiyo. Kwa sababu kanuni ya 44 (iv) ndiyo inamuelekeza Mjumbe kutoa maoni yake si maoni ya kamati.

Kwahiyo, ni vyema kuirudisha kwenye kamati kama utakuwepo muda jioni basi tuweze kuendelea. Laa kama haupo jioni basi tunaweza kuendelea kesho baada ya masuala na majibu ili tuone maoni ya kamati. Maoni ya kamati ndio yanayowakilisha wananchi wote. Kwahiyo, Mhe. Mwenyekiti, nikushauri tu uirudishe kwenye kamati na kesho tuweze kuisoma au jioni. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante wacha tumsikile Mnadhim hapa naye ataweza kutoa Mhe. Waziri Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais aweze kutoa ufafanuzi wa suala hili. (*Makofi*)

Mhe. Waziri Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti,

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, utulivu. Waheshimiwa Wajumbe tuisikilize serikali itasema nini.

Mhe. Waziri Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hii ilikuwa hoja ya Baraza naomba nisome kifungu cha 47 cha Kanuni zetu halafu tutaendelea na kifungu (1) na (2) ili kutusaidia katika kufanya maamuzi.

1) Shughuli za kawaida za Baraza zitatekelezwa kwa njia ya hoja na maagizo mengine yatakayokuwa yamewekwa katika orodha ya shughuli.

2) Shughuli za kawaida zitaanza kwa wakati Spika atakapomwita Mjumbe wa kwanza aliyetoa taarifa ya kutoa hoja mwanzoni mwa shughuli za Baraza au kumwita Mjumbe anaehusika na hoja ya kwanza iliyoko mwanzoni mwa shughuli, au atakapomwita Katibu wa kusoma orodha shughuli.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hoja hii ilikwisha amuliwa na Baraza na ikawe kama Azimio na serikali ikaleta hiyo taarifa ya Maazimio ambayo yametakiwa yaletwe ya Baraza. Sasa haikupaswa kwenda kwenye kamati ni utaratibu wa kawaida sasa kuliongoza Baraza lako, ili kupata majibu ilihitaji Mwenyekiti atoe maoni yake sawa akitaka mwenyewe aliewasilisha taarifa hii ya hoja binafsi aseme sawa au kama Wajumbe wana jambo wataweza kuchangia. Haya ndio majibu yetu yameridhika yanakasoro na kadhalika utatueleza. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri ameshatoa ufafanuzi nadhani ufafanuzi wake ni mzuri sana na ni vyema tuupokee na tuufanyie kazi. Kwa hivyo, kwa mujibu wa kanuni alivyoisoma maelekezo yameweka bayana kitu hichi ni vyema tufuate muuongozo wa Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili ya Rais kama alivyotuelekeza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mohamed Said Mohamed nimekuona

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Nimemruhusu Mhe. Mohamed Said Mohamed.

UTARATIBU

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa heshima kubwa naomba sasa tusome Kanuni ya 48 falisi ya (3). Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu.

Kanuni ya 48(3) inasema hivi:-

> "mtoa hoja yoyote awe waziri au ni mjumbe mwengine yoyote anaweza kuomba hoja yake ipelekwe moja kwa moja katika Baraza au ipelekwe kwenye kamati inayohusiana na hayo".

Mhe. Mwenyekiti, kanuni inatuelekeza hivyo na mimi ndio niliyekuwa nimetoa hoja na lakini na serikali imeleta majibu lakini kilichokosekana ni utaratibu wa hoja ile serikali kutoipeleka kwenye kamati. Sasa naomba tutumie kanuni hiyo tuirudishe kwenye kamati ili ijadiliwe na kamati itowe maoni yake kwa ufasaha zaidi, ili basi wananchi au wale ambao tuliowawakilisha hapa wawe na muda mzuri wa kupata maoni ya kamati pamoja na majibu mazuri sana ambayo Mhe. Waziri ameyatoa, ningekushauri sana Mhe. Mwenyekiti tuirudishe kwenye kamati ili basi tuweze kuijadili tena hoja hii.

Mhe. Mwenyekiti: Nimekusikia Mhe. Mjumbe lakini pia hii kanuni inasema sio lazima irudishwe kwenye kamati lakini mjumbe anapewa nafasi ili aweze kutoa maoni yake baadae wananchi wajumbe nao watapata nafasi ya kuweza kuichangia hoja hiyo tumekubaliana Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mjumbe alileta Hoja Binafsi na hoja ikajadiliwa, Baraza likapitisha maazimio ili serikali ilete majibu, serikali imeleta majibu, Baraza lina uwezo wa kuyakubali majibu yetu au kuyakataa haya majibu yetu hayapwasi kwenda kwenye kamati, kwa sababu ni maazimio ya Baraza la Wawakilishi sisi mumetupa kazi tukaifanye majibu yetu ndio haya. Kwa hivyo, muyakubali au tuyakatae Mhe. Mwenyekiti naomba kusema hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mgeni Hassan Juma.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nachukua fursa hii kuwapongeza wote wale ambao wametoa hoja kwa mujibu wa kanuni, na ni kweli kwamba kanuni zetu zinasema kwamba Kanuni ya 44(3), naomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

Kanuni ya 44(3) inasema hivi:-

> Mwenyekiti wa Kamati anayehusika na mjumbe mwengine anayeidhinishwa na kamati atapewa nafasi ya kutoa maoni kwa niaba ya kamati.

Kanuni ya 44(4) inasema hivi:-

> "Mjumbe anaweza kujadili na kutoa maoni kuhusina mjumbe wowote wa Baraza la Wawakilishi".

Mhe. Mwenyekiti, huu usiwe mzozo wa kuendelea kupoteza muda wetu, nashauri isomwe kuna taarifa nyengine isomwe baada ya hapo ripoti hii ipelekwe kwenye kamati, mwenyekiti arudi tena hapa sasa tuanze kujadili nashauri kwamba isomwe kuna taarifa nyengine ambayo inatakiwa isomwe irudi halafu itajadiliwa hapa ndani ya Baraza baada ya kamati kujadiliwa ahsante mwenyekiti.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe nimekusikia maoni yako na sasa Waheshimiwa Wajumbe maoni tumeyasikia mbali mbali na maoni ya mwisho ni vyema tuyachukue kwamba hili suala kwanza tuliwache na baadae tuendelee na hii hoja nyengine, ili kama kutakuwa kuna ulazima hasa basi tutairudisha kwenye kamati lakini ufafanuzi ushatolewa vifungu vyote hapa wajumbe tunaweza kuchangia kwa nafasi ambayo kuwa imewekwa kwa mujibu wa kanuni.

Kama kamati haikotoa maoni wajumbe wamepewa nafasi kwa hivyo, tusipoteze muda ambayo kuwa tuna mambo mengine ya kujadiliwa naomba sasa tukubaliane kwa hilo Waheshimiwa Wajumbe. Kwa hivyo, hoja hii tunaiweka kwanza tunaiwacha na sasa nitamwita Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo, na Uvuvi, ili aweze kuleta taarifa ya serikali, Mhe. Waziri karibu sana.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti,kwa ruhusa yako kwanza naomba kukushukuru kwa kunipa fursa hii, pili naomba Baraza lako kupokea taarifa ya serikali juu ya hoja binafsi iliyotolewa na Mhe. Mohamed Said Mohamed kama ifuatavyo….

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, naomba utulivu kidogo, Mhe. Waziri subiri, Waheshimiwa Wajumbe utulivu Mhe. Waziri anasoma taarifa, Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti eneo la chijio la Kisakasaka, lina ukubwa wa ekari 100 ambapo ekari 90 zimetengwa kwa ajili ya karantini na ekari 10 zimetwengwa kwa ajili ya ujenzi wa chinjio la kisasa. Chinjio dogo la Kisakasaka lilianzishwa baada ya kuhamishwa lilikokuwa chinjio kuu hapo Gulioni ambapo hivi sasa ndipo lilipo jengo la *ZSTC*, jengo hili kiasili lilikuwa ni nyumba ya makaazi ambayo ilibadilishwa matumizi yake ili kuziba pengo la ukosefu wa chinjio, katika Mkoa wa Mjini Magharib.

Chinjio la Kisakasaka, halikidhi haja hasa ukizingatia mahitaji wa uchinjaji wa kisasa kwa kukidhi haja ya kuuza nyama katika mahoteli ya kitalii na hata kusafirisha nyama nje ya nchi ambapo Wizara iliwasilisha *ZIPA* michoro ya chinjio la kisasa kwa lengo la kutafutiwa wafadhili kwa kusaidia ujenzi wake. Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imepokea barua kutoka *ZIPA* inayotujulisha ya kwamba wawekezaji kutoka Japan wameonesha nia ya kujenga chinjio la kisasa na watakuja Zanzibar hivi karibuni, ukiangalia liambatisho namba 1 ambapo Halmashauri husika tayari imeshajulishwa.

Chinjio hili ni pekee ambalo lililokuwa likimilikiwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo, na Uvuvi hapa Unguja, chinjio la Kisakasaka limegatuliwa na hatimae karibuni litakabidhiwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Magharib B Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Aidha, ukusanywaji wa mapato yake kila siku, na ukaguzi wa nyama unafanya na mamlaka ya chakula na madawa chini ya Wizara ya Afya, chini ya wataalamu wa mifugo na pia kukusanya mapato yanayotokana na ukaguzi wa nyama kwa kila siku. Hivyo, kuhusu mgawanyo wa mapato wa kijiji ni hoja inayopaswa kujadiliwa na wamiliki wa chinjio hilo ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Magharib B na uongozi wa Shehia ya Kijiji.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi inakusanya mapato yanayotokana na eneo la kantini ya mifugo ambayo hupokea mifugo kutoka nje ya nchi ikiwa ni chanzo cha mapato ya serikali, mapato ya karantini ya mifugo inayoingizwa Zanzibar yanapelekwa hazina moja kwa moja kila mwezi. Kwa mnasaba huo ni vyema ombi hili likapelekwa katika taasisi husika zinakusanya mapato hayo. Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri, taarifa imesikilikana sasa tusubiri kidogo, katibu menzani endelea.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, naomba muongozo wako.

MUONGOZO

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Hoja imetolewa lakini hatujaweza kujadili wala kusema chochote na kwa sababu hio basi maombi ya wananchi yatakuwa ndio yamekwenda hewani ningekuomba sana kiti chako, kiweze kuwaruhusu wajumbe angalau waseme chochote au mimi mtoa maoni au mleta maombi kwa niaba ya wananchi wa Kisakasaka, niseme chochote kuhusu *petition* ambayo nimeweza kuileta mbele yako na majibu haya hayakutosheleza nimeyaona. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo, Mhe. Mohamed Said Mohamed nimekusikia na *petition* imeshatolewa hii, tumesikia sote tumewakilishiwa hapa. Sasa ni vyema mwenye kutoa *petition* au ombi hili na wewe ukatoa taarifa yoyote na baadae tukaendelea na kitendo kinachofuata mbele yetu. Mhe. Mohamed Said Mohamed endelea.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, niendelee kukushukuru sana, lakini nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa jibu lake zuri sana alilolitoa kwa wananchi wa Kisakasaka. Lakini niseme tu maombi haya

ya wananchi wa Kisakasaka yalizingatia kuletwa kwenye Baraza lako tukufu na serikali kuyafanyia kazi. Sasa kama leo Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi anazungumza, kuwa mambo haya au maombi haya yapelekwe kwenye halmashauri husika, na kifungu cha 43(5) serikali yote ipo kwa pamoja kwenye Baraza la Wawakilishi.

Kwahivyo, si vyema kuona na kusema maombi haya yapelekwe pale wakati maombi yameletwa kwenye Baraza la Wawakilishi na serikali na waziri yupo mwenye kushughulikia Tawala za Mikoa na wala kwenye kamati sidhani kama imepita. Sasa jambo hili linaanza kutupa ukakasi mkubwa sana, walasiwezi kuona mbele kwa serikali yangu, kuona jambo hili haliwezi kujibiwa hapa la wananchi wa Kisakasaka.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wa Kisakasaka walileta maoni yao, walileta maombi yao kwa serikali yao, lakini leo wanaambiwa warudi kwenye halmashauri sio vyema. Tuombe serikali ipo kwa pamoja, waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mkoa yupo, lakini kama hayupo yupo Mnadhimu wa Serikali kama ulivyomwita, lakini sasa hatuna kwenye Baraza hili. Kwa hivyo, naomba sana maombi haya ya wananchi hawa yashughulikiwe, na hichi kitu tulichoambiwa *ZIPA* imepelekewa, *ZIPA* imefanya nini hiki ni kigugumizi wala hakiendi popote. Hivyo, tunawaomba sana yashughulikiwe matatizo ya wananchi wa Kisakasaka. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, barabara yao mbovu. Ukipita Mhe. Mwenyekiti, nitakuchukua uende ukaone, hakuna miundombinu yoyote katika kijiji kile, tabu sana. Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru. *(Makofi)*
Mhe. Mwenyekiti: Ahsante. Mhe. Mjumbe, nimekusikia na kwa vile ...

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, kuhusu utaratibu.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mjumbe yeye hakuuliza halmashauri, halmashauri anaijua. Kaiuliza serikali ndani humu na serikali inawajibika kujibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, taja kanuni unayozungumza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, Kanuni ya 37. *(Vicheko/Makofi)*

Mjumbe halmashauri anaijua, yeye kaiuliza serikali ndani na serikali ina wajibu wa kujibu humu ndani, hakuuliza Kwamtipura wala hakuuliza Paje.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, Mhe. Mjumbe nimekusikia. Mhe. Mnadhimu wa Serikali yupo na ataweza kutoa maelezo zaidi. Au Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ataendelea kutoa maelezo zaidi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimshukuru sana Mhe. Mohamed Said Mohamed, kwa kuleta hoja ya wananchi wa Kisakasaka. Nataka nikiri kabisa kwamba amefanya kazi

yake ya uwakilishi ya kuweza kuwatetea wananchi na ndio wajibu wa mwakilishi yeyote.

Pili, Mhe. Mwenyekiti, tukumbuke tu Baraza hili lilipitisha sheria ya kuanzisha utaratibu wa kukagua madaraka ya serikali. Ugatuzi maana yake tunawapelekea wananchi mamlaka yao chini, Baraza hili lilipitisha sheria kwa kufanya hivyo halikufanya kwa kubahatisha. Kwa hivyo, yako mambo yataamuliwa na Serikali za Mitaa, yako mambo yataamuliwa na Serikali Kuu, huu ndio utaratibu ambao tumejipangia ndani ya Baraza letu. Kwahivyo, jambo hili na kwasababu wawakilishi wangependa serikali iamuwe.

Sasa naomba Mhe. Mwenyekiti, Baraza lako liridhie tu tulichukuwe tena serikalini tukalifanyie kazi, halafu turudishe majibu kwa ule utaratibu wa kawaida. Lakini nasema utaratibu wa kiserikali upo wa wananchi kushughulikiwa matatizo yao nchini. Kwahiyo, kama Baraza linafikiria ni vizuri tukalifikiria juu huku, basi mimi nafikiria tulichukuwe tulipeleke tutakaa na wenzangu wa Serikali za Mitaa, ili tuone ni kiasi gani tunaweza tukalitatua hili tatizo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri. Naam Mhe. Hamza Hassan Juma endelea.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimshukuru sana tena sana Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kama Mhe. Waziri alivyotoa hii hoja na mjengo hoja mwenyewe, mleta petition mjumbe makini sana Mhe. Mohamed Said Mohamed, kusema kwamba hajaridhika na ripoti hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia nampongeza sana Mhe. Mohamed Said Mohamed, lakini uamuzi au ushauri alioutoa Mhe. Waziri, nafikiri huu ndio ushauri wa busara, kwasababu kweli tumepitisha sheria ya Serikali za Mitaa kuleta ugatuzi katika halmashauri zetu mbalimbali. Lakini tuangalie Mhe. Mwenyekiti, chinjio hili la Kisakasaka sio kila wilaya inaweza kuanzisha chinjio, hili ni chinjio la kitaifa. Mifugo yote inayotoka nje haturuhusiwi sisi katika maeneo mengine kuchinja wanyama kama hawa. Kwa kweli, pale kwanza wanaingia wanawekwa kwenye karantini wanachunguzwa, serikali ikihakikisha kwamba wanyama hawa wako salama hawawezi kuleta athari yoyote kwa jamii, basi ndio pale serikali inatoa kibali kwa ajili ya kuleta machinjio haya. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa kusema tunaziachia tu halmashauri. Halmashauri wache wakachinje ng'ombe waliokuweko mitaani au mashambani, lakini waliotoka nje ya nchi, mimi nadhani hoja ya Mhe. Mohamed Said Mohamed ya kuwekwa miundombinu mizuri kule Kisakasaka, vilevile na wananchi wakawekewa *guarantee* maalum ya afya zao, kwasababu ile mifugo inapoingia sio kama tunahakikisha kila pahala imesha kaguliwa, inakuja kukaguliwa pale, inawezekana kuna baadhi ya maradhi yakaja kuanza kuenea pengine kabla ya ile nyama kuchinjwa.

Kwakweli, napongeza sana ushauri wa Mhe. Waziri, na sisi kama wajumbe wa Baraza, naomba tukubaliane na ushauri wa waziri, ili waende wakakae serikalini waangalie. Nafikiri hii hoja ya Mhe. Mohamed Said Mohamed itasaidia kuweza kuboresha ile miundombinu kule Kisakasaka, ili sasa hata wale ambao wenye

mahoteli na wengine wanaonunua nyama ambayo inachinjwa Kisakasaka, watakapokwenda pale watajiridhisha, isijekuwa kama chinjio lililokuwa la kuku pale Marikiti ya Darajani, ambapo ilikuwa utadhani labda wale kuku pengine walasitaki kusema mambo mengine ambayo tutakuwa tunajikashifu sisi wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, napongeza sana na naomba hii ripoti Mhe. Waziri aichukuwe tena arudi nayo akakae. Vilevile, naomba Mhe. Mwenyekiti nafikiri wangeunda hasa timu ndogo wakaenda kukagua, hayo aliyoyazungumza Mhe. Mohamed Said Mohamed. Je, kweli haya yaliyozungumzwa miundombinu hairidhishi, hali hii hairidhishi. Baadaye naamini watakuja na mpango hasa katika ugatuzi, halmashauri watawapa kazi yao kwa ajili ya kuweka miundombinu, lakini bado lile eneo litakuwa ni eneo la kitaifa, ambapo mifugo yote inayotoka nje itakuwa inafikia pale na baadae itaingia mitaani.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kukubali na kuwashawishi wajumbe wenzangu tuikubali hoja ya Mhe. Waziri, ili aende akaifanyie kazi tena, naamini waziri huyu makini sana atatuletea ripoti ambayo itaturidhisha na sote tutaridhika. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia nimuombe waziri. Mhe. Waziri ni hodari sana wa kuhangaika na kutafuta misaada mbalimbali, basi hebu liingize katika mradi lile chinjio ili liwe chinjio la kisasa, ili watu waige mfano. Leo wizara hii hii tayari kuna soko ambalo wametujengea pale Kinyasini sio kuzuri sana, leo ukienda Malindi kuna soko zuri sana. Sasa nitashangaa sana Mhe. Waziri katika mipango yeke kama atashindwa kuliingiza Chinjio la Kisakasaka kuliwekea miundombinu iliyo bora, ili na sisi Zanzibar tuingie katika hiyo karne ya watu ambao wanaojali afya ya watu wao. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hamza Hassan Juma. Nampa fursa tena Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kuhusu taarifa.

TAARIFA

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Taarifa tu Mhe. Mwenyekiti. Kwanza nataka nimshukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma kwa maelezo mazuri sana na yenye ufasaha, tena ni swahiba wangu. Nilitaka nitoe ufafanuzi tu.

Mhe. Mwenyekiti, karantini ni jukumu la Serikali Kuu, machinjio kila wilaya ina uwezo wa kuwa na machinjio yake na ndio maana ukienda Kaskazini, hivi karibuni tu nilikwenda kufungua machinjio mazuri tu, sehemu ya karantini ni jukumu la Serikali Kuu na ndio maana hata pale Kisakasaka ng'ombe wakiingia kwanza suala la karantini linasimamiwa na Serikali Kuu yenyewe, yaani wizara. Machinjio yote tulikubaliana kabisa kwamba kila wilaya kuwe na machinjio mazuri ya kisasa kama tulivyofanya kwenye masoko ya samaki.

Kwa hivyo, nataka niwaahidi Waheshimiwa Wajumbe, *exercise* au utaratibu wa halmashauri kushughulikia machinjio yao kwa maeneo yao ni wajibu wao na sisi kazi yetu ni kutoa wataalamu. Sisi kazi yetu ni kuanzisha karantini, tunayo ya Kisakasaka na Kaskazini Pemba tayari tumeshafungua nyengine, huu ndio utaratibu wa serikali. Mhe. Mwenyekiti, ng'ombe wote wanaotoka nje kwanza wanakaguliwa na Serikali

Kuu, halafu watu wa machinjio wanaruhusiwa kuchukua. Nilitaka niweke hili *clear* ili watu wasichanganye mambo mawili ni tofauti. Buku moja linashughulikiwa na Serikali Kuu kwamba chochote kinachoingia ndani ya nchi ni wajibu wa Serikali Kuu, na ndio wizara yangu inalisimamia hili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa machinjio ya wilaya tunaendelea kuyajenga kuwasaidia halmashauri ili yamilikiwe na wananchi wenyewe kuhusu zana na mahitaji wanayohitaji. Nilitaka niliweke hili *clear.* Nataka nimuhakikishie Mhe. Mjumbe na tena nimshukuru sana Mhe. Mohamed Said Mohamed, juzi wameleta wawekezaji katika wawekezaji waliowaleta miongoni mwao walikuwa na *interest* ya kuendeleza machinjio haya ya kisasa. Mimi nafikiri wanafanyakazi nzuri na hiyo kazi tutafanya kwa uadilifu mkubwa sana. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu taarifa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Machano Othman Said, nimekuona kuhusu taarifa.

TAARIFA

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Mimi nilitaka kutoa taarifa tu kwamba, pamoja na kuwa Kisakasaka kuna chinjio kubwa, lakini na Halmashauri ya Kaskazini B wana machinjio mawili. Moja Mahonda na wanalo jengine la kisasa Mwanda ambalo pia linapokea ng'ombe kutoka Tanzania Bara na wana sehemu ya kuweka karantini. Kwa hivyo, mkizungumzia machinjio nafikiri halmashauri ndio wenyewe.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Kuhusu utaratibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kifungu 59(3). Mpaka aniruhusu kule mwenyekiti, tunaongozwa na sheria sisi na kanuni.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mohamed Said Mohamed Dimwa alipoleta hii hoja, hakuleta juzi wala jana. Leo Mhe. Waziri anamuambia arudishe serikalini, yaangalie hayo maelezo ya 59(3) kaileta serikalini lini, halafu yarudishwe serikalini, kwa maana hiyo alipoleta haikuletwa serikalini ile hoja imepelekwa wapi. Alipoleta Mhe. Mohamed Said Mohamed hoja alileta serikalini ninavyojua mimi, leo irudi tena serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, chombo hiki kinaongozwa kwa kanuni na kanuni ndio hizi mlizotupa. Kweli Mhe. Mohamed Dimwa ndio tunamfanyia haki. Imekwenda serikalini halafu inarudi tena serikalini tunafanya nini, *we serious*.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nimekusikia kaa kitako. Haya ni makubaliano. Mhe. Mjumbe, waziri amekubali kuweka sawa mambo yaliyotakikana. Kwahivyo, na wajumbe naomba mridhike na hilo, waziri inarudi ili kwenda kuiweka sawa vizuri na yeye baadae ataweza kuona taarifa ambayo italetwa mbele yetu tuweze kuifanyia kazi.

Kwa hivyo, sasa tunaendelea hili jambo limeshachukua muda mrefu, tunaendelea. Naomba Waheshimiwa Wajumbe, tuwatambue wageni wetu wa leo hapa, ambao ni kutoka kwa Mhe. Spika. Ndugu Ramadhan Issa Abdalla ni Mkurugenzi wa Ofisi ya Bunge Zanzibar, Ahsante sana karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, wageni wengine ni wa Mhe. Ali Salum Haji ni Mnadhim na ni Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani. Jumla ya wageni hao ni 20, ni Wajumbe wa Jumuiya ya Wazazi wa Jimbo, wakiongozwa na ndugu Ali Yussuf ni Mwenyekiti wa Wazazi wa Jimbo, na Awadh Haji Hassan ni Katibu Mwenezi, na ndugu Salama Saleh Wema ni Katibu Malezi na Elimu. Hawa jumla yao ni 20, nitawaomba wasimame kwa pamoja ili kuweza kusalimia. Ahsanteni karibuni sana.(*Makofi*).

Waheshimiwa Wajumbe, wageni wengine wa leo ni wa Wawakilishi wa Viti Maalum Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, Mhe. Zaina Abdalla Salum, Mhe. Amina Iddi Mbarouk, Mhe. Hamida Abdalla Issa na pia Mhe. Lulu Msham Khamis. Wageni hawa kutoka Uongozi wa *UWT* Mkoa wa Magharibi kichama, jumla yao ni 16. Naomba wasimame kwa ujumla wao kwa sababu ni 16 hapa wakiongozwa na Zainab Ali Maulid ni Mwenyekiti wa Mkoa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, wengine ni wageni wa Mhe. Mohamed Said Mohamed Dimwa Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae, hawa ni wananchi wa Kisakasaka jumla yao ni 7, naomba ni wataje. Kwanza ni ndugu Hassan Hamad Hashim, ndugu Rajab Idrissa Mwinyi, Juma Makame Mwadini, ndugu Simai Zaidi Mussa, ndugu Asha Rajab Maulid, ndugu Amina Thabit Chum na wa mwisho ni ndugu Fatma Ali Pandu. Karibuni nyote katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, wengine ni wageni wa Mhe. Masoud Abrahman Masoud wa Jimbo la Bububu. Hawa ni viongozi wa Kamati ya Siasa na *Secretariat* ya Jimbo la Bububu, jumla yao ni 12 wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Jimbo ndugu Yumenk Kibwana Nzuki, akifuatiwa na ndugu Mohammed Ali Waziri ni Katibu. Wengine hawa wote wafuate kwa pamoja ili waweze kusimama kwa pamoja ni Wajumbe wa *Secretariat* ya Jimbo la Bububu wote wasimame. Ahsanteni karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea. Sasa namwita Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ili aweze kuwasilisha hoja. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango karibu sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako hili tukufu kwa mara ya kwanza, Mapendekezo ya Mwelekeo wa Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Mwelekeo wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuanza kuwasilisha, naomba uniruhusu nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa maelekezo yake katika usimamizi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo na bajeti ya serikali. Pia naomba nimshukuru Makao wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi kwa usimamizi mzuri wa Utekelezaji wa majukumu ya serikali. Nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu

na Watendaji wote wa wizara zote kwa mashirikiano mazuri yaliyopelekea kupata mafanikio makubwa kwa mwaka 2016/2017 na nusu ya kwanza ya mwaka 2017/2018. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwakweli Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti Mhe. Mohammed Said Mohammed, na Makamu wake pamoja na wajumbe wa Kamati ya Bajeti ninawashukuru kwa dhati kabisa kwa nzuri wa kupitia mpango huo ninaouwasilisha mbele ya Baraza na kwa mashirikiano yao mazuri na wizara zetu.*(Makofi)*
Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa michango waliotupatia Kamati ya Bajeti ni kama ifuatavyo:

1. Walitaka haja ya kuwa na vipaumbele vichache kwa maeneo maksusi;

2. Walizungumzia suala la miradi ya Maendeleo kuwepo na maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa miradi hiyo;

3. Katika sekta ya uchumi walitaka kilimo kiimarishwe katika maeneo yote hususan umwagiliaji maji upatikanaji wa pembejeo na mbegu bora, lakini katika sekta ya utalii walisisitiza sana haja ya kuwa na takwimu sahihi za ziimarishwe na ziwe na uchambuzi wa kina. Kamati ya Bajeti pia ilizungumzia suala la deni la taifa na wakataka uwepo uchambuzi wa kina pamoja na uhususiano deni na dhima ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

4. Mhe. Mwenyekiti, kamati pia ilizungumzia suala la utekelezaji wa bajeti na kusema kwamba malengo ya mapato yawe na uhusiano unaokwenda na uchumi;

5. Lakini pia waligusia suala la ajira kwa vijana na kutaka liwe na mikakati ya uhakika na itekelezwe kwa ukamilifu; na

6. Pia walizungumzia suala la zao la karafuu wakaeleza haja ya kueonekana manufaa kwa wananchi kwani pesa nyingi zinatumika kununulia karafuu hizo.

7. Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti pia ilizungumzia suala la kufanyika mapitio ya mfumo wa kodi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza kwamba maoni haya ya kamati, wizara yameyachukua na itayafanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, mapendekezo haya yanatokana na matakwa ya Sheria ya Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016, kifungu cha 39 (1)-(3), vinavyomtaka Waziri anayehusika na masuala ya fedha kutayarisha na kuwasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi Mapendekezo ya Kijumla ya Mwelekeo wa Uchumi, Mpango na Bajeti *(Budget Framework Paper)* kwa mwaka unaofuata. Baraza la Wawakilishii lina wajibu wa kuyapitia mapendekezo haya, kuyajadili na kuyakubali pamoja na kuruhusu utekelezaji wake utakaopelekea kutayarishwa na kuwasilishwa kwa Mswada kamili wa Mpango na Bajeti katika Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, Kabla ya kuanza na Mkabala huo, naombwa uniruhusu nieleze kwa muhtasari Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2017, Mpango wa Maendeleo

na Bajeti kwa mwaka 2016/17 pamoja na Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa nusu mwaka ya 2017/18.

Taarifa ya Mapitio ya Hali ya Uchumi, 2017

Hali ya Uchumi Duniani

Uchumi wa Dunia

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi Duniani, uchumi wa dunia umekua zaidi katika kipindi cha nusu mwaka (January – June) 2017 kwa kasi ya ukuaji wa wastani wa asilimia 0.3 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 0.1 katika kipindi kama hicho 2016.

i. Kwa nchi zilizoendelea kasi ya ukuaji wa uchumi iliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 0.5 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 0.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2016.

ii. Kwa nchi zinazoibukia kiuchumi ukuaji ulifikia wastani wa asilimia 0.8 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 0.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2016.

iii. Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 0.4 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 0.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2016.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi hicho, kasi ya mfumko wa bei duniani ilikuwa na sura tofauti kama ifuatavyo:-

a. Nchi zilizoendelea kasi ya mfumko wa bei imepanda hadi kufikia asilimia 1.7 kutoka asilimia 0.8 kwa kipindi cha miezi sita mwaka 2016.

b. Kwa nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi kasi ya mfumko wa bei imepungua kufikia wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2017 kutoka wastani wa asilimia 4.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2016.

c. Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara kasi ya mfumko wa bei imepungua hadi kufika asilimia 11 mwaka 2017 kutoka asilimia 11.3 kwa kipindi kama hicho mwaka 2016.

Ukuaji wa Uchumi wa Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, Katika kipindi cha (Januari – Machi) mwaka 2017, uchumi wa Zanzibar ulikuwa kwa kasi ya asilimia 6.3 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.0 kwa kipindi kama hicho mwaka 2016. Ukuaji huo umechangiwa zaidi na Sekta za Huduma, Viwanda na Kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha robo mwaka ya pili (Aprili –Juni) mwaka 2017, uchumi umekua kwa kasi ya asilimia 8.2 ikilinganishwa na asilimia 8.8 kwa robo mwaka ya pili 2016.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2017, kasi ya mfumko wa bei za bidhaa na huduma nchini imeshuka hadi kufikia wastani wa asilimia 5.6 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.7 mwaka 2016. Kushuka huko kumesababishwa na kushuka kwa mfumko wa bei za bidhaa za chakula. Mfumko wa bei wa bidhaa zisizo za chakula, kasi yake imepanda na kufikia asilimia 5.6 mwaka2017 kutoka asilimia 4.8 mwaka.

Aidha, katika kipindi cha nusu mwaka (Januari – Juni) 2017 shilingi ya Tanzania imeendelea kuwa imara sawa ikidhihirika kwa punguzo dogo la thamani la asilimia 0.26 ilipobadilishwa dhidi ya dola ya kimarekani kwa wastani wa shilingi 2,231.2 kutoka wastani wa shilingi 2,225.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2016.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha Januari-Juni 2017 uingiaji wa watalii umeongezeka kwa asilimia 18.6 kutoka watalii 143,851 mwaka 2016 kufikia watalii 170,581 katika kipindi kama hicho mwaka 2017. Watalii wengi waliotembelea Zanzibar walitoka nchi ya Italia, Uingereza, Ujerumani na Israel.

Mhe. Mwenyekiti, thamani ya uagiziaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 31.8 kutoka shilingi 143.2 bilioni mwaka 2016 kufikia shilingi 188.7 bilioni (Januari – Juni) mwaka 2017. Aidha thamani ya usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi imeongezeka kwa asilimia 41.1 kutoka shilingi 46 bilioni mwaka 2016 kufikia shilingi 64.9 bilioni (Januari- Juni) mwaka 2017. Hatahivyo, kasi kubwa ya ukuaji wa uingizaji dhidi ya ile ya usafirishaji imepelekea kuongezeka kwa nakisi ya biashara kwa asilimia 27.4 kutoka nakisi ya jumla ya shilingi 97.2 bilioni mwaka 2016 kufikia jumla ya shilingi 123.8 bilioni (Januari - Juni) mwaka 2017.

Uwekezaji binafsi kupitia *ZIPA*

Mhe. Mwenyekiti, Idadi ya miradi mipya iliyoidhinishwa na Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar (*ZIPA*) imeongezeka kwa asilimia 83 kutoka miradi 6 (Januari – Juni) mwaka 2016 hadi miradi 11 sambamba ongezeko la thamani kwa asilimia 633.2 kutoka Dola za Kimarekani 29.3 milioni kufikia Dola za Kimarekani 186.4 milioni (Januari-Juni) mwaka 2017. Idadi ya ajira mpya imeongezeka kwa asilimia 7.8 kutoka ajira 1,155 kufikia ajira 1,245 kwa kipindi kama hicho mwaka 2016.

Miradi ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*PPP*)

Mhe. Mwenyekiti, serikali imeridhia kufanyika kwa upembuzi yakinifu kwa miradi ipatayo 11 ambayo iko katika hatua mbalimbali. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi na uendeshaji na masoko, viwanda vya usarifu wa mazao ya kilimo na uvuvi, viwanja vya michezo. Aidha kwa miradi ya upatikanaji wa umeme wa kutumia jua na mradi wa ujenzi wa Bandari ya Mafuta na Gesi huko Mangapwani, upembuzi yakinifu wa awali umekamilika. Hatua inayofuata ni utayarishaji wa upembuzi yakinifu kamili ambao serikali umeshautolea maelekezo.

Uchambuzi wa Matokeo ya Hali ya Rasilimali Watu Katika Utumishi wa Umma Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ina takriban watumishi wa umma (serikali, taasisi na mashirika) wapatao 34,085, wanaume ni 17,228 sawa na asilimia 51 na wanawake ni 16,857 sawa na asilimia 49. Aidha, kwa mujibu wa Matokeo ya utafiti wa nguvu kazi *(Integrated Labour Force Survey)* wa mwaka 2014 yameonesha kuwa kiwango cha vijana wenye umri 15-35 wasiokuwa na ajira kimefikia asilimia 21.3. Kati ya vijana hao kundi la vijana wenye umri wa miaka 20 – 24 ndio kundi kubwa zaidi ambao wamefikia asilimia 28.5. Vijana wa mjini wanaongoza kwa kuwa na asilimia 33.6 ukilinganisha na wale wa vijijini ambao ni asilimia 11.9.

Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2016/17

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2016/17 ni sehemu ya mwanzo ya utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar (MKUZA III), uliopangwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano na kukamilika mwaka 2020 sambamba na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020.

Mhe. Mwenyekiti, MKUZA III unakusudia kuendeleza mageuzi ya kiuchumi na kijamii na kupunguza umaskini kwa kuimarisha uchumi endelevu, kujenga miundombinu imara, kukuza uzalishaji kwenye sekta za kilimo, utalii na viwanda vidogo vidogo; kuimarisha rasilimali watu; ubora wa huduma za jamii ikiwemo elimu, afya, mazingira endelevu na misingi ya utawala bora.

Mkakati huo umegawika katika maeneo makuu matano ambayo kama ifuatavyo:

(i) Kuwezesha ukuaji wa uchumi jumuishi na endelevu;

(ii) Kukuza uwezo wa rasilimali watu;

(iii) Kutoa huduma bora kwa wote;

(iv) Kuweka mazingira endelevu na uhimili wa mabadiliko ya tabianchi; na

(v) Kushikamana na misingi ya utawala bora.

Mhe. Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2016/17 ulitegemewa kugharimu jumla ya shilingi 395.9 bilioni. Serikali ilipanga kutoa shilingi 71.1 bilioni sawa na asilimia 18 ya bajeti yote ya kazi za maendeleo ambapo kati ya fedha hizo, shilingi 58.0 bilioni ni kwa miradi ya vipaumbele, yenye mikataba au dhima *(commitment)* na shilingi 13.1 bilioni kwa miradi mengine. Shilingi 324.8 bilioni sawa na asilimia 82 zilipangwa kutoka kwa washirika wa maendeleo ambapo shilingi 89.2 bilioni ni ruzuku na shilingi 235.6 bilioni ni mkopo. Hadi kufikia mwisho wa mwezi wa Juni 2017, jumla ya shilingi 164.2 bilioni zilitolewa sawa na asilimia 41.5 ya Bajeti ya maendeleo ambapo shilingi 50.8 bilioni zilitolewa na Serikali sawa na asilimia 71.4 ya bajeti ya serikali na shilingi 113.5 bilioni sawa na asilimia 34.9 zilitolewa na Washirika wa Maendeleo.

Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Julai - Disemba 2017

Mhe. Mwenyekiti, Ili kuhakikisha utekelezaji wa MKUZA III unafanyika kwa ufanisi miradi mbalimbali imekuwa ikitekelezwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Katika kipindi cha miezi sita, miradi ifuatayo imetekelezwa katika maeneo ya Vipaumbele kwa mwaka 2017/2018:

i. Kuimarisha miundombinu ya maeneo ya uingiaji nchini (yanayojumuisha bandari na viwanja vya ndege), barabara pamoja na nishati.

ii. Mkakati wa utafutaji Rasilimali Fedha

iii. Kuimarisha viwanda vidogo vidogo kwa kuongeza thamani bidhaa na ubora wa vifungashio.

v. Kuimarisha kilimo kwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji maji, uvuvi na mifugo.

vi. Kuimarisha ubora wa huduma za kijamii zikiwemo elimu, afya, michezo na upatikanaji wa maji safi na salama.

vii. Utawala bora na uimarishaji wa taasisi, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na uwekaji mji katika hali ya usalama.

MAPITIO YA BAJETI YA MWAKA 2016/17

Mapato

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/17, serikali ilipanga kukusanya jumla ya shilingi 841.5 bilioni. Kati ya Fedha hizo, mapato ya ndani ni shilingi 482.4 bilioni na mapato kutoka nje ni shilingi 324.8 bilioni. Kiasi kilichobakia cha shilingi 34.3 bilioni kinatokana na mikopo ya ndani ya shilingi 33.0 bilioni na Msamaha wa Madeni (MDRI) shilingi 1.3 bilioni.

Matumizi

Mhe. Mwenyekiti, serikali ilikadiria kutumia jumla ya shilingi 841.5 bilioni katika mwaka wa fedha 2016/17 ikihusisha matumizi ya kazi za kawaida ya shilingi 445.6 bilioni sawa na asilimia 53.0 ya bajeti kuu, na matumizi ya kazi za maendeleo ya shilingi 395.9 bilioni sawa na asilimia 47.0.

Utekelezaji Halisi kwa Mwaka 2016/17

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2016/17, jumla ya shilingi 644.37 bilioni zimekusanywa, sawa na asilimia 76.5 ya lengo la kukusanya shilingi 841.5 bilioni. Makusanyo haya yanajumuisha makusanyo ya ndani ya shilingi 521.88 bilioni na mapato kutoka nje ya shilingi 108.73 bilioni. Aidha jumla ya shilingi 8.11 bilioni zilikopwa kutoka soko la ndani. Vilevile, misaada ya kibajeti ya shilingi 5.66 bilioni ilipokelewa kwa mwaka wa fedha 2016/17.

Mhe. Mwenyekiti, Mapato ya ndani yameonekana kufanya vizuri zaidi katika kipindi cha mapitio kwa kufikia shilinigi 521.88 bilioni, sawa na asilimia 108 ya lengo la

mwaka. Kati ya makusanyo hayo, mapato ya kodi ni shilingi 478.12 bilioni ambayo ni sawa na asilimia 106.9 ya makisio ya jumla ya shilinig 447.2 bilioni. Aidha, mapato yasiyo ya kodi yamefika shilingi 43.76 bilioni ambayo ni sawa na asilimia 124.3 ya makisio ya jumla ya shilingi 35.20 bilioni. Kwa upande wa ukuaji, mapato yasiyo ya kodi nayo yamekuwa kwa asilimia 55.45 kutoka shilingi 28.15 bilioni za mwaka 2015/16.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa mapato ya nje jumla ya shilingi 108.73 bilioni zilikusanywa, mapato shilingi 46.87 bilioni ni za ruzuku na shilingi 61.86 bilioni zinatokana na mikopo. Hili ni ongezeko la asilimia 9.1 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2015/16, ambapo jumla ya shilingi 104.9 bilioni zilikusanywa. Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepokea Misaada ya kibajeti yenye thamani ya Jumla ya shilingi 5.66 bilioni kwa mwaka wa fedha 2016/17.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya mapato yaliyokusanywa kwa Mfuko wa Miundombinu kwa mwaka wa fedha 2016/17 yalifikia jumla ya shilingi 27.13 bilioni sawa na asilimia 103 lengo la jumla ya shilingi 26.32 bilioni kwa mwaka huo. Kati ya mapato hayo ya shilingi 27.13 bilioni, *ZRB* ilikusanya shilingi 17.32 bilioni sawa na asilimia 103 ya lengo la shilingi 16.80 bilioni. *TRA* kwa upande wake ilikusanya shilingi 9.81 bilioni sawa na asilimia 100 ya lengo la kukusanya kiwango hicho.

Matumizi:

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mapitio, matumizi halisi yalifikia jumla ya shilingi 635.5 bilioni. Kati ya matumizi hayo jumla ya shilingi 526.7 bilioni zilitumika kutoka kwenye mapato ya ndani na shilingi 108.7 bilioni zilitumika kutoka kwa washirika wa maendeleo. Aidha, kati ya matumizi hayo, matumizi ya kazi za kawaida yalifikia shilingi 475.5 bilioni sawa na asilimia 107 ya lengo la shilingi 445.6 bilioni.

Utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha Miezi Sita 2017/18 (Julai - Disemba):

Mapato ya Serikali

Mhe. Mwenyekiti, Katika mwaka wa fedha 2017/18 serikali ilikadiria kukusanya jumla ya shilingi 10873 bilioni ikijumuisha, mapato kutokana na vyanzo vya ndani jumla ya shilingi 675.8 bilioni sawa na asilimia 25.7 ya pato la taifa. Kati ya fedha hizo, jumla ya shilingi 627.0 bilioni zitatokana na makusanyo ya vyanzo vya kodi na shilingi 48.8 bilioni ni kutokana na vyanzo visivyo vya kodi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi cha miezi sita (Julai hadi Disemba 2017) mapato ya ndani yalifikia shilingi 320.3 bilioni sawa na asilimia 96 ya makadirio ya kipindi hicho. Katika kipindi kama hicho kwa mwaka uliopita (2016/2017), mapato ya ndani yalifikia jumla ya shilingi 249.5 bilioni. Utendaji huu unamaanisha ukuaji wa mapato kwa shilingi 70.8 bilioni sawa na asilimia 28.4. Kati ya makusanyo hayo ya shilingi 320.3 bilioni, mapato kutokana na kodi yalifikia shilingi 298.6 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 96 ya makadirio wakati mapato yasiyokuwa ya kodi yalifikia shilingi 21.7 bilioni sawa na asilimia 103 ya makadirio.

Ukusanyaji wa Mapato Kitaasisi

Mhe. Mwenyekiti, Jumla ya mapato halisi katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2017/18 yalifikia shilingi 460.0 bilioni ikiwa ni asilimia 85 ya makadirio ya kipindi hicho. Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) ilikusanya jumla ya shilingi 126.3 bilioni sawa na asilimia 100 ya makadirio, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 24.7 ikilinganishwa na ukusanyaji wa kipindi kama hicho kwa mwaka 2016/2017. Aidha, Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) ilikusanya jumla ya shilingi 161.9 bilioni sawa na asilimia 92.7 ya makadirio ya nusu mwaka. Mapato hayo yameongezeka kwa mwaka 2017/2018 kwa asilimia 28.9 ikilinganishwa na makusanyo ya

kipindi kama hicho mwaka 2016/2017 ya jumla ya shilingi 125.6 bilioni.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi hicho cha miezi sita, mapato ya mawizara yalifikia shilingi 21.7 bilioni sawa na asilimia 103 ya lengo. Makusanyo ya Kodi ya Mapato kutoka kwa wafanyakazi wa SMT waliopo Zanzibar yalifikia shilingi 10.5 bilioni sawa na asilimia 100 ya makadirio ya kipindi hicho. Aidha, Serikali ilikopa shilingi 20.0 bilioni kwa hati fungani kutoka soko la ndani.

Mapato ya Mfuko wa Miundombinu

Mhe. Mwenyekiti, Jumla ya mapato yaliyopokelewa kutokana na Mfuko wa Miundombinu kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2017 yamefikia shilingi 16.19 bilioni sawa na asilimia 90.5 ya bajeti ya shilingi 17.88 bilioni kwa kipindi cha miezi sita. Mchanganuo wa Mapato hayo ya shilingi 16.19 bilioni inajumuisha makusanyo kutoka *ZRB* ya shilingi 11.53 bilioni sawa na asilimia 90.2 ya makadirio ya bajeti ya nusu mwaka ya shilingi 12.77 bilioni pamoja na *TRA*, shilingi 4.66 bilioni sawa na asilimia 91.1 ya makadirio ya bajeti ya nusu mwaka ya shilingi 5.11 bilioni.

Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

Mhe.Mwenyekiti, Katika kipindi cha nusu mwaka wa Fedha2017/2018 (Julai – Disemba 2017), Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepokea ruzuku na mikopo kwa ajili ya Miradi na Programu za Maendeleo iliofikia shilingi 117.2 bilioni sawa na asilimia 30 ya makadirio ya mwaka 2017/18. Kati ya fedha hizo ruzuku ni shilingi 21.5 bilioni na mikopo ni shilingi 95.7 bilioni. Aidha, misaada ya kibajeti yenye thamani ya jumla ya shilingi 0.796 bilioni na misamaha ya madeni yenye thamani ya shilingi 1.7 bilioni imepokelewa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu mapato ya nje, kuongezeka kwa mapato kunatokana zaidi na kukwamuka kwa mradi wa jengo Jipya la Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume kutoka Benki ya *Exim* ya China na pale walipotoa malipo ya awali ya *USD* 35.2 milioni.

MATUMIZI

Matumizi ya Serikali

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha miezi sita (Julai – Disemba, 2017) jumla ya shilingi 595.6 bilioni zilikadiriwa kutumika. Kati ya matumizi hayo yaliyokadiriwa, shilingi 351.5 bilioni ni kwa kazi za kawaida na shilingi 244.1 bilioni ni kwa kazi za

maendeleo. Hadi kufikia Disemba 2017 matumizi halisi yalifikia shilingi 463.8 bilioni sawa na asilimia 77.9 ya makadirio ya kipindi hicho. Kati ya matumizi hayo shilingi 298.3 bilioni zilitumika kwa kazi za kawaida na shilingi 165.5 bilioni zilitumika kwa kazi za maendeleo.

Matumizi ya Kazi za Kawaida

Mhe. Mwenyekiti, Matumizi ya kazi za kawaida kwa kipindi cha miezi sita (Julai – Disemba 2017) yalifikia jumla ya shilingi 298.3 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 32.7 ikilinganishwa na matumizi ya kipindi kama hicho mwaka 2016/2017 ambapo jumla ya shilingi 224.7 bilioni zilitumika. Kati ya matumizi hayo, matumizi ya mishahara yalifikia shilingi 138.8 bilioni sawa na asilimia 100 ya makadirio ya kipindi hicho. Matumizi hayo ni sawa na ongezeko la asilimia 39.6 ikilinganishwa na kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 ambapo jumla ya shilingi 99 bilioni zilitumika. Ongezeko hilo limechangiwa zaidi na kulipwa kwa mishahara mipya ambayo ilianza kutumika robo ya mwisho kwa mwaka 2016/17.

Mhe. Mwenyekiti, matumizi mengineyo ya kuendesha serikali *(Other Charges)* yamefikia shilingi 54.2 bilioni sawa na asilimia 70 ya makadirio ya kipindi hicho, matumizi hayo ni sawa na ongezeko la asilimia 16.5 ikilinganishwa na matumizi ya mwaka wa fedha 2016/2017 ambapo jumla ya shilingi 46.5 bilioni zilitumika.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa upande wa ruzuku kwa taasisi mbalimbali za serikali, jumla ya shilingi 48.1 bilioni zilitolewa sawa na asilimia 90 ya makadirio ya kipindi hicho. Kiwango hicho ni sawa na ongezeko la asilimia 17.2 ikilinganishwa na kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2016/2017 ambapo jumla ya shilingi 28.4 bilioni zilitumika.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi hicho, matumizi ya huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali yalifikia shilingi 57.1 bilioni sawa na asilimia 70 ya makadirio na sawa na ongezeko la asilimia 13.5 ukilinganisha na matumizi hayo katika mwaka wa fedha 2016/17 ambapo jumla ya shiligni 50.3 bilioni zilitumika. Matumizi haya ni kwa ajili ya kulipia viinua mgongo, pencheni, ulipaji wa mishahara kwa viongozi wakuu wa serikali, malipo ya wazabuni pamoja na matumizi mengineyo ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, Ongezeko la matumizi kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali limetokana na ongezeko la Mishahara kwa Watumishi wa Umma ambalo linapelekea kuongezeka kwa viwango vya malipo ya Kiinua Mgongo kwa Wastaafu na ongezeko la pencheni lililoongezwa kutoka shilingi 40,000 kwa kima cha chini hadi shilingi 90,000 kwa mwezi sawa na asilimia 125. *(Makofi)*

Matumizi ya kazi za Maendeleo

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mapitio, jumla ya matumizi kwa kazi za maendeleo yalifikia shilingi 165.5 bilioni sawa na asilimia 67.8 ya lengo la shilingi 244.1 bilioni kwa miezi sita. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani zilikuwa shilingi 48.3 bilioni, sawa na asilimia 89.8 ya makadirio ya shilingi 53.8 bilioni na fedha za nje zilikuwa ni shilingi 117.2 bilioni sawa na asilimia 61.6 ya makadirio ya shilingi 190.3 bilioni ya miezi sita.

Matumizi ya Mfuko wa Miundombinu:

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya shilingi 34.9 bilioni zilikadiriwa kutumika kwa miradi iliyoorodheshwa chini ya Mfuko wa Miundombinu, hivyo kwa kipindi cha miezi sita (Julai hadi Disemba 2017), jumla ya shilingi 12.36 bilioni zimetumika sawa na asilimia 35 ya bajeti ya mwaka.

Deni la Taifa

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Disemba 2017, Deni laTaifa limeongezeka kwa asilimia 15.3 na kuwa shilingi 436.22 bilioni kutoka shilingi 369.9 bilioni za Disemba 2016. Katika deni hili la shilingi 436.22 bilioni, deni la ndani lilikuwa ni shilingi 158.77 bilioni na deni la nje limefikia shilingi 276.45 bilioni. Hatahivyo, deni hili la taifa bado linahimilika kwani ni sawa na asilimia 16.5 tu ya pato la taifa.

Matarajio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka 2017/18

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa mwenendo wa makusanyo katika kipindi cha miezi sita ilioishia Disemba 2017, matarajio ya makusanyo hadi kufikia mwezi Juni mwaka 2018 ni shilingi 960.3 bilioni (yanayohusisha na gawio la shilingi 13.5 bilioni kutoka Benki Kuu ya Tanzania) sawa na asilimia 88.5 ya bajeti ya mwaka ya shilingi 1.085 trilioni. Hali hii ni sawa na ukuaji wa asilimia 27 ikilinganishwa na ukusanyaji wa mapato kwa mwaka uliopita 2016/17.

Mhe. Mwenyekiti, kati ya fedha hizo, mapato ya kodi yanatarajiwa kufikia shilingi 600.9 bilioni, sawa na asilimia 95.8 ya bajeti ya shilingi 627.01 bilioni, ambapo ni sawa na ukuaji wa asilimia 25.5 ikilinganishwa na ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha uliopita 2016/17. Mamlaka ya Mapato Tanzania - Zanzibar (*TRA*), inatarajiwa kukusanya shilingi 256.05 bilioni sawa na asilimia 98.9 sawa na ukuaji wa asilimia 26 ikilinganishwa na ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha uliopita 2016/17.

Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) inatarajiwa kukusanya shilingi 323.8 bilioni sawa na asilimia 93.2; ambapo ni sawa na ukuaji wa asilimia 27 ikilinganishwa na ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha uliopita 2016/17. Kodi ya Mapato kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano inatarajiwa kufikia shilingi 21.0 bilioni sawa na asilimia 100 ya lengo.

Mhe. Mwenyekiti, mapato yasiyokuwa ya kodi yanatarajiwa kufikia shilingi 61.56 bilioni sawa na asilimia 126, ambapo ni sawa na ukuaji wa asilimia 40.6 ikilinganishwa na ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha uliopita 2016/17. Mapato ya mawizara yanategemewa kufikia shilingi 45.36 bilioni sawa na asilimia 108.4 ya makadirio ya mwaka ya shilingi 41.84 bilioni. Gawio la Mashirika ya Serikali linatarajiwa kufikia shilingi 3.2 bilioni sawa na asilimia 106.7 ya makadirio ya mwaka ya shilingi 3 bilioni. Gawio la Benki Kuu ya Tanzania, linatarajiwa kufikia shilingi 13 bilioni sawa na asilimia 325 ya makadirio ya mwaka ya shilingi 4 bilioni.

Mfuko wa Miundombinu

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/18, matarajio ya mapato ya mfuko wa Miundombinu ni shilingi 32.4 bilioni sawa na asilimia 93 ya makadirio ya Bajeti, ambapo *TRA* inatarajiwa kukusanya shilingi 9.3 bilioni na *ZRB* inatarajiwa kukusanya shilingi 23 bilioni.

Mapato kutoka Nje:

Mhe. Mwenyekiti, mapato kutoka nje yanatarajiwa kufikia shilingi 224.8 bilioni ambayo yanajumuisha mambo yafuatayo:

i. Ruzuku na Mikopo shilingi 219.5 bilioni.

ii. Misaada ya Kibajeti (GBS) ni shilingi 2.79 bilioni.

iii. Msamaha wa Madeni (MDRI) ni shilingi 2.5 bilioni.

Matarajio ya Matumizi, Julai – Juni 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti, hadi Juni 2018, matumizi yanatarajiwa kufikia shilingi 945.6 bilioni sawa na asilimia 87.1 ya bajeti ya mwaka ya shilingi 1.085 trilioni. Matumizi ya Kazi za Kawaida yanatarajiwa kufikia shilingi 587.1 bilioni na Matumizi ya kazi za Maendeleo yanatarajiwa kufikia shilingi 358.5 bilioni.

Mwelekeo wa Bajeti, 2018/19

Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo, 2018/19

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2020 ikiwa katika kipindi chake cha mwisho cha miaka mitatu. Serikali imeidhinisha Mkakati mpya wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUZA III) unaotekelezwa na Wizara na Taasisi zote.

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi hakutarajiwi kuwa na mabadiliko makubwa kwa kwa maeneo yatakayopewa kipaumbele. Hivyo, katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2018/19, maeneo yatakayopewa kipaumbele ni kama ifuatavyo:

1. Kuimarisha miundombinu ya maeneo ya uingiaji nchini ikiwemo barabara na nishati;

2. Kuimarisha zaidi Utalii nchini;

3. Kuimarisha viwanda vidogo vidogo kwa kuongeza thamani bidhaa na ubora wa vifungashio;

4. Kuimarisha kilimo kwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji maji, uvuvi na mifugo;

5. Kuimarisha ubora wa huduma za kijamii zikiwemo elimu, afya, michezo na upatikanaji wa maji safi na salama;

6. Kuendeleza tafiti mbalimbali za kiuchumi na kijamii kwa maendeleo ya nchi. *(Research for Development);*

7. Kukuza uwezo wa raslimali watu katika fani adimu zikiwemo afya, viwanda, mafuta na gesi asilia ili kukuza ufanisi katika maeneo hayo;

8. Kuimarisha ajira kwa vijana kwa kuwawezesha pamoja na kuwapatia taaluma na ujuzi stahiki;

9. Utawala bora, uimarishaji wa taasisi na uwekaji mji katika hali ya usalama.

Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, mwelekeo wa hali ya uchumi kwa mwaka 2018 unategemea kwenda sambamba na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2020, kutekeleza MKUZA III na Maendeleo katika kupunguza Umaskini pamoja na kutekeleza Ilani ya uchaguzi ya Tawala Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015.

Mhe. Mwenyekiti, Pato Halisi la Taifa kwa mwaka 2018 linatarajiwa kukua kwa kasi ya wastani wa asilimia 7.1. Matarajio ya ukuaji wa uchumi yatatokana na mambo yafuatayo:

1. Kuendelea na juhudi za kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula kwa ununuzi wa matrekta mapya 20 ambayo yataongeza kasi ya uzalishaji wa ndani;
2. Kuongezeka kwa usafirishaji wa zao la karafuu kutokana na msimu mkubwa kwa zao hilo katika mwaka 2017;
3. Kuongezeka kwa uhamasishaji wa uwekezaji wa ndani na nje kwa kutekelezwa miradi mipya;
4. Kuongezeka kwa kiwango cha idadi ya watalii wanaoingia nchini kutokana na kupatikana wa masoko mapya ya utalii.

Shabaha na Malengo ya Uchumi kwa 2018.

Mhe. Mwenyekiti, shabaha na malengo ya uchumi kwa mwaka 2018 ni kama ifuatavyo:-

i. Ukuaji wa pato halisi la taifa kukua na kufikia asilimia 7.1 mwaka 2018 na
hii italinganishwa na na ukuaji wa asilimia 7.0 mwaka 2017;

ii. Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei katika tarakimu moja;

iii. Mapato ya kodi kuwa asilimia 24.2 ya pato la taifa mwaka 2018/19 kutoka asilimia 23.8 kwa mwaka 2017/18;

iv. Matumizi ya serikali yanatarajiwa kuwa asilimia 38 ya pato la taifa mwaka 2018/19 ikilinganishwa na asilimia 36 mwaka 2016/17;

v. Kupunguza nakisi ya bajeti kutoka asilimia 5.3 mwaka 2017/18 hadi asilimia 3.9 mwaka 2018/19. Nakisi hii inajumuisha na misaada kutoka nje; na

vi. Kuendelea kuwepo kwa hali ya amani na utulivu.

Mwelekeo wa Mapato

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018/19, serikali inatarajia kukusanya jumla ya shilingi 1.21 trilioni zikiwemo shilingi 787.2 bilioni zitokanazo na vyanzo vya ndani, shilingi 387.7 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo na shilingi 35 bilioni mikopo ya ndani.

Mapato ya Ndani

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kuwa tunatarajia kukusanya kutoka vyanzo vya ndani Jumla ya shilingi 787.2 bilioni, katika mwaka 2018/19 hii itakuwa ni sawa na ukuaji wa asilimia 19.6 ikilinganishwa na matarajio ya mapato ya mwaka wa fedha 2017/18. Kati ya fedha hizo, shilingi 722.2 bilioni ni mapato yatokanayo na kodi, na shilingi 65 bilioni ni mapato yasiyokuwa ya kodi (yanayojumuisha makusanyo ya Mapato ya Mawizara ya shilingi 56 bilioni, Gawio la Mashirika ya Serikali yanayotarajiwa kuwa ni shilingi 5 bilioni na Gawio kutoka Benki kuu ya Tanzania la shilingi 4 bilioni).

Hatahivyo, kati ya jumla ya mapato yote hayo yanayotarajiwa kutokana na vyanzo vya ndani, mapato yaliyokasimiwa matumizi maalum na hivyo kutoweza kugawanywa kwenye matumizi mengine ni kama ifuatavyo:

a) Fedha kwa ajili ya Mfuko wa Miundombinu ambazo ni shilingi 39.4 bilioni;
b) Asilimia 5 ya makusanyo inayobaki *ZRB* inayotarajiwa kuwa ni shilingi 20.0 bilioni
c) Makusanyo kwa ajili ya Mfuko wa Barabara yanatarajiwa kuwa ni shilingi 16.5 bilioni;
d) Ada ya Bandari kwa mchango wa madeski inatarajiwa kuwa ni shilingi 1.0 bilioni;
e) Mfuko wa Maendeleo ya Elimu (SDL) yanatarajiwa kuwa ni shilingi 13.5 bilioni; na
f) Ada ya Usalama wa Anga *(Safety Fee)* inayotarajiwa kuwa ni shilingi 6.4 bilioni.

Mapato ya Nje

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018/19, serikali inatarajia kupokea jumla ya shilingi 387.8 bilioni kutoka kwa washirika wa maendeleo, zinazojumuisha ruzuku ya shilingi 90.8 bilioni na mikopo ya shilingi 296.9 bilioni.

Mwelekeo wa Matumizi

Mhe. Mwenyekiti, serikali inakadiria kutumia jumla ya shilingi 1.21 trilioni katika mwaka wa fedha 2018/19 ikiwemo matumizi ya kazi za kawaida ya shilingi 671.8 bilioni na matumizi ya kazi za maendeleo ya shilingi 508.1 bilioni.

Mhe. Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba katika bajeti tunayoendelea nayo, tuliripoti kupungua kwa utegemezi wa bajeti kwa ruzuku kutoka nje kutoka asilimia 11.1 mwaka 2016/17 hadi asilimia 7.3 mwaka 2017/18. Kutokana na mchango wa ruzuku ya shilingi 90.8 bilioni katika bajeti ya shilingi 1.21 trilioni ya mwaka 2018/19, utegemezi wa bajeti unatarajiwa kushuka zaidi na kufikia asilimia 7.1.

Vigezo vya Ugawaji wa Rasilimali Fedha

Mhe. Mwenyekiti, ugawaji wa fedha za maendeleo kwa mwaka 2018/19 umezingatia mambo makuu yafuatayo:

i. Maeneo ya vipaumbele vya taifa kwa mwaka 2018/19;

ii. Maagizo maalum ya serikali kwa mujibu wa vipaumbele vya taifa ikiwemo.

   a. Elimu bure hadi Sekondari.

   b. Ununuzi wa Dawa za lazima *(essential drugs).*

   c. Ujenzi wa Mahkama kuu na Wizara ya Fedha.

   d. Utekelezaji wa Matokeo kwa Ustawi (R4P)

iii. Marekebisho ya kawaida ya mishahara pamoja na kuzingatia ajira mpya.

iv. Programu na miradi ya kimkakati *(Flagship Projects)* iliyotajwa katika *MKUZA III;*

v. Programu na miradi yote ambayo serikali ina dhima *(Commitment)* kutoka kwa Washirika wa Maendeleo;

vi. Programu na miradi yote iliyokuwa haijakamilika utekelezaji wa shughuli zake kwa bajeti ya mwaka 2017/18.

vii. Ilani ya uchaguzi ya Chama Tawala (CCM) ya 2015. (*Makofi*)

Mfuko wa Miundombinu

Mhe. Mwenyekiti, Mfuko wa Miundombinu umekadiriwa kukusanya na kutumia jumla ya shilingi 39.4 bilioni ambazo zitatumika kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Bodi ya Mapato *(ZRB)* inakadiriwa kukusanya shilingi 27.6 bilioni ambapo Mamlaka ya Mapato *(TRA)* nayo inakadiriwa kukusanya shilingi 11.8 bilioni.

Sura ya Bajeti

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuzingatia hali ya bajeti kwa mwaka 2018/2019, mapato ya ndani pamoja na ruzuku na mikopo yanatarajiwa kufikia shilingi 1.21 trilioni ikihusisha:

- Mapato ya ndani ya shilingi 787.2 bilioni, na
- Ruzuku na Mikopo kutoka nje ya shilingi 387.8 bilioni.

Kwa upande wa matumizi, jumla ya shilingi 1.21 trilioni zinatarajiwa kutumika kama ifuatavyo:

- Matumizi kwa kazi za kawaida shilingi 701.8 bilioni, Ikijumuisha :
  - i) Mishahara (Wizara) shilingi 301.7 bilioni
  - ii) Mishahara (Taasisi za Ruzuku) shilingi 39.8 bilioni
  - iii) Matumizi Mengineyo (Wizara) shilingi 163.7 bilioni
  - iv) Matumizi Mengineyo (Ruzuku) shilingi 66.6 bilioni
  - v) Mfuko Mkuu wa Serikali (CFS) shilingi 130.0 bilioni
- Matumizi kwa Kazi za Maendeleo shilingi 508.2 bilioni.

i) Mchango wa Serikali shilingi 120.4 bilioni.

ii) Mikopo na Ruzuku shilingi 387.8 bilioni.

Kwa kuzingatia mapato na matumizi hayo, kumejitokeza nakisi ya bajeti ya shilingi 35 bilioni ambayo imepangwa kuzibwa kwa mikopo ya ndani, na kufanya jumla ya mapato kufikia shilingi 1.21 trilioni.

Mhe. Mwenyekiti, taarifa hii imeambatanishwa na viambatanisho sita na naomba kuviwasilisha mbele yake Mhe. Mwenyekiti.

i Kiambatisho nam. 1: Mapendekezo ya Mchanganuo wa Mapato ya Ndani kwa mwaka 2018/2019;

ii Kiambatisho nam. 2: Mapendekezo ya Mfumo wa Bajeti kwa mwaka 2018/2019;

iii Kiambatisho nam. 3: Mchanganuo wa Miradi inayofadhiliwa kwa Mikopo na Ruzuku kutoka nje kwa mwaka 2018/2019;

iv Kiambatisho nam, 4: Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kimafungu

v Kiambatisho nam. 5: Utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha Miezi Sita (2017/2018) na;

vi Kiambatisho nam. 6: Utekelezji wa Bajeti kwa Mwaka 2016/2017. (*Makofi*)

Hitimisho

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, kwa heshima kubwa, sasa naliomba Baraza lako liidhinishe mapendekezo na hatimae likubaliane na Mwelekeo wa Makadirio ya Matumizi ya shilingi 1.21 Trilioni ikiwemo shilingi 701.8 bilioni kwa matumizi ya kawaida na shilingi 508.2 bilioni kwa kugharamia Mpango wa Maendeleo; na kuiruhusu Wizara ya Fedha na Mipango kutayarisha na kuwasilisha Mwelekeo wa Uchumi, Mpango wa Maendeleo pamoja na Mwelekeo wa Bajeti kwa mwaka 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Tume ya Mipango izikishirikiana na wizara mbalimbali za serikali bado zinaendelea na jitihada za kutafuta mapato pamoja na kuendelea na mijadala ya ufadhili wa programu na miradi mbali mbali ya maendeleo na washirika wa maendeleo, pana uwezekano wa kubadilika kwa mapato na matumizi hayo. Hivyo, naliomba Baraza lako liidhinishe mkabala huu pamoja na mabadiliko ya bajeti yatakayotokana na sababu zilizo ainishwa hapo juu.

Mhe. Mwenyekiti, Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, taarifa imewasilishwa na imeungwa mkono. Sasa, naomba nisome tangazo kwanza hapa.

TANGAZO

Mhe. Mwenyekiti: Mweyekiti wa Baraza la Wawakilishi *Sports Club* Mhe. Hamza Hassan Juma anawatangazia Waheshimiwa Wajumbe wote pamoja na wapenzi na wachezaji wa Baraza la Wawakilishi *Sports Club*, kuhudhuria katika mazoezi yatakayofanyika siku ya Alhamis ya tarehe 8/3/2018 kwa utaratibu ufuatao. Wanaume *Footbal*l uwanja wa Wazee Maisara, Wanawake *Netball* viwanja vya Baraza la Wawakilishi Chukwani, mazoezi yatafanyika siku ya Alhamis, Ijumaa na Jumamosi kuaniza saa 12 hadi saa 2:00 asubuhi. Shime tuhudhurie kwa wingi ikiwa ni njia mojawapo ya kuimarisha afya zetu pamoja na kujiandaa kwa ajili ya michezo ya Pasaka.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba nimpishe Mhe. Mwenyekiti kuendelea na kikao hichi Mhe. Mwanaasha Khamis Juma karibu sana.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti, Mwanaasha Khamis Juma alikalia kiti)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba nimuite Mhe. Mwenyekiti, wa kamati ya bajeti.

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti) Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa sasa naomba kuwasilisha hotuba ya maoni ya Kamati ya Bajeti juu ya Mapendekezo ya Mwelekeo wa Uchumi na Mpango wa Maendeleo na Mkabala wa bajeti, kwa mwaka 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mweyezi Mungu kwa kutujaalia siku nyegine ya uhai katika kutekeleza majukumu yetu ya kitaifa katika kuwatumikia wananchi naowawakilisha.

Mhe. Mwenyekiti, pili nikushukuru wewe kwa niaba ya Kamati ya Bajeti kunipa fursa hii adhimu kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu, maoni ya Kamati ya Bajeti juu ya Rasimu ya Mapendekezo ya Mwelekeo wa Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti 2018/19.

Mhe. Mwenyekiti, naomba ikumbukwe kuwa, uwasilishaji huu wa maoni ya Kamati juu ya waraka nilioutaja ni kwa mujibu wa matakwa ya Kanuni ya 92(1) ya kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2016 inayolipa uwezo Baraza kujadili na kushauri juu ya Mapendekezo ya Mwelekeo wa Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka unaofuata uliowasilishwa na waziri mwenye dhamana ya mambo ya mipango.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na upya wa utaratibu huu kwa Baraza lako tukufu, niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa umahiri wao mkubwa waliouonesha katika kuupitia, kuhoji na kushauri mambo mbalimbali yaliyogusiwa katika waraka huu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo.

1. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Mwenyekiti
2. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Mjumbe
4. Mhe. Abdalla Ali Kombo - Mjumbe
5. Mhe. Shehe Hamad Mattar - Mjumbe
6. Mhe. Simai Mohamed Said - Mjumbe
7. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Mjumbe
8. Ndg. Abdalla Ali Shauri - Katibu
9. Ndg. Kassim Tafana Kassim - Katibu
10. Ndg. Asha Said Mohamed - Katibu

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi kwa kushirikiana na wahusika mbali mbali, imeupitia na kuufanyia tahmini ya kina waraka wa Mapendekezo ya Mwelekeo wa Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Mkabala wa Bajeti kwa mwaka 2018/2019 katika maeneo mbalimbali ya waraka huo. Naomba kwa niaba ya kamati kutoa tathmini na maoni juu waraka huo.

Tathmini ya Kamati katika Mapitio ya Hali ya Uchumi 2016

Uchumi wa Dunia

Mhe. Mwenyekiti, wastani wa ukuaji wa uchumi katika Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi Duniani kwa kipindi cha Januari-Juni, inaonesha kukuwa kwa wastani wa asilimia 0.3 ukilinganishwa na wastani wa ukuwaji wa 0.1 katika kipindi cha Januari-Juni 2016. Wastani huu umekwenda sambamba na ukuwaji wa uchumi wa kanda tofauti ambapo nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara imekuwa na ukuaji wa uchumi mdogo kwa wastani wa asilimia 0.4 kulinganisha na nchi zinazoendelea zenye uchumi

uliokuwa kwa wastani wa asilimia 0.5, na nchi zinazoinukia kiuchumi ambazo uchumi wake ulikuwa kwa asilimia 0.7.

Mhe. Mwenyekiti, ukuaji huo wa kiuchumi unaonesha kuwa nchi za kusini mwa jangwa la sahara ikiwemo Zanzibar na Tanzania kwa ujumla hazijaweza kwenda sambamba na kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia ikilinganishwa na nchi nyengine ulimwenguni, hali inayoonekana pia kupitia kasi ya mfumko wa bei ambapo nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara zimeendelea kuwa na kasi ya mfumko mkubwa wa bei wa asilimia 11 ikilinganishwa na nchi zilizoibukia ambazo zina mfumko wa bei wa 4.2 na nchi zilizoendelea zina mfumko wa asilimia 1.7.

Ukuaji wa Uchumi wa Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, ukuaji wa uchumi wa Zanzibar kwa kiasi kikubwa unachangiwa na sekta ya huduma, kilimo na viwanda, ambapo kwa kipindi cha Januari- Juni 2017 umeonekana kukua kwa kasi ya asilimia 6.3 hadi kufikia asilimia 8.2.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wa sekta hizi kwa ukuaji wa uchumi wa Zanzibar, hautokani na tija inayopatikana moja kwa moja na wananchi, bali ni kutokana na ukweli kwamba wananchi waliowengi wamejiajiri katika sekta hizo hususan kilimo ambacho zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wanategemea sekta kilimo kwa njia moja au nyengine katika kujipatia kipato na kuimarisha maisha yao. Kimsingi, sekta ya kilimo bado haijawekewa mazingira ya kibiashara na kumfanya mwananchi wa kawaida kuendelea kuishi maisha duni kwa kutegemea kilimo cha kienyeji. Kamati inaishauri serikali kuwawezesha wakulima wadogo kwa kuwapatia mafunzo ya kilimo cha biashara na kuwawekea mazingira yatakayowawezesha kuhama kutoka katika kilimo cha kizamani ambacho kimsingi kina tija ndogo kwa kuwapatia mikopo nafuu sambamba na kuendeleza na miundombinu ya umwagiliaji maji.

Mhe. Spika, kwa upande wa Sekta ya Viwanda, licha ya kuwa na mchango mkubwa kiuchumi kama inavyoonekana katika waraka, bado Zanzibar haijaitumia sekta hiyo ipasavyo kutokana kuendelea na kuwa na viwanda vichache ambavyo haviwezi kuleta ushindani wa bidhaa zinazozalishwa nchini. Kutokana na mchango wa viwanda katika ukuaji wa mazingira ya visiwa vya Zanzibar. Kamati inaishauri serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kuangalia namna ya kuwashajihisha wawekezaji wakubwa na wadogo kufanya uwekezaji katika viwanda vya uzalishaji ambayo vinaendana na mazingira ya Zanzibar, ikiwa ni pamoja na viwanda vya kusarifu mazao ya baharini na viwanda vya kuunganisha bidhaa *(Assembling Plant)*

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuimarika kwa shilingi ya kitanzania dhidi ya dola ya kimarekani kwa punguzo dogo la thamani la asilimia 0.26 kwa wastani wa shilingi 2231.2 kutoka wastani wa shilingi 2225.54. Kamati inaishauri serikali kuongeza kasi ya uzalishaji wa bidhaa za ndani ili kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi ambao unapunguza thamani ya shilingi dhidi ya dola.

Aidha, kamati bado inaona upo umuhimu kwa serikali kuhimiza matumizi ya shilingi ya kitanzania katika mfumo wa kulipia huduma mbali mbali zinazotolewa na taasisi binafsi na zile za serikali kwa lengo la kupunguza mahitaji ya dola ya Kimarekani kunakoshusha thamani shilingi ya kitanzania.

Mhe. Mwenyekiti, waraka pia unaonesha kuongezeka kwa watalii katika kipindi cha Januari- Juni 2017 hadi kufikia watalii 170,581 kutoka watalii 143,851 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2016, ikiwa watalii wengi ni kutoka Italia,Uengereza na Ujerumani. Kamati imebaini bado kuna fursa pana zaidi ya kuongeza idadi hiyo ya watalii wanaokuja nchini kwa kuitangaza zaidi Zanzibar kimataifa katika nchi za Asia na nchi nyengine zinazoinukia kichumi ambazo kimsingi zina idadi kubwa ya watu ambayo inaweza kutumika kama fursa kwa upande wa Zanzibar.

Uwekezaji Binafsi Kupitia *ZIPA*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi cha Janunari-Juni 2016 miradi ya uwekeaji kupitia *ZIPA* imeongezeka kutoka miradi 6 katika hadi kufikia miradi 11 katika kipindi Januari-Juni 2017 na kupelekea ongezeko la ajira kwa asilimia 7.8 kutoka ajira 1,155 kufikia 1,245 katika mwaka 2017.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa serikali inatekeleza bajeti inayotumia programu *(PBB)* ambayo kimsingi inazingatia zaidi matokeo. Kamati, inashauri taarifa za ajira zitakazowasilishwa mbele ya Baraza lako tukufu kwa ajili ya bajeti ya mwkaa 2018/2019 ziwasilishwe kwa kuonesha mgawanyo na maelezo ya kina kwa ajira hizo, ili Wajumbe wa Baraza na wananchi kwa ujumla wapate fursa ya kufanya tathmini ya ufanisi wa utekelezaji wa mipango na bajeti ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na serikali kuridhia kufanyika kwa upembuzi yakinifu kwa miradi 11 chini ya mwavuli wa *PPP*, hadi sasa hakuna mradi hata mmoja ambao umetekelezwa kupitia mfumo huo, ikiwa ni miaka mitatu sasa tangu Baraza lako tukufu kupitisha Sheria ya *PPP* Nam. 8 ya 2015. Kutokana na umuhimu wa mfumo wa *PPP* kwa ukuaji wa Uchumi. Kamati, inashauri serikali ichukue jitahada za makusudi kuhakikisha miradi hiyo inaanza kutekelezwa kwa mfumo wa *PPP* kwa kuwa nchi nyingi ulimwenguni zimefanikiwa kiuchumi kwa mashirikianao na sekta binafsi. Aidha, kutokana na changamoto za utekelezaji wa Sheria ya *PPP*, kamati inashauri serikali kuifanyia mapitio Sheria pamoja na Sera ya *PPP* ambazo kimsngi utekelezaji wake ni mgumu.

Utekelezaji Halisi wa Bajeti kwa Mwaka 2016/2017

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, serikali ilipanga kukusanya jumla ya shilingi 841.5 bilioni kati ya fedha hizo, mapato ya ndani ni shilingi 482.4 bilioni na mapato kutoka nje ya nchini ni shilingi 324.8 bilioni. Aidha, kiwango cha shilingi 34.3 bilioni kinajumuisha mikopo ya ndani ya shilingi 33.0 bilioni msamaha wa madeni wa shilingi 1.3 bilioni.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji halisi, jumla ya shilingi 644.37 bilioni zimekusanywa zinazojumuisha mapato ya ndani ya shilingi 521.88 bilioni na mapato kutoka nje ya shilingi 108.73 bilioni na jumla ya shilingi 8.11 bilioni zilikopwa kutoka soko la ndani na misaada ya kibajeti ya shilingi 5.66 bilioni zilipokelewa.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imearifiwa mapato ya ndani yaliyokusanywa ni kiasi cha shilingi 521.88 bilioni na matumizi halisi yaliyofanyika kutoka kwenye mapato ya ndani ni jumla ya shilingi 526.7. Kamati inaishauri serikali kufanya matumizi yake kwa kuzingatia kuwa mapato inayokusanya yanakuwa endelevu kwani vianzio vya

ndani ndio vya uhakika katika kupanga matumizi na hivyo si busara kutumia fedha yote inayokusanywa.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuimarika kwa makusanyo ya mapato ya ndani katika miaka tofauti ya utekelezaji wa bajeti ya serikali, kimsingi bado utekelezaji wa jumla wa Bajeti kwa mwaka 2016/2017 umekua na nakisi kubwa kwa kutekelezeka kwa asilimia 76.5 pekee na kuacha nakisi ya asilimia 23.5 ya utekezaji. Nakisi hii kwa kiasi kikubwa inaonekana kuchangiwa na kutopatikana kwa fedha kutoka nje ambapo kwa mwaka 2016/2017, ni bilioni 108.726 pekee zilizopatikana kati ya bilioni 324.800 ambazo ni sawa na asilimia 33. Kamati inashauri katika bajeti ya 2018/2019 kufikiria zaidi namna ya kupunguza utegemezi wa bajeti ambao unasababisha utekelezaji usioridhisha kwa bajeti kuu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imeridhishwa na makusanyo yasiyo na kodi kwa mwaka 2016/2017, kwa kufikia shilingi bilioni 43.76 ambayo ni sawa na asilimia 124.3 ya makisio ya jumla ya shilingi 35.20 bilion. Kamati, inashauri serikali kuwa wabunifu zaidi katika kukusanya mapato yasiyo ya kodi kwa lengo la kuwapa nafuu wananchi wa kawaida. Kwakuwa makusanyo hayo tozo zake hazimgusi mwananchi wa kawaida moja kwa moja, tofauti na ilivyo kwa mapato yatokanayo na kodi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2016/2017 Mamlaka za ukusanyaji wa mapato yaani *ZRB* na *TRA* zimeonekana kufikia malengo waliyojiwekea, ambapo *ZRB*, imefika malengo kwa asilimia 103 na *TRA* kwa asilimia 100. Kamati inashauri serikali kuongeza umakini wa kuweka malengo hayo kwa lengo la kuwa na shabaha zinazoendena na uwezo halisi wa taasisi hizo.

Utekelezaji wa Bajeti kwa Kipindi cha Miezi Sita 2017/18 (Julai – Disemba)

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilipokea taarifa ya mapato ya serikali kwa kipindi cha Julai – Disemba 2017/18 yanayojumuisha mapato ya taasisi, mapato ya mfuko wa miundombinu na mapato kutoka kwa washirika wa maendeleo, ambapo kiujumla kamati imebaini kuwa ukusanyaji wa mapato ni mzuri. Kwakuwa, hali ya ukusanyaji mapato ni wa kuridhisha, kamati inasisitiza mapato yote yanayokusanywa kutoka katika mifuko maalum itumike katika matumizi yaliyokusudiwa ikiwemo ada ya Bandari inayopaswa kutumika katika kuchangia ununuzi wa madawati na Mfuko wa Maendeleo ya Elimu (*SDL*) utumike katika shughuli za Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kama ilivyotajwa katika Sheria ya Kuanzisha Mamlaka hiyo Sheria Nam. 8 ya mwaka 2006.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na matumizi ya kazi za kawaida, kamati imearifiwa kuwa katika kipindi cha Julai – Disemba 2017/18 jumla ya shilingi 595.6 bilioni zilikadiriwa kutumika. Kati ya matumizi hayo yaliyokadiriwa, shilingi 351.5 bilioni ni kwa kazi za kawaida na shilingi 244.1 bilioni kwa kazi za maendeleo. Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Disemba 2017 matumizi halisi yalifikia shilingi 463.8 bilioni ambapo kati ya hizo shilingi 298.3 bilioni zilitumika kwa kazi za kawaida na shilingi 165 bilioni zilitumika kwa kazi za maendeleo. Kwa kipindi hicho, kamati imebaini kuwa matumizi yaliyofanyika hayakupindukia makadirio na hivyo matumizi ya namna hii ndio yanayotakiwa kwa kuwa haitopelekea serikali kupangua bajeti zake nyengine.

Deni la Taifa

Mhe. Mwenyekiti, kamati imearifiwa kuwa hadi kufikia Disemba 2017, deni la taifa limeongezeka kwa asilimia 15.3 ukuaji huo unaojumuisha deni la ndani na la nje. Kwakuwa, serikali imekuwa ikitoa taarifa zinazohusiana na ukuaji wa deni la taifa, kamati inaishauri serikali kutoa ufafanuzi juu ya mpango waliojiwekea wa namna ya kulipa deni hilo *(Debt Payment Plan)* ili wananchi wafahamu kwa kiasi gani deni hilo limepangwa kupunguzwa na pia kupatiwa taarifa kila baada ya muda kwa namna gani serikali imeweza kulipa deni hilo.

Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo, 2018/19

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2018/19, utekelezaji wa mpango wa maendeleo, katika viapumbele vyake ni pamoja na kuimarisha miundombinu, utalii, viwanda vidogo vidogo, kilimo na kuimarisha huduma za kijamii. Katika vipaumbele ambavyo serikali itavifanyia kazi kwa bajeti ya mwaka 2018/19, kamati inaishauri serikali juu ya kuweka vipaumbele vichache na ambavyo vitakuwa na uhalisia.

Mhe. Mwenyekiti, ili vipaumbele hivyo viweze kupimwa utekelezaji wake, kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kuweka wazi vipaumbele vyake ikiwa ni pamoja na kutaja idadi na sehemu ya miundombinu ya uingiaji nchini itayofanyika, kuainisha aina gani ya utalii utakaoimarishwa na mikakati iliyopangwa katika kuimarisha sekta hii, namna gani sekta ya kilimo itakavyoimarishwa, aina za tafiti za kiuchumi na kijamii zitakazofanywa kwa maendeleo ya nchi.

Aidha, vipaumbele vya kitaifa kwa mwaka 2018/19 kwa namna vilivyoainishwa katika waraka, ni vigumu kuweza kupima utekelezaji wake. Kwakuwa serikali inatekeleza bajeti inayotumia Programu (*PBB*) ambayo kimsingi inazingatia zaidi matokeo, kamati inasisitiza kuwepo kwa takwimu zitakazoonesha namna ya vipaumbele hivyo vitakavyoweza kupimwa utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, moja kati ya maeneo yanayopendekezwa kuwa vipaumbele vya taifa kwa mwaka 2018/2019 ni kumarisha miundo mbinu ya maeneo ya uingiaji nchini, barabara, na nishati. Kimsingi miundombinu hii ni muhimu sana hasa kwa kuzingatia kwamba kutoendelezwa kwake kunaleta taswira mbaya ya nchi yetu na kwa wageni wanaotembelea, lakini pia hurejesha nyuma wawekezaji hususani katika Sekta ya Utalii ambayo ina mchango mkubwa kwa taifa. Kwakuwa, maeneo ya uingiaji nchini ni mengi, kamati inashauri kipaumbele hichi kifafanuliwe zaidi ili kujua ni barabara gani hasa zimelengwa kuimarishwa kwa mujibu wa mpango wa maendeleo wa mwaka 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kipaumbele cha kuimarisha utalii. Kamati, inaishauri serikali itanue wigo wa sekta hiyo kwa kuhamasisha na kuimarisha utalii wa kimatibabu na elimu *(medical and educational tourism)* sambamba na kuwawekea mazingira mazuri wawekezaji yatakayowarahishia kuwekeza katika maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, huduma na miundombinu katika maeneo ya uingiaji nchini bado haijafikia kiwango cha kuridhisha, hivyo kamati inasisitiza serikali kulitekeleza vyema eneo hili ikiwa ni pamoja na kuimarisha huduma na mazingira ya maeneo ya viwanja vya ndege na bandarini na kuzitengeneza barabara zinazoelekea maeneo

hayo, sambamba na kuweka taa za barabarani. Aidha, serikali izingatie kuweka mazingatio maalum ya kuimarisha miundombinu ya msingi katika maeneo yenye uwekezaji mkubwa hususani kwa hoteli za kitalii.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine la kipaumbele kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ni kuimarisha huduma za kijamii ikiwemo elimu, afya, michezo na upatikanaji wa maji safi na salama. Huduma za jamii ni eneo muhimu sana ambalo linamgusa mwananchi moja kwa moja. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto kadhaa katika utekelezaji wake, ambapo licha ya juhudi kubwa za serikali katika kutoa huduma hizo, bado mahitaji yanaendelea kuwa makubwa siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inasisitiza uimarishaji wa huduma za elimu uzingatie sana ubora wa elimu unaopatikana kwa kuweka mikakati madhubuti itakayohakikisha kuna uwiano wa kasi ya kuongezeka kwa wanafunzi na walimu wanaoajiriwa, upatikananji wa vifaa vya kusomeshea sambamba na kuongeza idadi ya madarasa ambayo yatapunguza mrundikano wa wanafunzi. Aidha, serikali iweke mazingatio maalum kwa skuli za mashamba kwakuwa matokeo katika skuli hizo yamekuwa hayaridhishi. Hii inadhihirika wazi kupitia matokeo ya kidato cha pili na cha nne katika miaka ya hivi karibuni ambapo Zanzibar imekua ikishika mkia.

Mhe. Mwenyekiti, juhudi za kuongeza ubora wa huduma pia zinapaswa kufanywa katika sekta ya afya ambayo pia ina changamoto ya uchache wa madaktari kwa baadhi ya hospitali, ambapo madaktari wachache waliopo hulazimika kuhudumia wagonjwa wengi kinyume na viwango vinavyotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto ya utoaji wa huduma za jamii kiujumla zinaathiriwa kwa kiasi kikubwa na mahitaji makubwa ya huduma hizo yasiyokwenda sambamba na uwezo wa serikali katika kutoa huduma, kutokana na kasi ya ongezeko la idadi ya watu. Kamati, inaelewa changamoto ya utamaduni wa Zanzibar kuhusu idadi ya watu ambao kwa kiasi kikubwa unatokana na suali la kiimani. Hatahivyo, kamati inaishauri serikali itowe elimu kwa wananchi kuhusu athari za ongezeko kubwa la idadi ya watu na namna linavyoathiri uwezo wa serikali katika utoaji wa huduma za msingi kwa jamii.

Mhe. Waziri wa Afya lazima atekeleze na aoneshe haja ya nyota ya kijani kwa jamii.

Mhe. Mwenyekiti, kipaumbele chengine kinachotarajiwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ni kuimarisha ajira kwa vijana kwa kuwawezesha, pamoja na kuwapatia taaluma na ujuzi stahiki.

Kamati, inahofu hata kama vijana hao watapatiwa taaluma na ujuzi stahiki bila ya kupatiwa mitaji, bado itakuwa hatuja wasaidia kuondokana na changamoto ya ajira kwakuwa wapo vijana wengi ambao wamejikusanya lakini wanashindwa kupata mitaji ya kujiendeleza. Hivyo, kamati inashauri serikali izingatie kuandaa utaratibu utakaowawezesha vijana hao kupatiwa mitaji, mara baada ya kupata taaluma na ujuzi stahiki.

MKUZA III na Dira ya Maendeleo ya 2020

Mhe. Mwenyekiti, moja kati ya nyenzo muhimu zinazozingatiwa katika kuandaa na kutekeleza Bajeti ya Serikali ni Mkakati mpya wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUZA III). Hatahivyo, Baraza hili likiwa ni chombo muhimu chenye jukumu la kusimamia bajeti ya serikali, halijapatiwa mafunzo ya kutosha kuhusu mkakati huo, hali hii inawakosesha fursa Waheshimiwa Wajumbe kutoa mapendekezo yanayokwenda sambamba na malengo ya mkakati huo, ambao ni muhimu sana katika kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya 2020.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inatoa wito kwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikia na Afisi ya Baraza la Wawakilishi kuandaa utaratibu utakaowawezesha Wajumbe wa Baraza lako kupata mafunzo kuhusu Mkakati huo, sambamba na mipango mengine muhimu ya maendeleo ya kitaifa na kimataifa, ambayo inahusiana na utekelezaji wa bajeti ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, ni takriban miaka mtatu tu iliyobakia kabla hatujafikia kipindi cha mwisho cha utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2020. Hatahivyo, pamoja na mafanikio yaliyopatikana kwa baadhi ya malengo, bado kuna changamoto kadhaa za utekelezaji wa malengo ya Dira hiyo, ambapo kwa muda mchache uliobakia huenda baadhi ya malengo hayo kutofikiwa ikiwemo suala zima la upatikanaji wa maji safi na salama kwa asilimia 100 pamoja na ubora wa kiwango cha elimu hususani katika ngazi za msingi *(Primary Education).* Kamati inaishauri serikali kufanya mapitio ya utekelezaji wa Dira ya 2020 ambayo kimsingi tuko nyuma katika utekelezaji wake, ili kuona kwa kiasi gani changamoto za utekelezaji wa malengo hayo zinaweza kutatatuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, kutofikia shabaha za malengo hayo pia kutapelekea kutofikia shabaha za malengo mengine ya dunia ikiwemo malengo ya maendeleo endelevu *(Sustainable Development Goals - SDGs)* ambayo kimsingi kuyafikia kwake kuna tegemea sana mafanikio ya utekelezaji wa malengo ya mipango ya maendeleo ya ndani.

Mhe. Mwenyekiti, njia nzuri ya kupima mafanikio ni kulinganisha tulichokipanga na kile tunachopaswa kukifikia kwa mujibu wa malengo ya kitaifa na kimataifa, kwa kuwa serikali inatekeleza bajeti inayotumia Programu (*PBB*) ambayo kimsingi inazingatia zaidi matokeo. Ili tuweze kupata sura halisi ya mafaniko na changamto za utekelezaji wa bajeti na mipango yetu. Kamati, inaishauri serikali, taarifa za utekelezaji wa bajeti na mipango ya maendeleo zinazo wasilishwa Barazani zifafanuliwe kwa upana zaidi, kwa kuwekwa takwimu na shabaha zake, ikiwemo pato la mwananchi mmoja mmoja, ukuaji wa ajira na mgawanyo wake, ongezeko la idadi ya watu na athari zake, uwiano wa madaktari na wagonjwa na uwiano wa walimu na wanafunzi.

Matarajio ya Ukuaji wa Uchumi kwa Mwaka 2018/19

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pato la taifa linatarajiwa kukua kwa kasi ya wastani wa asilmia 7.1. ikilinganishwa na wastani wa asilimia 7.0 kwa mwaka 2017. Pamoja wa ukuaji huo, ambao pengine tungeweza kusema ni ishara nzuri ya hali ya uchumi wetu. Hatahivyo, kasi ya ongezeko hilo ni dogo ambayo ni tofauti ya asilimia 0.1 tu ukilinganisha na mwaka 2017. Hii ina maana kwamba bado tuna kazi kubwa ya kuhakikisha tunafikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya 2020 ya

kuwa na ukuaji wa uchumi wa endelevu wa asilimia 9 hadi 10, licha ya kuwa tuna muda mchache wa kufikia malengo ya dira hiyo.

Hitimisho

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na jitihada nzuri zinazochukuliwa na serikali katika kuhakikisha mapato yanaongezeka, iwapo serikali haitoweka mikakati madhubuti katika kuhakikisha nidhamu katika matumizi ya fedha hizo, athari chanya ya mapato hayo haitoonekana. Hivyo, kamati inaendelea kusisitiza serikali isimamie vyema nidhamu ya matumizi ya fedha kwa kuhakikisha taratibu na sheria za matumizi ya fedha zinazingatiwa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha miradi ya maendelo inatekelezwa kwa muda na kiwango kinachostahiki.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyegine tena na kushukuru kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu mapendekezo ya mwelekeo wa Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2018/2019. Pia niwashukuru Wajumbe wote wa Baraza kwa kunisikiliza kwa umakini wakati nikiwasilisha maoni ya kamati juu ya waraka huu, naomba wauchangie na waishauri vyema serikali, kwakuwa huu ni msingi wa bajeti ya serikali naamini maoni na ushauri wa Wajumbe utakua na nafasi kubwa katika kurekebisha na kuzingatia mawazo yao ili kuifanya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2018/2019 kuwa na ubora unaostahiki.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijamaliza hotuba yangu nimshukuru sana Waziri wa Fedha na Uchumi wa Maendeleo kwa kazi kubwa ambayo tumeshirikiana na yeye pamoja na Afisi wake na Katibu Mkuu ndugu yangu Khamis Mussa kwa kazi kubwa ambayo tuliifanya jana. Hivyo nataka kusema pamoja na kazi hii tuliyoifanya na muelekeo huu mzuri wa serikali tuendelee sana kuunga mkono jitihada za serikali zinazofanywa mara kwa mara.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo na pongezi zangu ndogo sasa naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Mohammed Said Mohammed, Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae lakini pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea, sasa mchangiaji wetu wa mwanzo naomba nimwite Mhe. Suleiman Sarahan Said, Mwakilishi wa Chakechake, atafuatiwa na Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) na Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil ajiandeae.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kuchangia machache kuhusu Hotuba ya Mkabala wa Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Mwelekeo wa Bajeti wa mwaka 2018/2019 kwa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la kwanza kama nilivyokuwa namnukuu Mwenyekiti wa Kamati nampa pongezi sana watendaji pamoja na waziri wanaohusika na kitabu hiki. Kwakweli, kina sifa yake kimechanganua mambo yote na kuelekea mpango wa kwamba tunajua tujipange kuelekea wapi, kweli hiki ni kitabu kizuri kichojipanga kwa bajeti pamoja na yote. Pamoja na mafanikio yaliopatikana basi pia nimpongeze

sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika uongozi wake anaotuongoza na kutufikia malengo haya, pia nimpongeze Makamu wa Pili wa Rais katika juhudi zake za kuiongoza serikali katika wizara zake zote.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nifurahie lakini pia nione kwamba tunafanye katika ukurasa wa 5 kifungu cha 13 hapa uchambuzi wa matokeo ya hali ya rasilmali watu katika utumishi wa umma. Mhe. Mwenyekiti, ni jambo kidogo lililonishutuwa lakini sijui tunaliwekaji lakini mtungaji wetu huyu ametufafanulia vizuri sana, kwamba tuna vijana kuanzia miaka 20 mpaka 24 ambao wana asilimia 28.5 ni vijana wengi sana tayari inakaribia robo tatu ya watu wote ni watu muhimu sana tunawafanyia nini na tunawatumiaje hawa ili kuweze kukuza pato letu la nchi.

Lakini kilichonishangaza ni badala ya kuona badala kwamba vijana walioko shamba ni wengi kumbe vijana walioko mjini ni wengi wana asilimia 33.6 vijana walioko mjini, asilimia 11 ndio walioko mashamba au vijijini hili kidogo nimeliona kwamba nilikuwa nafikiria vijana wengi wako mashamba kumbe vijana wako mjini, nimeshukuru kwa hiki kiatabu lakini tunawafanyaje katika hali kama hii na hawa ndio nguvu kazi.

Kwahivyo, hiki nilikuwa nasema kuna haja kwa serikali kuangalia kwa kina ni sababu zipi zile zile zilotufanya vijana hawa waje mjini na kuacha kule shamba kwenye mambo mengi ya uzalishaji, sasa inabidi serikali tukae tutizame nini ambacho kitatusaidia hapa.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala la hili la pato la mwananchi au pato la serikali tunalozungumzia tunaliona pato limekua la nchi, pato limekuwa la mtu binafsi lakini tatizo linalojionesha katika maisha yetu pato la ubinafsi linakuwa halionekani, kuna vingi ambavyo havimfii mtu kule chini ambavyo vinaweza vikazungumsha pesa, vikazungumsha maisha.

Mhe. Mwenyekiti, ni lazima adhma na vitu tulivyo vikusudia mabenki lazima tuyatumilie yalivyo na tuweze kuyawekea mikakati, riba zipunguwe na wananchi wakopeshwe pesa zizunguke sasa wafanya biashara wa benki wanafanya kwasababu wanafedha anakuwekea mikakati yake ya kubana au ya kuongeza hii tunayoita riba, mfanyakazi haji juu nini wale wanaokwenda kukopa hawaji juu kima ni kikubwa na sisi tunaona hata kama serikali inataka kukopa inakwenda kukopa kwenye mikopo nafuu, ili tuweze kuendelea kwa mikopo hii ya kibenki inayokwenda hii inatumaliza mtu anazunguka matokeo yake hata mkopo unamshinda kurudisha.

Halafu, tunaona kwamba pato limekuwa lakini mtu wa chini haji juu lakini Mhe. Mwenyekiti ni lazima kwa sasa hivi lazima tuachane na mambo mengi tuliyokuwa nayo lakini viwanda lazima tuvijenge kwa hali mali kupunguza uagiziaji wa mizigo mengi inayotoka nje ambapo pesa zetu zinapotea sana.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona kwenye kitabu nimefurahi lakini nikasema niseme nimeona katika sekta ambazo zimewekezwa kwamba zinaweza mna sekta ya afya humu nakumbuka hapa tumepitisha hapa Sera ya Hospitali ya Mnazimmoja ya kuweza kuifanya iwe Hospitali ya Rufaa tungeita watu wa Comoro kuja kutibiwa hapa, tungeita watu wagonjwa wote hawajafikia lengo wote wanakwenda India wanazichukua pesa zote wanazipeleka India hawafanyi biashara wale wanakwenda

kutibu mwili wao, pesa zote wanaziacha kule ndio ukakuta India wameweka *open* pale ukitaka kwenda wewe ni raha tu nende mbio mbio ukatibiwe pesa zote zinaondoka.

Kwahivyo, lazima na sekta yetu sisi ya afya ikuwe tupunguze pesa zetu kupeleka nje kama tumeona tumefika hapo tumeshindwa katika hospitali, basi tuimarisheni wale waganga wa kienyeji ili na watu wengine waje huku, maana kama sekta ya afya haifanyi kazi vizuri, basi hii sekta ya waganga wa kienyeji nayo inatakiwa na sisi tunasifikiana Tanzania kwa kuroga tumo kwa kuweka mambo sawa. Kutokana na hali hiyo, naomba sana Mhe. Mwenyekiti, kama sekta ya afya yetu haikuwi bado tunahamisha watu wetu kupeleka pesa nje, basi na sisi tuweke kitege uchumi chetu. Kwahivyo, hicho ndicho nilikuwa nataka kusema Mhe. Mwenyekiti tukiangalie.

Mhe. Mwenyekiti, humu nimealingalia kitu sijapata takwimu kamili sekta ya utalii kuimarika hapa katika hoja za Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo akija katika mazungumzo yake mengi hata kitabu cha mwaka jana kile cha bajeti anasema tuna watalii karibu laki tatu na ngapi na tunamsimamo wa kusema mpaka tukifika 2020 tutakuwa na watalii laki tano, mwendo huu ndio tunaokwenda. Lakini cha kuchangaza kwenye kitabu hiki kuna watalii laki moja na sabini sasa hapa naona kama tuko laki na sabini hiyo *target* itafika? Sasa kama tuko laki tatu na imekuwaje haya mahesabu yameenda kidogo au sijafahamu, lakini nimeona kwamba humu muna watalii kama laki moja sabini na *something* halafu kwenye utalii tuna rekodi watu laki tatu, kwahivyo hapa labda tuangalie tu inakuwaje sasa tuangalie zaidi.

Mhe. Mwenyekiti naomba kuishauri serikali, madeni iliyonayo serikali sina wasiwasi nayo yameshasema yanahimilika na yanakwenda, ya nje kwasababu wametukopesha wenyewe tuyaache kama yalivyo, watu walioko ndani walipwe ili pesa izunguke utamkuta kila mtu ambaye ana biashara anakwambia anaidai serikali yule ukitaka kwenda kumkopa anakwambia sipati ngoja mpaka nilipwe, sasa pesa haizunguki mle ndani.

Kutokana na hali hiyo, naiomba serikali ifanye jitihada zake zote, ili madeni ya ndani haraka hata juzi Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli niliwahi kumsikia tunatenga bilioni kadhaa kwa ajili ya kulipa madeni ya ndani nchi itafufuka, tukilipa madeni ya ndani nchi itafufuka, tukilipa madeni ya ndani kila mmoja anang'ara pesa itakuwa inatembea. Kwahivyo, serikali isibane sana pesa za ndani iachie, madeni ya nje tena watatizama muhali wazo wa kulipa itakuwaje. Kwa hiyo, naomba sana kuhusu habari hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, bado nasema tena serikali ingawa ina *target* iondokane na kukodi maofisi, iondokane na kukodi maofisi serikali inakwenda vizuri ina kusanya pesa vizuri inakwenda mtindo mzuri pesa yake haibariki haikai ikiingia imetoka, mambo inayokula serikali mengi naomba yapunguzwe yakiwepo maofisi yanakula pesa sana. Kwahivyo, naomba kwasababu ardhi ni mali ya serikali, basi tuchukuweni ardhi tujenge maofisi. Hivyo, nashauri zile pesa angalau zinapokusanywa ziweze kutulia tufanye mambo mengine ambayo yana muelekeo wa kuangalia sana.

Lakini kitu chengine ambacho nakizungumzia biashara, kwakweli biashara ni serikali ukitizama ndio inayofanya biashara, ingawa utasema serikali haitaki biashara lakini ndio inayotupa miongozo ya biashara serikali. Mhe. Mwenyekiti, naiomba serikali

ikafungua milango vizuri sana kwenye biashara na wananchi wanaotaka kuja kuwekeza kukawa na wepesi wa kuweza kupata vibali pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo, ili kuweza kuwekeza, lakini tukiwangaisha na mambo mengine, kwasababu yule mtu akisha kujenga kiwanda hapa Mhe. Mwenyekiti hakiondowi tena kile kiwanda kinakuwa cha kwetu hata kiwanda cha mtu kinakuwa kiwanda cha kwetu.

Sasa tatizo linakuwa ukiritimba mwengine unaokwenda kwa watendaji, kwasababu ana cheo fulani atazuwia zuwia mpaka umpe chochote hii iondoke iweze kuweka usawa wa serikali, ili tuweze kupata hivi vitu ambavyo vinafanyika haraka na wananchi wapate ajira ndio tuanavyoweza kwenda sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie suala la kilimo Zanzibar bado tunanua vitu nje sana hata sikumbii nje na Tanzania Bara bado tunanunua vitu nje yaani, bado ukulima bado haujafikia lengo la kuweza kutumia vitu vya ndani na pesa yetu isiondoke, pesa yetu ya serikali inaondoka mpaka ya vitu vidogo vidogo mpaka ya bizari pesa yetu inaondoka kwa bizari. Kwakweli, hivi sasa angalau nashukuru utasikia kuna hizi tunaita *spice* za Zanzibar, lakini hazijatosha kabisa tungepata ukulima na tusione ukulima huu wa vitu vidogo vidogo ni mwepesi ni mzito na ni mzuri unachukuwa pesa nyingi za serikali huu. Kwahivyo, ningeomba sana tukahakikisha kwenye upande wa kilimo tunaweza kwenda vizuri sana ili kuepukana na mambo haya ya utumiaji pesa.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tatizo kubwa tunaloimarika leo moja tu hapa mtu mmoja asipoleta mchele serikali nzima inayumba kwa chakula hamna, bado hatujafikia malengo ya kuweza kutumia, lazima nchi nyingi tu huko duniani zinasimama kwa kilimo, nchi nyingi duniani zinasimama kwa utalii, sisi kila kitu tunacho sisi ni mipango na matumizi bora ndio tatizo tu. Kwa kweli, kila kitu tunacho Mwenyezi Mungu ametupa bahari, tuna mameli ya kutosha kuweza kuwekeza na kufanya kila kitu, tumepata uwanja wa ndege huo hapo japo haujamalizika, Mhe. Mwenyekiti humu nimeona pesa zimo na mambo yatakamilika, na namuomba Mwenyezi Mungu amsaidie, ili umalizike ule uwanja ushakuwa na maneno mengi mimi hata kuusemea sitaki Mwenyezi Mungu ajaalie umalizike tu kwa hali hiyo.

Kwahivyo, nina uhakika nchi iliyobarikiwa bahari, nchi ilibarikiwa ardhi maana yake ni ya kilimo, nchi iliyobarikiwa anga kuna kina aina ya sekta ya kupata pesa tuna madini yanakuja katika mazingira haya haya na humu wameandika. Mhe. Mwenyekiti, kwanza kitu ambacho nakiomba sana jambo lolote linaloibuliwa lifanyiwe kazi na limalizike tunataka maendeleo ya haraka.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi haiwezekani tena kitu kinakaa miaka kumi, miaka kumi na tano, ishirini kitu unakizinduwa wewe mpaka anakuja mfalme wa tatu ndio anakuja kukimalizia hapana, muda tunawaona wanaokwenda wenzetu wanakwenda katika kasi inayokwenda likisemwa limetekelezeka limemalizika. Kwahiyo, naomba sana Mhe. Mwenyekiti tukafanye hivyo tukisema tutende, ili tuweze kwenda na *speed* ambayo inafanana.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kwenye ukurasa wa 18 mpaka 19, hapa kuna masuala ya kuimarisha miundombinu ya maeneo ya uingiaji nchini barabara na nishati, kuimarisha zaidi utalii nchini, kuimarisha viwanda vidogo na kuongeza

thamani bidhaa na ubora wa vifungashio, kuimarisha kilimo na kujenga miundo mbinu ya umwagiliaji maji, uvuvi na mifugo, kuimarisha ubora wa huduma ya kijamii ikiwemo, elimu afya, michezo upatikanaji maji safi na salama, kuendeleza tafiti za kiuchumi za kijamii na kimaendeleo, kukuza uwezo wa rasilimali watu katika fani ya adhimu zikiwemo afya, viwanda, mafuta na gesi asilia, ili kukuza ufanisi katika maeneo hayo. Kuimarisha ajira kwa vijana kuwawezesha pamoja na kuwapatia taaluma za ujuzi wastahiki, utawala bora, uimarishaji wa taasisi na uwekaji katika hali ya usalama.

Mhe. Mwenyekiti, hapa pote Mhe. Waziri amemaliza kazi bado tatizo letu tunalo ameweka maji safi na salama, kwakweli Mhe. Mwenyekiti mpaka sasa hivi watu wanahangaika na maji tu asubuhi kwanza anatoa pesa za mfukoni akanunuwe maji unampunguza pato lake hii amelisema mwenyewe waziri humu kwamba yakipatikana maji safi na salama lakini umimarishaji wa kinywa hapa Mheshimiwa kila kitu kimemalika. Tukiweka utalii vizuri tutakwenda, tukiweka miundombinu ya uingiaji wa wageni wetu bandarini na kwenye ndege tutakwenda, kuimarisha kilimo tutakwenda sasa hapa ndio kuna elimu na afya.

Mhe. Mwenyekiti, hii michezo sijaifahamu vipi maana yake sijaona kama kwetu hapa Zanzibar kuna michezo ambayo inaweza ikaingiza pato la taifa, sijaiona ikiungwa kwa kasi mchezo ni huu katika miaka yetu yote tumekuja kuona juzi mchezo huu wa mpira vijana wa *Zanzibar Heroes* walioshiriki Mashindano ya *CECAFA* sote na tumecheza sote kwa kuwa ndio jambo la kwanza hili. Lakini, sijaona kwamba tuna wachezaji ambao tunawapeleka nchi za nje wala michezo gani ambayo tumeimarisha sijaoina michezo yenyewe sasa hivi tunaipiga marufuku ngoma zote tushazipiga marufuku sijui michezo gani tutapeleka. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naomba sana bado sekta ya michezo sijaiona kama ina faida na kuipatia pato, labda tunaiweka kama sehemu ya mazoezi mimi ninavyoona ni sehemu ya mazoezi, tumeimarika sana kwa mazoezi alfajiri huku tunakwenda mbio kweli, lakini mchezo kama mchezo sijawaona watu ambao tumewaimarisha kimichezo hatuna mchezaji hata mmoja sisi. Kwa mfano, utasikia kule duniani Marekani wanaye Michael Jordan mchezaji, huku kule wapi wanae yule Filbert Bayi mwanariadha wa Tanzania Bara na sisi Zanzibar tuna nani sijamuna mchezaji hata mmoja labda Halikuniki. Ndiye nimuonaye maana yake sioni kitu chengine hasa sijui tunakwenda vipi ukisema sekta ya michezo ina pesa ina kila kitu lakini kwetu hatujaifanyia kazi.

Hizo miundombinu ya *academic* ziko wzapi huko skuli michezo haiko tena sasa tunakwenda wapi tumesambaratisha michezo yote ...

Mhe. Mwenyekiti: Malizia dakika mbili Mhe. Mjumbe.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ninakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti. Tumesambaratisha michezo skuli wametoka vipaji sana wachezaji wakubwa wakubwa wote hawa walitoka skuli, leo michezo skuli hakuna wala hazina au hakuna kiwanja hata moja, skuli zenyewe ni nyumba za kukaa watu hatujaziimarisha skuli zikaa kama skuli zikawa na *full facilities* ya kila kitu, skuli sasa hivi wewe ukitaka kafungue ni nyumba ya mtu akodisha na kufungua skuli hatwendi katika mpangilio kama hiyo, lazima tutakwama kwasababu vitu vyote vinataka maandalizi Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, naomba sana na tuna jukumu kubwa sana Mhe. Mwenyekiti na hili ndio kubwa tatizo la ajira kwa vijana. Kwakweli, kasema humu Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kama tunajitahidi, lakini mpaka leo serikali inaajiri watu thelathini na nne alfu bado kidogo serikali angalau watu hamsini elfu ianze na hapo kwenda mbele.

Bado watu thelathini na nne elfu kidogo na ndio ukakuta kila sekta unayokwenda watu hawatimii unaambiwa tuna ukosefu wa watu, tujitahidi kukusanya kodi na miundombinu, ili tupate ajira zaidi tuongeze.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na naungza mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Suleiman Sarahan Said Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) atafuatiwa na Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil, Mhe. Rashid Makame Shamsi na yeye ajiandae.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kuweza kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kuchangia Hotuba ya Mkabala wa Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Mwelekeo wa Bajeti kwa mwaka 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze kwa dhati Mhe. Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Makamishna, Wakurugenzi, Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoitanya na kutuletea mwelekeo huu ambao ni kitabu kidogo sana lakini roho ya nchi yetu. Kwahivyo, nawapongeza kwa utaalamu wao mzuri ambao tumeuona mbele ya macho yetu. *(Makofi)*

Lakini pili Mhe. Mwenyekiti, niipongeza kamati yetu Kamati ya Bajeti kwa mashirikiano mazuri walioshirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango juu ya kuhakikisha kwamba tunakwenda vizuri katika utekelezaji wa mipango ya serikali na maendeleo kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ni mtaalamu wa uchumi yeye mwenyewe pamoja na wasaidizi wake aliokuwa nao na hiki kitabu. Mhe. Mwenyekiti, kinaonesha dhahiri kwamba ni cha kitaalamu hutokwenda mbali kutoka na mipango na utekelezaji wake kwamba uko vizuri na utaelekea kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu tutafanikiwa.

Lakini kubwa niseme tu kwamba yote bajeti tuloanzia 2016/2017 tukaenda 2017/2018 imo humu na utekelezaji wake tumeuona na kukua kwa pato la taifa vilevile tumeona, kwahivyo huko kote naunga mkono na juhudi tumeziona lazimu turidhike na tuwazunge mkono wenzetu kwenye juhudi ya kukusanya mapato katika nchi yetu, ili kuhakikisha utekelezaji unatekelezeka.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuangalia hili nitakuwa na kurasa zangu kama mbili, tatu kwa ufupi sana ukurasa wa kumi na nane mwelekeo wa bajeti 2018/2019 japo Mhe. Suleiman Sarahan pale kanitangulia lakini na mimi nitasema kwa ufupi ili kuongeza nguvu.

Mhe. Mwenyekiti, ili tuendelee tunahitaji mambo mengi lakini tunahitaji kwanza afya njema, elimu, maji safi na mengineyo. Kwahivyo, naipongeza sana serikali kwa kukiangalia kifungu hiki cha (e) kuimarisha ubora wa huduma za kijamii zikiwemo elimu, afya, michezo na upatikanaji wa maji safi na salama. Mhe. Mwenyekiti, kadri tunavyokwenda kilio cha Wazanzibari wote nasema ni maji.

Kwa kweli, naiunga mkono serikali kwa kuliona hili lakini kwa makusudi ningemuomba Mhe. Waziri pamoja na juhudi za vipengele vya michezo, elimu ni jambo la lazima, afya ni jambo la lazima lakini maji ni lazima na ni la mwanzo kuliko yote hayo tunayotegemea, bila ya maji hatuna uhai. Hivyo, naiomba serikali kuliweka katika vipaumbele vya mwaka 2018-2019 basi twende kwenye maji angalau jambo hili libakie historia katika nchi kwa upatikanaji wa maji katika maeneo yote.

Mhe. Mwenyekiti, jengine lilowekwa hapa katika kipaumbele ni kuimarisha miundombinu ya maeneo ya uingiaji nchini wa barabara na nishati. Barabara ni jambo la lazima na tunashukuru zinaendelea vizuri. Lakini, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia Wizara ya Ujenzi na Usafirishaji barabara zinajengwa kwa wingi na nzuri na za thamani, lakini zinaharibika upesi kutokana na kiwango cha barabara zetu. Ningeomba tunapokuwa tayari kuhakikisha tunapata wakandarasi wazuri, basi tuwe tayari kukubali viwango vya sasa.

Mhe. Mwenyekiti, zamani tulikuwa na gari haizidi tani 2 au tani 3, leo kuna tani 20 au zaidi, kwa hivyo barabara zetu zinakufa upesi. Jengine kingo za pembeni ikishajengwa barabara kama haina kingo ya kuzuia mmong'onyoko ikija mvua barabara zinakatika. Kwahivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kwa hili tunatumia fedha nyingi kwenye barabara basi tuzihifadhi kwa lile jambo dogo ambalo litazistiri barabara zetu za muda mrefu.

Mhe. Mwenyekiti, nitatoa mfano wa barabara ambazo ziko hai mpaka leo. Kuna barabara ya Bububu imejengwa zaidi ya miaka 40 lakini unazikuta barabara ziko safi, ukienda Uwanja wa Ndege halikadhalika mmong'onyoko wa pembeni unasaidia zikiwekwa kingo huwa barabara hazikatiki, na ndio maana ukienda sehemu nyengine barabara zilizokuwa hazikujengewa kingo utakuta kama mna misumeno mle pembeni ukiweka gari *puncher*. Kwahivyo, namuomba sana Mhe. Waziri hili tuliangalie.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile Zanzibar tumebahatika tumezungukwa na bahari, na bahari hii ni uchumi katika nchi yetu. Bado twende mbio sana kuhakikisha kwamba tunapata nyenzo za kuwapa vijana wetu wakapata ajira kwa ajili ya kilimo, kwanza kilimo na uvuvi, uvuvi ni rasilimali tosha. Kwakweli, mara nyingi husema hapa Mhe. Mwenyekiti Tanzania Bara wana ziwa Victoria, wanasafirisha minofu ya samaki tani kwa tani, kwa nini sisi bado kisiwa chetu hiki cha Unguja na Pemba tunashindwa kutafuta viwanda ambavyo vitatusaidia kuimarisha samaki wetu kuwasafirisha nje na kupata soko zuri, kwa sababu samaki wa maji ya chumvi, sio samaki wa maji ya ziwa tofauti ipo sana. Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri tufanye tafiti zetu, tutafute wawekezaji, ili tuhakikishe kwamba fedha zinaingia kutokana na uvuvi, tunakosa fedha nyingi sana katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia juzi juzi kuna meli sijui 16 zimekamatwa wanaambiwa kila meli itatoa bilioni moja kama sikosei, kama ni adhabu. Watu wamekuja mpaka hapa bahari kuu tunakosa fedha, watu wanaingia kimagendo

wanakwenda kuchukua samaki sisi tunawatizama macho hatuelewi vipi. Tutafute wawekezaji na wawekezaji hao waje watusaidie.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika kuhakikisha kwamba kuwekeza si vibaya serikali itapata fungu lake na wawekezaji vilevile wanapata fungu lao. Hili twende mbio sana, wamo watu duniani wako tayari kuja kuekeza katika sehemu hizo, tutoe ushauri, tutoe maelekezo ili waje tusijibane sisi wenyewe wakati wanaoweza wapo ili faida ipatikane kwa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utalii naungana sana na mwelekeo huu mzuri. Utalii ni pato la taifa, na utalii lazima twende mbio tuhakikishe kwamba tunautangaza kwa kila hali. Utalii si kuingia watalii tu lakini na makusanyo yake yadhibitiwe, kwasababu tunaweza kuambiwa tumeingiza watalii laki tano au laki nne, siku nyengine pato lake halieleweki. Kwahivyo, namuomba sana Mhe. Waziri na wizara inayohusika kwenye sekta kila inayomgusa mtu kwanza tuzingatie mapato ya nchi yawe mbele kuliko jengine, vyenginevyo hatufiki. Watalii wanakuja wengi, *figure* inakuwa nzuri lakini kutokana na hali ambayo haieleweki pato linakuwa haliingii vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kuimarisha ajira kwa vijana hii inataka taaluma kubwa sana. Mhe. Mwenyekiti, naungana sana na vipaumbele hivi, vijana wetu wamo wengi mitaani, lakini vijana wetu wanataka kuelimishwa, na vijana wetu wanataka nyenzo. Kwahivyo, ni vyema tukawakusanya vijana wetu tukawaweka vizuri na tukawapa nyenzo wakafanya kazi zao kwa faida yao na kwa faida ya taifa kwa jumla. Kutokana na hali hiyo, wakikusanywa wakifanya kazi vizuri na wakipata pesa za kuwaendesha wao na faida katika serikali itaingia. Hivyo, ni vyema hili tuliangalie kwa hali na mali.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu ukurasa wa 19, mwelekeo wa hali ya uchumi nitasema kwa ufupi sana.

Mhe. Mwenyekiti, tunasema kwamba pato halisi la taifa kwa mwaka 2018 linatarajiwa kukuwa kwa kiasi cha wastani asilimia 7.1. Mhe. Mwenyekiti, hii ni faraja na tunategemea iwe hivyo, kwa hiyo nimuombe tu Mhe. Waziri tuongeze kukusanya mapato na mapato haya yatusaidie.

Pia Nam.1 imesema katika ukurasa wa 19, kuendelea na juhudi za kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula kwa ununuzi wa matrekta mapya 20. Mhe. Mwenyekiti, matrekta ni changamoto nzuri na mpaka leo nimeshuhudia wakati mwengine unaangalia watu wanalalamika matrekta eneo fulani hayajafita. Kwakweli, silaumu najua uchache tuliokuwa nao, lakini tuwakaribishe wananchi wenye uwezo wa kuingiza matrekta waingize, tusitegemee serikali kila kitu. Serikali ina mambo mengi na mambo mengi hayo yote kwa jamii yetu na vijana wetu na wananchi wetu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kama wananchi wataambiwa tu mnaingiza mabasi ingizeni, magari ya mizigo lakini leteni na matrekta. Naamini katika matrekta hayo wakipewa mpango mzuri kodisha kwa kiasi fulani kinachokubalika kutokaana na hali za wananchi wetu, basi zao la mchele litaongezeka mara mbili kuliko tulivyo. Lakini tukisema serikali tu matrekta 20 siku nyengine kuna mtu mmoja tu anaweza kuyaleta hapa akafanya kazi mote Unguja na Pemba. Hivyo, tutoe wito tu kwamba kila anayetaka kuekeza katika

sehemu ya kilimo akaribishwe, hatuna ardhi ya kumpa yeye, tuna ardhi ya kulimiwa hiyo kidogo tuliyokuwa nayo kwa manufaa ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, hili litatusaidia kama nilivyosema na linafaa zaidi kusaidiwa. Lakini jengine kuongezeka kwa usafirishaji wa zao la karafuu, na hili tumeliona zuri, kuongezeka kwa uhamasishaji wa uwekezaji ndani na nje miradi mipya.

Mhe. Mwenyekiti, huangalia sana hapa Zanzibar ardhi yetu ni ndogo, lakini kilio kikubwa watu waje kuekeza si vibaya. Lakini hiki kidogo tulichokuwa nacho tukidhibiti, lakini ndio tunakaribisha watu haya mengine kuna maeneo yamekaa mpaka leo hayajengwa. Maeneo makubwa mtu kachukua hapa siku nyengine mpaka Kiembesamaki au padogo, eneo lile limekaa kimya halijaguswa na mtu yeyote mwenye mali kakaa tu kimya. Tutafute taratibu ambazo ni za kisheria wale wote wenye maeneo ambayo wameyaweka hawajayafanyia kazi, basi serikali iyachukue iwape wengine wanaotaka kutekeleza hayo kwa ajili ya manufaa ya nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, uwezekano huo kama utachukuliwa manufaa yataongezeka katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nitalozungumza hapa shabaha na malengo ya uchumi, ukurasa wa 20…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe una dakika tatu.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Eeh!

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika tatu.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Haya, Mhe. Mwenyekiti basi kwakuwa muda umekwenda niseme tu labda mwelekeo wa mapato, ukurasa wa 20, kifungu cha 51.

Kwa mwaka wa fedha 2018-2019 serikali inatarajia kukusanya jumla ya trilioni 1.21, hii ni sehemu kubwa na tumepata faida kubwa. Kwahivyo, namuomba Mhe. Waziri tuongeze bidii, tukusanye mapato kwa wingi, ili tuhakikishe kwamba Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ukurasa wa 23 inatekelezeka kwa wale wote waliogombea 2015-2020. Mhe. Mwenyekiti, nampongeze sana Mhe. Waziri, kitabu hiki ni kizuri sana, kifupi sana, kina mambo mengi ambayo yanakidhi haja kwa maendeleo ya nchi yetu. Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti naikubali ripoti hii na nampongeza sana Mhe. Waziri nimeikubali kwa asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru sana Mhe. Ali Suleiman Ali Mwakilishi wa Kijitoupele kwa mchango wako. Sasa, naomba nimwite Mhe. Rashid Makame Shamsi, atafuatiwa na Mhe. Machano Othman Said na Mhe. Asha Abdalla Mussa ajiandae.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu kuhusiana na mwelekeo huu wa kibajeti 2018-2019.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango na watendaji wake wote kwa kuweza kuwasilisha hotuba hii ya Mkabala wa Uchumi,

Mpango wa Maendeleo na Bajeti kwa mwaka 2018-2019. Lakini, nimpongeze pia Mwenyekiti pamoja na Kamati yake ya Bajeti kwa uwasilishaji wao na maoni yao. Pia niwapongeze na wajumbe wenzangu ambao wamenitangulia juu ya michango yao ambayo ina lengo na nia ya kuweza kujenga na kuimarisha uchumi na kipato cha nchi hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii ya mwelekeo wa kibajeti ni nzuri, imepangika vizuri na iko wazi, ni fupi lakini yenye kueleweka. Nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa upangaji wake wa ripoti pamoja na watendaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, ninaanza kuelekeza michango yangu katika suala la kitakwimu zaidi, kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuisoma ripoti hii pamoja na kwamba wenzangu Mhe. Suleiman Sarahan Said alizungumzia changamoto ya kitakwimu kwenye utalii, mimi sitaki niogelee huko lakini nielekee katika ukuaji wa deni la taifa.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukuaji wa deni la taifa Mhe. Waziri katika ukurasa wa 15 alieleza kwamba katika ukuaji wa deni la taifa 2016 ilikuwa ni 369.5 bilioni, ukilinganisha na 2017 shilingi 436.22 bilioni.

Mhe. Mwenyekiti, wasi wasi wangu takwimu ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango inasutana kidogo na takwimu ambayo tuliipata katika ripoti ya Kamati ya Bajeti ya 2018, ambapo wao walisema kwamba ukuaji wa deni la taifa ni 401.6. Sasa hii ni hatari kidogo tunapopata vyanzo tofauti au *figure* tofauti za kitakwimu, kwasababu tunaweza tukapotosha wananchi. Ni vyema sana takwimu zetu zikawa zinachukuliwa katika chanzo kimoja. Nafikiri Tume ya Mipango ndio ambayo inaweza ikaona bajeti ya uhakika juu ya hilo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwenye ukusanyaji wa mapato 2017-2018 taarifa za Waziri wa Fedha na Mipango katika ukurasa wa 11 inasema kwamba ilipangiwa kukusanya shilingi 187.3 bilioni. Lakini katika Kamati ya Fedha, Ripoti ya Kamati ya Fedha iliyowasilishwa juzi ina 159.4 bilioni, lakini kwenye Kamati ya Bajeti iliyowasilishwa kuna 187.4 bilioni. Takwimu hizi za ukusanyaji wa mapato ndani ya mwaka huu zinatofautiana, sasa sijui tukamate ipi. Lakini mimi najua *source* nzuri ya habari hizi ni Tume ya Mipango, kwahiyo tunapowasilisha hizi takwimu kwakweli tunahitaji umakini mkubwa na mimi napendekeza tuwe na chanzo cha uhakika ya takwimu ambazo tunazileta Barazani kwa sababu wananchi wanatusikia.

Mhe. Mwenyekiti, nikotoka katika suala la kitakwimu nije sasa katika suala la maeneo ya vipaumbele. Mhe. Mwenyekiti, naungana mkono sana na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango juu ya maeneo muhimu ambayo yameanishwa juu ya vipaumbele katika mwelekeo wa bajeti 2018-2019. Maeneo yote yaliyotajwa yana umuhimu wake kwa wananchi na kwa mustakaba mkubwa sana wa uchumi yetu.

Wenzetu wa Kamati ya Bajeti kama alivyotangulia kusema Mhe. Waziri wa Fedha walitoa hoja juu ya kuona kwamba maeneo hayo ya vipaumbele ni mengi ukilinganisha kwamba katika mwelekeo wa mwaka jana kulikuwa na maeneo matano. Lakini katika mwelekeo huu tunaoenda nao 2018-2019 maeneo hayo yameongezeka kutoka matano kuja maeneo tisa. Sasa wenzetu wana wasi wasi pengine juu ya

utekelezaji wake. Hivyo, kitaalamu unaweza ukaongeza maeneo katika suala zima la vipaumbele, pamoja na kwamba ni vizuri kuwa na maeneo kidogo sana. Napenda ninukuu ripoti ya 2017-2018.

"Serikali inaelewa haja ya kuwa na maeneo machache ya vipaumbele kwa utekelezaji, ili kuweza kuwa na matokeo mazuri zaidi".

Mhe. Mwenyekiti, hii ni hotuba ya 2017-2018 kwamba serikali inaelewa umuhimu wa kuwa na maeneo kidogo ambayo yanaweza kutekelezeka. Lakini hiyo sio neno suala ni kuweza kujiuliza katika maeneo matano ya mwaka jana ule ufanisi wake uko vipi. Ukiweza kujitathmini kwamba kwenye maeneo ya vipaumbele vya mwaka uliopita tumefikia wapi, hivyo tunakuwa na *access* ya kuweza kuongeza na maeneo mengine. Lakini kama tunakuwa na mapungufu maana yake sio busara sana kuweza kuwa na maeneo mengi ambayo wakati mwengine hayatekelezeki.

Kwahiyo, niombe sana cha muhimu kikubwa sana ni tathmini, tathmini lakini na hali ya mapato ya nchi yetu. Vilevile, suala jengine ambalo linajitokeza unaweza ukawa na mapato mazuri lakini ukakosa ule ufuatiliaji na usimamizi mzuri wa maeneo yenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, nashauri tu kwamba tuangalie hali ya uchumi na uwezo wetu katika kusimamia hayo maeneo ambayo tumeyapanga. Lakini suala la uhaba na wingi nafikiri inategemea vilevile uwezo wetu wa kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti, katika maeneo ya vipaumbele nimeweza kuangalia maeneo mawili, suala zima la kuimarisha zaidi utalii wa nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, hili eneo ni muhimu sana katika suala zima la maendeleo ya kiuchumi ya nchi yetu kwa sababu asilimia kubwa sana ya fedha za nje inategemea sana sekta hii ya utalii.

Sasa kuna haja katika programu ambazo zitaandaliwa na kuidhinishiwa fedha tuna suala la utalii kwa wote. Suala hili la utalii kwa wote kwa kweli ilikuwa ni nyimbo, lakini utekelezaji wake bado haujashamiri, na hili linaweza likasaidia uchumi wa mtu mmoja mmoja kama kila mwananchi wa nchi hii atakuwa anashirikishwa katika suala zima la utalii. Kwa hiyo, lile agizo la Rais juu ya utalii wa wote, mimi nafikiria linapaswa kuangaliwa zaidi katika mwaka huu wa fedha unaokuja ili kuweza kuona wananchi wetu wananufaika na sekta hii.

Mhe. Mwenyekiti, lakini bajeti katika Kamisheni ya Utalii. Kamisheni hii ndio chombo muhimu sana ambacho kinaitangaza na kuweza kushajihisha wawekezaji kuweza kuja nchini katika suala zima la utalii pia na wageni. Sasa bajeti yake kwa kweli inahitaji kuongezwa kwa sababu wenzetu wana kazi kubwa. Nchi yetu kama hii inapaswa kuwa na *centre* ambazo watalii watakuwa wanapata *information* na wanzetu walikuwa na prgramu hiyo ambayo mpaka leo imeshindikana.

Sasa ni vyema sana wenzetu tuwatizame hii kama tunataka kuweza kuona kwamba utalii unaongezeka. Vilevile, katika kuimairisha na kuongeza vile vivutio zaidi. Tuna maeneo mengi ya kuweza kuongeza ili kuwe na vivutio, kulikuwa na mbio kwa mfano za *marathon* na *triathlon* hapa Zanzibar, ambazo zilikuwa zinaongeza wageni kuja nchini, hivi sasa hivyo vitu vimepotea. Kwa hivyo, tunaweza tukaa tena

tukafikiria baadhi ya vianzo vyengine vya kiutalii ambavyo vinaweza vikavuta wageni zaidi.

Lakini, nikizungumzia kwa mfano msitu wa Jozani tunapokea taarifa kwamba wageni wanaoingia nchini, basi hata robo hawafiki wanaotembelea msitu ule ambao ni kivutio chetu. Sasa tunahitaji kutangaza zaidi. Hivyo, ni vyema kuangalia ndani ya msitu ule kuna vianzo gani ambavyo ni vivutio.

Jambo la kusikitisha Mhe. Mwenyekiti, kila mwaka msitu wa Jozani unaingia moto hata mwaka huu tumepata ripoti hiyo. Sasa chanzo hichi kinaweza kikakifaka wakati basi kisipate wageni. Ni vizuri sana sekta inayohusika kuweza kuangalia tatizo liko wapi kwamba kila mwaka msitu huu unapoteza ekari nyingi kwa kuingia moto. Sasa ni vyema sana kuweza kuangalia suala hili.

Suala jengine ndani ya utalii ni utalii wa makundi *package tour*. *Package tour* ni aina ya utalii ambayo kwa nchi yetu kwa kweli inatupunguzia yale mapato halisi ambayo tunayatarajia. Ni vyema sana wizara au taasisi zinazohusika kuweza kuangalia kasoro za aina hii ya utalii ili nchi yetu iweze kunufaika nayo.

Lakini jengine nimeangalia suala la kuimarisha kilimo kwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji maji. Katika eneo hili Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka huu unaokuja tunatakiwa tuweze kuangalia mambo muhimu ambayo hivi sasa ni kero kwa wakulima wetu. Ni kweli kwamba suala la umwagiliaji maji haliko katika kiwango kikubwa na tunapaswa kuweza kulitizama, ili wakulima wetu wengi waweze kulima kwa kumwagilia, ili tuwe na chakula kingi cha ndani kuliko kile cha kuagiza nje.

Suala kubwa sana wanalalamika wakulima hata juzi kwenye vyombo vya habari ni utayarishaji wa mashamba, utayarishaji wa mashamba unachelewa na hii kutokana pengine na uhaba wa matrekta. Lakini walizungumzia juu ya utaratibu wa maafisa kilimo wanahisi hawaelewi vyema ule wakati wa kuweza kutayarisha mashamba. Kwa hiyo, hapa taaluma inahitajika.

Kwa kweli, wanasikitika sana juu ya matrekta kushindwa kufanyakazi zake vizuri kutokana na ukavu wa ardhi. Sasa sijui kama ni aina ya matrekta au ni kasoro ya ardhi yetu. Lakini nalo ni suala la kuweza kutizama kwasababu linawatia wakulima hasara katika kutumia jembe la mkono. Lakini jengine ni kupatikana kwa pembejeo bora na zipatikane kwa unafuu na kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka katika vipaumbele hivyo viwili nije sasa nimalizie katika suala zima la deni la tiafa. Mhe. Mwenyekiti, imeelezwa katika ripoti hii kwamba kuna deni la taifa bado limesemwa linahimilika kwani ni sawa na asilimia 16.5 tu ya pato la taifa. Hii inaonesha kwamba tuko katika hali nzuri na nivipongeze vyombo vya ukusanyaji wa mapato lakini vilevile serikali kuweza kupunguza deni.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, katika muelekezo ya bajeti tunayokwenda kutakuwa na nakisi ya bajeti ya Tanzania shilingi 35 bilioni ambazo nakisi hii imeelezwa kwamba itazibwa na mikopo ya ndani. Sasa tukitizama lile deni ambalo tunalo halafu na huku kutakuwa na nakisi ya bajeti ambayo tutalazimika kuweza kuziba shilingi hizo thalathini na tano bilioni za mikopo ya ndani.

Je, tukichanganya na ile *speed* ya kuweza kulipa lile deni tulilokuwa nalo, kwasababu hapa lazima kuna mambo mawili, ile *speed* ya kulipa deni ambalo tunalo na huku kuna nakisi hiyo ya thalathini na tano bilioni maana yake tuweze kujaza hiyo. Je, bado taifa letu litakuwa deni hili la taifa litakuwa linahimilika. Kwa sababu kama halihimiliki maana yake tuweze kutizima hii hali, vyenginevyo tunaweza tukaja kujikuta kwamba taifa lina deni kubwa sana.

Mwisho, kabisa Mhe. Mwenyekiti, niipongeze sana kamati na wenzetu wameomba kwa sababu hii ni kamati mpya ambayo inalingana na ile kamati yangu ya Kanuni kwa ufupi mafunzo kwa kamati hii ni muhimu sana. Wenzetu wapatiwe mafunzo zaidi, ili wawe na uwezo mkubwa wa kuweza kumudu majukumu yao mazito ya masuala mazima ya bajeti ya nchii. Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, niunge mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Rashid Makame Shamsi Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite, Mhe. Asha Abdalla Mussa atafuatiwa na Mhe. Machano Othaman Said na nimekuona Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil basi pia ujiandae.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ili kuweza kuchangia hotuba ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo na Mwelekeo ya Bajeti ya mwaka 2018-19.

Mhe. Mwenyekiti, niungane na wenzangu kumpongeza Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na watendaji wake wote, ambao wameweza kutayarisha hotuba hii na hii leo kuweza kuiwasilisha katika Baraza hili tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kitabu hichi tukikiangalia kwa haraka haraka tunakikuta kimechambua mambo mengi, tena yamefafanuliwa kwa kina na vilevile imeonesha hali halisi nzima ya ukuwaji wa uchumi kwa dunia nzima pamoja na uchumi wa Zanzibar. Lakini Mhe. Mwenyekiti, pia tumeona utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2016-17, pia tumeona muelekeo, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya mwaka 2017-18 kwa kipindi cha muda wa miezi sita.

Mhe. Mwenyekiti, niungane na Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kwa kuchangia machache kabisa katika hotuba hii kama alivyotangulia kusema Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Bajeti mimi nikiwa Mjumbe wa Kamati hii ya Bajeti ambapo tulipitia jana hotuba hii kwa kina na kuweza kutoa maoni yetu. Naomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango aweze kuchukuwa maoni ambayo ya Wajumbe ambao watakaotoa hapa ili kwa kuweza kuyafanyia kazi na kuifanya sura ya bajeti ya mwaka 2018-19 iwe ambayo imejaa mambo mengi na iweze kutekelezeka kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nitanza kuzungumzia ukurasa wa 3 mpaka wa 4 kutokana na ukuaji wa uchumi wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, tumeona kwamba lengo la serikali kwa upande wa utalii tumeona jinsi ya uingiaji wa watalii ulivyokuwa. Lakini Mhe. Suleiman Sarahan hapa na yeye alipokitizama kitabu hichi ameona mkanganyiko wa takwim ni kweli hata na mimi nimeona kwa sasa hivi maana jana tulipitia kwa haraka haraka ukilinganisha na Ripoti ya Kamati ya Utalii ambayo tuliyoipitisha juzi, tumeona kwamba kuna ukanganyiko wa takwimu ya watalii. Kwa mwaka 2016

tuliona kwamba kuna watalii ambao wameongezeka laki tatu na sabini sita mpaka kufikia laki nne na thalathini na tatu elfu.

Kwakweli, katika hotuba hii ya Mhe. Waziri imeonesha kwamba kuna ongezeko la watalii wafikao laki moja na sabini mia tano thamanini na moja. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha akae kwa kina pamoja na watendaji wake waangalie kwa umakini zaidi ili waweze kuleta takwim sahihi ambayo ya ongezeko hili la watalii hapa nchini. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini ningependelea zaidi ili kuimairisha sekta hii ya utalii hapa Zanzibar na kuweza kuleta ajira nyingi kwa vijana wetu, lakini pia kuweza kuwavutia wawekezaji, ili waweze kuja kuekeza zaidi hapa kwetu Zanzibar. Hivyo, naomba sana serikali kupitia ripoti hii au hotuba hii katika utekelezaji wa mwaka 2018-19, basi tuone kwamba inapatikana takwim halisi ya wawekezaji ya watalii hapa nchini, lakini pia tuone kwamba tuimarishe miundombinu katika maeneo ya uwekezaji hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, nikija kwenye ukurasa wa 19 kwenye Mwelekeo wa Hali ya Uchumi ya Zanzibar ambao tunauona ifikapo mwaka 2018-19. Mhe. Mwenyekiti, tunatarajia kukua kwa kiasi cha wastani asilimia 7.1 matarajio ambayo tunayategemea kwa kipindi cha mwaka 2018-19 na tumeona mambo ambayo tukiyafanikisha tunaweza kufanikiwa kwa asilimia hiyo 7.1. Kwanza uzalishaji wa mazao ya chakula pamoja na ununuzi wa matrekta.

Kwakweli, niwapongeze sana Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuona suala hili na tunaona kwamba asilimia kubwa ya wananchi wa Zanzibar ni wakulima na tunategemea sana kilimo, tutakapoongeza haya matrekta 20 na yale 20 ya mwanzo nadhani tutafikia lengo ambalo tumekusudia katika sekta hii ya kilimo. Mhe. Mwenyekiti, tunaweza kuzalisha mazao zaidi pamoja na kutengeneza ajira nyingi zaidi kupitia kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuna mambo mengi hapo wameelezea kwamba kutakuwa na uhamasishaji wa wawekezaji hapa nchini, narudia tena kwamba naomba sana sekta hii ya utalii izidi kutangaza katika nchi mbalimbali, ambazo watalii wake wanaingia hapa nchini kwa idadi ndogo, lakini tuweze kuwatangazia nchi ambazo wanaweza kuja watalii wengi na kuweza kuingiza mapato zaidi katika nchi yetu hii ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie la mwisho kwamba vigezo vya ukuwaji wa rasilimali fedha katika ukurasa wa 22 mpaka 23. Mhe. Mwenyekiti, katika ripoti hii tumeona kwamba mambo ambayo watazingatia katika rasilimali fedha ikiwemo vipaumbele vya taifa vya mwaka 2018-19. Vilevile, tumeona maagizo maalum ya serikali kwa mujibu wa vipaumbele vya taifa, pia tumeona programu na miradi yote ambayo iliyokuwa haijakamilika katika kutekeleza shughuli za mwaka 2017-18.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo zuri sana na ni jambo jema wenzetu kuona kwamba wakati kabla ya kuona mambo ambayo wanaweza kuyaweka katika vipaumbele vya mwaka 2018-19 wameona kwamba wazingatie mambo ambayo hayakuweza au vipaumbele ambavyo havikuweza kukamilika katika mwaka 2017-18.

Mhe. Mwenyekiti, naamini kwamba ukiangalia zaidi uchumi wetu wa Zanzibar tunaweza kupanga vipaumbele ambavyo vile vinaweza kutekelezeka, tukizingatia

hivyo tunaamini kwamba tutaweza kufikia lengo kwa asilimia mia moja, pamoja kukusanya mapato zaidi ya yale ambayo tumeweza kuyakusanya ndani ya mwaka huu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haya machache kabisa niungane na wenzangu kwa kuunga mkono kwa asilimia mia moja hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ambayo ameiwasilisha hapa Barazani. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Asha Abdalla Mussa Mwakilishi wa Jimbo la Kiwengwa kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe kabla sijamwita Mhe. Machano Othman Said naomba niutambulishe ugeni uliotufikia hivi punde wangeni hawa ni wa Mhe. Waziri wa Mawasiliano, Ujenzi na Usafirishaji Mhe. Balozi Ali Karume. Wageni wenyewe ni kama wafuatao wa kwanza Dkt Abdalla Hasnuu Makame (Mwenyekiti wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kutoka Tanzania) na pili Muhandisi, Moh'd Habib Mnyaa. Mhe. Mwenyekiti wa Wabunge wa Afrika Mashiriki kutoka Tanzania pamoja na Mhe. Moh'd Mnyaa karibuni sana. (*Makofi*)

Sasa naomba nimwite Mhe. Machano Othaman Said atafuatiwa na Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil na Mhe. Abdalla Ali Kombo ajiandae.

Mhe. Machano Othaman Said: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Mpango wa Maendeleo ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Lakini pili naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote wa Wizara ya Fedha na Mipango na zaidi Tume yetu ya Mipango ya Zanzibar kwa mpango huu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika matarajio ya mwaka 2018-19 tunatarajia kukusanya trilioni moja nukta moja saba tano, ambazo zitakuwa ni matumizi na makusanya ya serikali. Mhe. Mwenyekiti, mpango huu ni mzuri na kama walivyoanza wenzangu nichukuwe fursa hii kuishukuru sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwanza kwa kukusanya vizuri mapato yake ya serikali lakini pia kwa matumizi mazuri ya serikali. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti wakati akiwasilisha maoni ya kamati alizungumzia kwamba utekelezaji wa bajeti ni karibu asilimia 70. Kama hivyo, ndio kweli basi pia ni jambo jema na la maana sana, kwasababu si nchi nyingi katika Afrika ambazo zinapanga bajeti zikafika alau asilimia 60 ya matumizi ya mpango huo walioupanga. Kwa bahati nzuri sisi huku *backbenchers* tuko kwenye Kamati za Kudumu za Baraza tukienda kwenye wizara tunauliza tunaona na tunatoa kwenye mchango wetu kwa hakika kwa wizara nyingi wamepata fedha nyingi katika bajeti kama walivyoomba. Lakini ukiangalia pia Taasisi zetu Kuu za *ZRB* na *TRA* malengo yao ya makusanyo ya fedha wamekusanya kwa zaidi ya asilimia mia moja, hili ni jambo la maana sana.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie vipaumbele ambavyo vimezungumzwa humu na nimewasikia baadhi yao kina Mhe. Suleiman Sarahan na Mhe. Ali Suleiman Ali wakiviunga mkono lakini pia kuweka msisitizo. Mhe. Mwenyekiti, nataka kuweka

msisitizo vipaumbele vya serikali ni vizuri lakini miongoni mwao vingi vyao vinategemea baadhi ya vipaombele ukisema unazungumzia utalii maana yake lazima uzungumzie na miundombinu iliyokuwa safi na salama na miundombinu hiyo lazima uwe na maji safi na salama uwe na barabara nzuri lakini uwe na nishati ya umeme ya kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, bado tunalo tatizo la ukosefu wa maji safi na salama katika maeneo yetu. Kwakweli, naamini kama Waheshimiwa Wawakilishi 54 wenye majimbo, ukiwasimamisha mmoja mmoja na uwaulize wewe kipaumbele chako nambari moja ni nini au tatizo lako ni nini, changamoto yako ni nini, basi atasema maji, ukimuuliza tena mara ya pili tatizo lako ni nini basi atasema ni maji, na ukimuuliza mara ya tatu atakuambia ni maji. Kwa hivyo, kwa ujumla tunalo tatizo la maji.

Mhe. Mwenyekiti, sisi ambao tunawawakilisha wananchi tunajiuliza kulikoni, kwasababu tunaelewa na tunafahamu, kwamba serikali inatumia fedha nyingi katika sekta ya maji, lakini bado tatizo la maji ni kubwa. Kutokana na hali hiyo, ombi langu kwa serikali kwa kupitia mpango huu, kwamba mwaka huu wa 2018/2019 uwe mwaka wa marekebisho wa kuimarisha miundombinu ya maji na wananchi wa Zanzibar wapate maji safi na salama kwa kiwango kikubwa. Tukiweza kufanikiwa maji, tunaweza kukuza uchumi kwa wananchi kufanya shughuli zao nyengine za maendeleo, lakini pia na watalii kuja hapa wakiwa na uhakika wa kupata maji safi na salama.

Pili Mhe. Mwenyekiti, ni barabara. Katika kipindi hiki barabara zimeharibika nyingi kwa mvua. Kwa mfano, katika mkoa ambao kwa Zanzibar unapokea watalii wengi ni Mkoa wa Kaskazini Unguja, ndio ambao una mahoteli makubwa, una wageni wengi na una mazingira mazuri. Lakini ili ufike Kaskazini ni lazima upitie njia ya barabara ya Bububu. Ukianzia pale Kwakisasi mpaka Kwanyanya barabara haipitiki. Kuna kipindi watu walikuwa wanakimbia barabara hii wanapitia Kianga, Kitundu, Mwakaje halafu ndio wanaunganisha kwenda Kaskazini. Ingawa serikali tunaelewa kwamba ina mpango wa kujenga barabara mpya, sasa hivi nasikia kuanzia Kwanyanya kwenda Kaskazini. Lakini ule mradi ni kuanzia Kinazini mpaka Kikwajuni.

Kwa hivyo, mimi niombe kwamba kama ule mradi wa Kichina, ambao unajengwa na Wachina utaanzia Kwanyanya, basi serikali iwe na mpango mwengine wa kuanzia barabara, kuanzia pengine Kinazini mpaka Kituo cha Polisi Bububu mpaka huku mbele kumalizia. Mhe. Mwenyekiti, na kama ule ule unawezekana kuanzisha angalau Kituo cha Polisi Bububu kwenda mbele, pia itakuwa afadhali sana.

Mhe. Mwenyekiti, barabara pia katika maeneo ya Kaskazini. Kwa mfano, barabara ya Kijini, barabara ya Mkokotoni yaani Chaani Mkokotoni, nazo hizi ni lazima ziingizwe katika mpango wa kuimarisha na kuinua utalii wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tumefurahi katika mpango huu pia watashughulikia maendeleo ya majengo yetu kama *Airport*, nafikiri mara hii litamalizika jengo la *Airport*. Pia wataimarisha milango yetu ya bandari. Mhe. Mwenyekiti, hili litakuwa ni jambo la faraja sana. Pia ule mpango wa kujenga bandari binafsi katika maeneo ya huko Mangapwani nao ni mwema na utatusaidia katika kuimarisha uchumi wetu.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie Mfuko wa Miundombinu. Mhe. Mwenyekiti, mfuko huu umeanzishwa kwa lengo zuri na kwa bahati nzuri niipongeze serikali makusanyo yake yanakuwa mazuri. Kwa mwaka huu wa fedha wa 2018/19 wanatarajia kukusanya bilioni 34.9, hizi ni fedha nyingi. Lakini namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango na timu yake wajitahidi sana hizi fedha ziende katika miundombinu.

Tunalo tatizo bado kwa maeneo kama ya umeme kuunganisha kwa wananchi, kwasababu unaweza kusema inakaribia asilimia 90 pengine ya vijiji vya Zanzibar vinapata umeme, lakini inakuwa kijiji moja tu kimepata umeme kidogo, lakini maeneo mengi ya vijiji vile havina umeme na wananchi wengi wa maeneo yale wanataka umeme katika shughuli zao. Kwa hiyo, tukiweza kupata umeme katika vijiji vyetu, basi hata matumizi ya ukataji wa miti na kuni yatapungua na ukipunguza kutumia kuni na mambo mengine, maana yake unawasaidia wananchi kuimarisha uchumi wao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwe na mpango maalum wa serikali, ukiacha ile miradi mikubwa ya serikali ya upelekaji wa umeme, kuwe na mpango maalum wa kuwawezesha wananchi kuunga umeme au kujiungia umeme kwa utaratibu ambao hata kama kurejesha fedha baadae kidogo kidogo, lakini wananchi wawe wameweza kuungiwa umeme. Ni matarajio yangu kwamba tukiweza hili litasaidia sana katika shughuli zetu za maendeleo.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu hiki Mhe. Waziri pia kazungumzia tatizo la ajira kwa vijana. Kazungumzia vijana wa aina mbili, kazungumzia vijana kati ya umri wa miaka 15 na 35, tatizo lao ni karibu asilimia 21 na nusu. Lakini vijana kati ya miaka 20 na 24 ambao hawa ndio nguvu kazi halisi ya vijana, wana tatizo la ajira la asilimia 28.5 na kwa ujumla hatuwezi kuilaumu serikali kwasababu tunaujua uwezo wa serikali yetu.

Lakini nakumbuka upo mradi nao aliletwa mgeni, nafikiria alikuwa Serikali ya Rwanda walimtumia sana halafu akaja na Zanzibar ambaye nafikiri yuko kwenye Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Hivi tumefikia hatua gani na mradi wetu ule, kwasababu ukisema kila ambaye anamaliza chuo au anamaliza sekondari aende serikalini, basi hata wale watu aliowasema Mhe. Suleiman Sarahan kwamba leo tunawaajiri watu 50 itakuwa kidogo sana, kwasababu vijana wenyewe kila siku wanamaliza skuli na vyuo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri viongozi wetu wanasisitiza kila siku kwamba mtu asome, ili akimaliza Chuo Kikuu aweze kujiajiri mwenyewe. Sasa tuna wahamasisha vipi, tuna wasaidia vipi wale vijana ili waweze kujiajiri na kuondokana na hii asilimia 28, kwasababu kwa Zanzibar asilimia hii ni kubwa sana. Miaka mitano nyuma nafikiri ilikuwa ni asilimia 17, mitano, sita, saba au nane ilikuwa asilimia 17, sasa hivi asilimia 28 unakuta vijana hawana ajira. Maana yake ni nini kama vijana hawana ajira, maana yake mpaka mtu anafika miaka 24 anangojea alishwe na baba yake na mama yake, anafika wakati anaowa bado alishwe na baba yake na mama yake. Pengine atajukuu bado analishwa na baba yake na mama yake.

Sasa haya mambo yatatuumiza Mhe. Mwenyekiti, na yatarudisha uchumi wa nchi yetu, kwasababu inakuwa kila mtu hawezi kujitegemea kwasababu hakuandaliwa

kujitegemea. Kwahivyo, ni vyema Labda, kwa sababu nchi za wenzetu wanafanya, tungebadilisha pia na mfumo wa elimu yetu kuanzia sekondari iwe kuna vijana wanatayarishwa kuweza kujiajiri wenyewe ili kupunguza pengo la serikali la ajira. Sasa hivi serikali inatangaza nafasi za ajira 10, wanakwenda kufanya *interview* watu 3,000, naamini hata wale waliotangaza baadae wanaona aa! hata hizo barua zao kuzifungua inakuwa ni shida.

Kwa hivyo, naomba tu kwamba wakati tumewapata wale wataalamu kutoka nje wa kutusaidia mambo haya ya ajira, basi wajipange vizuri katika kuwatumia, ili tuweze kupata ile faida ambayo tulikusudia kupata.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mipango ya SMZ na mafanikio yake, ni lazima serikali iwe makini na iangalie sana. Jana gazeti moja nafikiri la Nipashe lilikuwa linazungumzia kwamba Zanzibar sasa ndio uchochoro wa madawa ya kulevya, tena mazungumzo haya ananukuliwa Kamishna wa Operesheni wa Taasisi ya Kupambana na Madawa ya Kulevya upande wa Tanzania Bara, ama lengo lilikuwa kusema huo ukweli au lengo jengine ni kwamba na sheria ile itumike huku, maana yake alikuwa anasema sheria ya Zanzibar dhaifu inatolesha faini milioni 20 au miaka 20 jela, kule Bara wanasema sisi huku tunafunga maisha. Akasema mpaka wale waliokwenda China juzi hawakupitia huku Bara, wamepitia kwa Zanzibar halafu wakenda zao China.

Sasa ukweli wenyewe hatuujui lakini tunaona kwamba hebu kama na sisi sheria zetu ziko dhaifu basi tuzirekebishe wenyewe Baraza la Wawakilishi ili tuendane na wakati, ili ile sababu kwamba Zanzibar ndio uchochoro wa madawa ya kulevya iondoke, kwa sababu nalo hili linadumaza ukuaji wa uchumi, kama tutakuwa hatuaminiki katika mapambano haya ya madawa ya kulevya, basi tutakuwa tunarejesha nyuma mapambano dhidi ya madawa ya kulevya, lakini ukirejesha nyuma mapambano haya maana yake pia unaudumaza uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa sababu ukiangalia hapa Zanzibar Januari hadi Machi 2016 uchumi umekua kwa asilimia 5, lakini Januari/Machi 2017 uchumi umekuwa kwa asilimia 6.3, hili ni jambo la kupongezwa serikali imejitahidi sana. Kwa kweli, naamini tuko salama sana kiuchumi sasa hivi Zanzibar, lakini lazima tumuunge mkono Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, serikali na serikali yenyewe ijuwe kwamba vita vya kiuchumi ni vikubwa. Kwa hivyo, lazima yale mapengo na kasoro ndogo ndogo zote tuziondowe ili tujenge uchumi, naamini tukienda hivi vizuri basi mwaka 2020 tutakuwa tuko katika asilimia pengine hadi 8. *(Makofi)*

Jambo la mwisho Mhe. Mwenyekiti, huu ni mpango wa 2018/2019, lakini tujuwe kwamba tumebakiwa na miaka miwili ya uchaguzi, ni lazima tuangalie na uchaguzi wetu tutauendeshaje kwa kupitia mipango yetu hii ya maendeleo. Tusije tukafikia kama Burundi. Burundi uchaguzi wao wananchi wameambiwa lazima wauchangie wenyewe wananchi wote wa Burundi, na lazima utowe fedha katika kuandaa uchaguzi. Sasa sisi ni lazima tujipange, unajua bajeti ijayo ya mwaka 2019/2020 na 2020/2021 zitakuwa ngumu kidogo katika makusanyo na matumizi yake.

Kwahivyo, lazima, wakati huu mpango amesema Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, huu mpango unaweza kubadilika kidogo, basi nashauri na kuomba ubadilike kidogo kwa kuingiza vielekeo, sio viashiria, vielekeo vya kuelekea uchaguzi wa 2020 ili

tusije tukayumba hapo katikati. Tunajua karibia uchaguzi basi hata mapato ya serikali yanaweza kupungua kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu ulikuwa huo mdogo. Nakiunga mkono hiki kitabu na naomba tuendelee na mpango huu kama ambavyo Mhe. Waziri ameupendekeza. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru sana Mhe. Machano Othman Said Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Ahmada Yahya, atafuatiwa na Mhe. Abdalla Ali Kombo, kama muda utaturuhusu basi Mhe. Hidaya Ali Makame ajiandae.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii mchana huu kwa ajili ya kuchangia hotuba ya Mkabala wa Uchumi, kuelekea Mpango wa Maendeleo na Mwelekeo wa Bajeti wa mwaka 2018/19.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kuishukuru na kuipongeza wizara hii pamoja na wataalamu wote ambao wameandaa kitabu hiki kidogo, lakini chenye maudhui makubwa na chenye kutuvusha katika jahazi la uchumi kuelekea mwaka 2018/2019. Roho yote iko hapa kwa kushirikiana na Tume ya Mipango. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika uchangiaji wangu nitakuja kwenye ukurasa wa 4.10. Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Fedha na Mipango siku za nyuma kulikuwa na mpango wa ku- *harmonize* uchumi, ukiitwa *Open General License,* ambazo zikisaidiwa na *Stabex Stabilising of Export* vitu viwili hivi na hizo ni *harmonisation* za uchumi. Hizi zilikuwa zinasaidia sana watu kuagiza bidhaa nchi za nje.

Mhe. Mwenyekiti, Wafadhili wa Maendeleo, leo tunawaita washirika wa maendeleo wanakuwa wanatia fedha baada ya mazungumzo yenye tija, ambazo zinakuwa-*supported* na wafanyabiashara kuagizia bidhaa nchi za nje. Kwa hivyo, kunakuwa hakuna uyumbishaji wa fedha za kigeni, kwasababu mfanyabiashara anatumia fursa ile ya *OGL* kwa kuweka *local money*. Kwa hivyo, uagiziaji wa bidhaa unakuwa mkubwa zaidi na usafirishaji kwa kutumia *Stabex* yaani, *stabilising of export*, sijui kauli ya serikali au Mhe. Waziri ule mpango bado unaendelea na ambao ulikuwa unawafanya wafanyabiashara waingize zaidi, na ndipo hapo uchumi ulipoanza kupaa wa Zanzibar, baada ya kuwepo *OGL* pamoja na *Stabex*, hivyo mpango ule sijui unaendelea au umeacha.

Mhe. Mwenyekiti, naamini ukuaji wa uchumi huu wa asilimia iliyoongezeka kwa kipindi kilichopita bado fursa ipo ya kuongezeka zaidi kuliko hapa na hasa tukirejea kule kwenye zile nukta mbili za *OGL* na *Stabex* hiyo nukta ya kwanza.

Nikija ukurasa wa 5 Mhe. Mwenyekiti, uchumi wowote duniani lazima uwe na rasilimali. Ni kweli tunatumia mfumo wa *cash budget*, tunapata tunatumia. Lakini mfumo wa kuwa na *real estate* zetu ni mfumo mzuri ambao utaongeza thamani ya nchi yetu. Kwa hivyo, upande wa nukta ya ujengaji wa Gati ya Mafuta Mangapwani, serikali ingefaa zaidi kulipa kipaumbele. Kadhia hii ya kuendelea leo mafuta yapo, kesho hakuna ni ukosefu wa pahala madhubuti pa kuhifadhi mafuta yetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, uchunguzi wa mwanzo nilioufanya kwamba katika Ukanda wa *East Afrika* Zanzibar tuna *potation* kubwa ya kuweka Gati ya Mafuta Mangapwani, kwakweli kina kikubwa cha maji na pahala pazuri. Kwa hivyo, nahisi serikali fursa ile ingechangamkia, ili tukazidisha mtaji wa kujenga *deport* yetu, mali yetu na tukaondokana na huu unyonge uliokuwa hauna faida, leo mafuta yapo kesho hakuna na wakati huo tutakuwa tumeongeza kwenye daftari la *assert* kwa ajili ya kujenga *deport* ile, hiyo nukta ya pili au ya tatu.

Nikienda kwenye nukta nyengine Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba bado tuna fursa kubwa ya ku-*harmonize* uchumi wetu. Suala la Bwawani ile ni mali na ni keki, suala la Viwanda Vidogo Vidogo ni mali na ni keki, *estate* zile tungepata kujua kwamba Bwawani imefikia hatua gani ya mpango wa maendeleo huu tunaosoma leo. Je, kutakuwa kuna mfumo au mabadiliko ya ukodishwaji wa mkataba wa awali au ndio bwana mkubwa kidogo na yeye ame- *shake* kwa hivyo na mradi nao pia ume- *shake.* Kwa hivyo, ningependa kusikia kauli ya serikali kwamba mali ile ni mali na lini itafufuliwa kusudi tuanze kushughulika na uchumi pale pahali pawe panazalisha.

Mhe. Mwenyekiti, lakini sio hapo tu, nashauri Wizara ya Fedha na Mipango, kwamba Viwanda Vidogo Vidogo ni pahali bora zaidi. Nilisema katika uchangiaji wangu, pale pahala kwa Zanzibar sasa hakuna pahali pazuri pa kuwekeza fursa kama ni pale, aidha kwa kukodisha majengo yale. Serikali ina mpango wa kujenga *gate* hivi karibuni, *shell* moja ile pale kwa siku za mbele itafika hata *ten thousand dollar per month,* leo zimekaa, zinavuja na haziko katika hali nzuri.

Kwa hivyo, nashauri ingeundwa *taskforce* ndogo tu ya kuyashughulikia majengo yale kuyafufua na tukarejesha heshima ya pale pahala na majengo yenyewe. Ikumbukwe kwamba pale kuna mwekezaji wa *Zantel* ambaye kila mwaka kwa namna moja au nyengine anaingia katika *champion* ya ulipaji kodi. Kuta zile zimeshabomoka zote, mapaa yameshabomoka yote. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba pale pahala pamo ndani ya damu yangu, mimi binafsi yangu nilishiriki pale kufanyakazi ya ujenzi wa Viwanda Vidogo Vidogo, katika miaka ya 26 nyuma. Kwa hivyo, serikali ifanye juhudi ifufuwe ile hali ya Viwanda Vidogo Vidogo, ifufuwe Bwawani kusudi viendelee kusaidia uchumi wa taifa letu.

Niliwahi kumsikia Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango alisema bado katika hali ya ukusanyaji wa mapato, tuna nafasi kubwa zaidi ya kuzidisha kuliko tulipofikia, jambo lile limewatia moyo sana wananchi. Ninaamini ikiwa tutazidisha bidii katika ukusanyaji wa kodi na kutunza rasilimali ambazo zipo mikononi mwetu, basi uchumi utaendelea kukua zaidi na zaidi kuliko hapo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo tutakuja katika uchangiaji wa huduma ya maji kila mjumbe anaeinuka anayapigania nafasi ya maji. Kwakweli, naamini serikali inamipango mizuri ya kufufua visima na huo mpango wa msaada kutoka Serikali ya India ambao utawasili au umo katika *process* za kukubaliwa. Kwahiyo, naomba Waheshimiwa Wajumbe wenzangu tustahamili kidogo hatuna wasiwasi tunaamini wenzetu wa India mkopo ule ushathibitika tatizo la maji nchi yetu itakuwa historia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa jumla mchango wangu umeishia hapo hutuba hii ya mkabala naikubali kwa asilimia mia moja tuchangamke zaidi fursa za kuongeza mapato zipo, kutunza rasilimali zetu zipo, na uchumi kukuwa kwa asilimia zaidi kuliko hapa. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Abdalla Ali Kombo.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako nakushukuru sana kwanza napenda kuishukuru ripoti hii lakini hasa ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango *comrade* Khalid pamoja na Mwenyekiti wa Kamati hii na pia napenda kuikubali ripoti hii mia kwa mia bila ya kasoro lakini nna michango midogo tu, na pia natangaza kwamba hii ni kamati yangu lakini nna vitu vidogo vidogo tu lazima tuongezee ongezee mafungu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyeki, kwanza ningesisitiza kwenye ukulima uchumi wetu tukitaka tusitake tunaegemea sana kwenye ukulima. Naishukuru serikali kwa juhudi zake zote za kuhangaika na mambo ya *irrigation* lakini bado naiomba serikali na hasa kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, bado tukimbie zaidi tuhakikishe tunapata muekezaji wa ukulima wa *irrigation*. Kuongeza matreka 40, 80 msaada wake upo lakini mdogo sana, na ningependa serikali iweke juhudi kama juhudi zilizowekwa kwenye ununuzi wa meli.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tukipata ukulima wa *irrigation* hatutategemea labda mpunga peke yake kuna mazao mengi, kuna ya mboga mboga na mazao mengi ambayo uchumi wa wananchi wa taifa utaongezeka. Sasa kama kila wilaya ilitowa pesa tukanunua meli basi uwezekano wa kila wilaya na kila halmashauri kutoa pesa tukatafuta *irrigation* mie nadhani kwenye nchi hii upo. Wanasema "*there is nothing impossible the question is how*". *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, jengine ukiacha labda hicho, kuna mazao kama boribo Muyuni, boribo ambayo inakubalika katika masoko yote ya nje nayo inapesa nyingi za nje au za kigeni tukikusudia tunaweza tukawakamata mpaka hawa Ras-al-Khaimah wakiacha visima vya juu huku hata visima vya mabondeni wanaweza wakatusaidia. Mhe. Mwenyekiti, kwakweli Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango yeye ni mtaalamu wa kuomba kwasababu masuala yanayotusaidia. Kwahivyo, Ras-al-Khaimah akawaendea baada ya kuchimba visima 150 , wakatuchimbia visima mpaka kwenye mabonde ya mpunga almuradi tufanikiwe.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nakuja kwenye utalii kitu ambacho kinaonekana kwa hivi sasa natunakokwenda ni moja katika kitu ambacho kinatusaidia kwenye pesa za kigeni. Sasa ningeomba tu hasa kwenye usafiri. Mhe. Mwenyekiti, serikali haifanyi biashara lakini ina mbinu nyingi ya kufanya mpaka utalii wetu uwe makini hasa kupitia kamisheni ya utalii kama tutakuwa na usafiri ambao unakubalika na unaaminika na ni wa kisasa. Kwa mfano, tukiwa na usafiri tunaweza kuchukua watalii Tanga, Dar-es-Salaam, Mombasa, Mtwara, Pemba na ikawa tunaigiza pesa kwenye nchi hii. Kwahivyo, naiomba serikali nayo ijitahidi tupate usafiri uwe wa utalii *special* kwa utalii inawezekana ikawa serikali kuu au ama kupitia manispaa zake, na manispaa kama ni mitaji ndio hii.

Mhe. Mwenyekiti, tena tunazungumzia Zanzibar. Zanzibar tunaiita *Spice Island*, lakini hizo *spice* hazipo ukilinganisha na ukubwa wa jina lake. Kutokana na hali hiyo, naiomba serikali basi ikatafuta maeneo, ndivyo wanavyofanya wenzetu duniani, kwa bahati nzuri sikai Makunduchi na Mwanakwerekwe tu nimetembea kidogo, wenzetu wanatafuta maeneo kama ni *spice* wanatafuta maeneo kama eka 20 au 40 wanapanda *spices* tofauti, zikeshakuwa tayari wageni wakija moja kwa moja wanafikia kwenye mashamba na serikali inakusanya pesa zake, aidha kupitia serikali yenyewe kuu au halmashauri ama taasisi yoyote lakini pesa zinakuwa zinapatikana.

Kwa hiyo, naiomba serikali katika mipango yake na imeanzisha Jozani tayari ni mpango mzuri tu serikali kuu inapata, wananchi wanapata. Kwa kweli, nadhani tumeshaanza isipokuwa tuzidisheni juhudi.

Mhe. Mwenyekiti, kitu chengine ambacho nimekiona ni makumbusho. Katika kutembea kwetu kuna nchi zinapata pesa nyingi ni makumbusho ukitizama wala sio makubwa si vitu vikubwa maana yake vitu ambayo sisi vipo. Kwa mfano, aina za watu wenyewe, ukitizama miaka 150 iliyopita watu wenyewe wa kijiji wa eneo fulani walikuwaje, hata hiyo lugha wanayo, mpaka hivi sasa hivi wengine hatuna, sasa vitu kama hivyo, kuna aina za vyakula, usafiri wao nguo zao michezo yao, kilimo chao, aina za wanyama, ndege, aina za nyumba. Sasa, tulimo kwenda kwa wenzetu vitu kama hivi vyote wamevikusanya pamoja na Wizara au Idara za Utalii zinakusanya pesa kama mchezo. Kwa hiyo, na sisi katika maeneo yetu yote ya Unguja na Pemba vitu kama hivi vipo ni juhudi tu za watu wa utalii.

Mhe. Mwenyekiti, kuna utaliii ambao unatokana na mazingira yenyewe. Kwa mfano, ukienda maeneo *Sweeden* juu, ambao kuna baridi ya kuua mtu kuna kitu inaitwa *Ice Hotel* msimu ukifika wanajenga hoteli za barafu kuna wale wanaofanya *snowing* mazingira yao ndio wanaofanya hivyo, na sisi tunamazigira yetu, ambayo tunaweza tukafanya. Brazil wamewekeza kwenye kanda kanda na sisi tunavyo vitu vingi, ambavyo vya kuwekeza tukapata pesa za kigeni, na wananchi wakapata pesa kwenye mambo ya utalii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuna kwenye zao la karafuu. Karafuu ni zao letu ambao tunalitegemea miaka mingi. Namuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, ili tupate fedha zaidi basi kuwe na usimamizi mzuri wa zao hili kwenye maeneo yote kuanzia kwenye mashamba, kuyajua mashamba, tunacho nunua, tunachouza, basi ombi langu kitu kama hichi kiwepo kitatusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, naona serikali bado iongeze juhudi kwenye uvuvi tunazungumza tu Mhe. Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi akija yeye huzungumza vifaranga vya samaki, lakini bado Mhe. Waziri sitaki azungumzie vifaranga nataka azungumzie makoo ya samaki, na hasa kwenye *deep sea* bado serikali haijaweka mkazo. Kwakweli, katika kuonesha kwamba serikali haijaweka mkazo kuna mambo ya *deep sea* Baraza la Wawakilishi linatakiwa kuridhia, ili kuwe na mambo ya ende mpaka sasa bado Baraza halijaridhia hapa unatizama *seriousness* ya sisi wenyewe yakoje na mambo ya *deep sea*. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naiomba serikali sasa hivi mnavyotuona tumekaa na samaki huko juu hasa kwenye bahari wamekaa hivivi, wana mratibu wana mnadhimu nasikia huko kuna wavuvi. Hivyo, naiomba serikali nayo, namimi mwenyewe binafsi nigeambiwa

natoa mashauri ningeunda Wizara ya Bahari na nikafuta baadhi ya wizara ambazo tija yake ipo lakini sio kubwa sana. Kwa hiyo, naiomba serikali iweke mkazo katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa naiomba serikali na pia natoa maoni kama Mwakilishi kama Abdalla Ali Kombo, ili mambo ya uchumi yaende lazima tuwe *serious*, hapa kila mtu anasifu China ukienda, lakini China imefikia pahala pale kwa sababu ya *discipline*, China ina *discipline* kila kona, kila *sector*, sasa kufeli kwetu sisi ni kwamba hatuna *discipline* na hasa kwenye matumizi.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa uzoefu wangu wa miaka hii mambo mengi yametuharibikia kutokana na kutokuwa na *discipline,* na hasa kwenye matumizi. Kwahivyo, naomba kungekuwa na taasisi rasmi ya kusimamia uchumi ikiwa ni kazi moja, kusimamia uchumi na nidhamu ya matumizi iwepo katika nchi, najuwa kuwa kuna Kamati ya Maadili, kuna Kamisheni ya Maadili, lakini bado watu wanapenya. Kutokana na hali hiyo, naomba kuwe na taasisi ya usimamizi wa matumizi na nidhamu ya matumizi. Vilevile, kuwe na kikosi cha kuwatia adabu waharibifu wa pesa hizi za serikali, iwe *special* kwasababu kama Kamati ya Maadili, wanasheria, hizi zote zipo lakini nchi haiendi, uchumi namna hiyo hautakwenda kama hatutokuwa *serious.*

Kwa hivyo, naiomba serikali hichi kitengo hakipo hichi lakini kifanywe kiwepo, wenzetu Bara hivi sasa wana Mahkama ya Mafisadi, maana sio kwamba tunazunguzia labda nchi nyengine tofauti ni wenzetu Bara na hapa iwepo, mimi bahati mbaya ni Mwakilishi lakini kama kupeleka *qualification* ningeomba na mimi.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia mifano tunayozungumza yote waharibifu, kuna uwanja wa ndege, kuna meli *fake*, kuna shida kwenye ardhi, haya yote kama hayakusimamiwa tusidanganye hatuna uchumi, hatuna uchumi Mhe. Mwenyekiti. Kwa mfano, ukienda kwenye ardhi kivumbi,ukija uwanja wa ndege kanyakanya, kwenye meli hatari. Sasa serikali naiomba kuwe na usimamizi na *discipline* ya matumizi ya rasilimali za serikali. Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru sana Mhe. Abdalla Ali Kombo kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe, kuna wachangiaji watano waliobakia nao watachangia jioni. Mchangiaji wetu wa mwanzo atakuwa Mhe. Hidaya Ali Makame, atafuatiwa na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, na Mhe. Miraji Khamis Kwaza.

Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuakhirisha kwanza niwashukuru na kuwapongeza, lakini pia ilitokea simtofahamu kipindi cha asubuhi wakati wa majadiliano yetu yanavyoendelea kuhusiana na hoja za Mhe. Mohammed Said Mohammed, ambazo zilijadiliwa na Baraza katika mkutano wa Disemba 2017 na Baraza likapitisha maazimio. Kwahivyo, kilichofanywa na serikali ni kuja kuleta majibu ya namna walivyotekeleza maazimio hayo. Hivyo, isingekuwa busara mjadala ule ukapelekwa tena kwenye kamati katika hatua hii, jambo hilo lisijadaliwe tena, kwasababu tayari serikali imeleta majibu ya hoja za Mhe. Mohammed Said Mohammed, ambazo zilishajadiliwa. Nawashukuru sana. Kwahivyo naakhirisha kikao hichi mpaka saa 11:00 za jioni.

(Saa 6:55 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea. Sasa naomba nimwite Mhe. Hidaya Ali Makame atafuatiwa na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu na Mhe. Miraji Khamis Mussa ajiandae.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuweza kuchangia machache juu ya hotuba hii ya Mkabala wa Uchumi na Mpango wa Maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nichukue fursa hii kwa kumpongeza sana Mhe.Waziri ambae ametuwasilishia hotuba hii leo asubuhi, na kwa kweli hotuba hii iko vizuri na niwapongeze sana pia Wajumbe kamati kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Fedha kwa kuweza kupita yale maeneo ambayo yanahusika na mengi ambayo wameyaona na wakayaorodhesha humu na sisi tukapata uwezo wa kuweza kuyachangia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa sina mengi ila tu ningependa sana niongee machache juu ya hotuba hii kuhusu muelekeo mzima wa vipaumbele vya kitaifa kwa mwaka 2018/19.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri tena, kwa kazi hii kubwa ambayo kaifanya akishirikiana na watendaji wake wote akaweza kuyaorodhesha haya, Mhe. Mwenyekiti kuna vipaumbele si chini ya tisa hapa vilivyowekwa, lakini katika vipaumbele hivi vyote ni vipaumbele ambavyo ndani ya nchi yetu hii kama vitafanyiwa kazi na kama vitazingatiwa basi kwa kweli niseme tu kwamba kero ya vijana wetu wa Zanzibar kuhusu suala la ajira na mengineyo basi linaweza likapungua kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika kipaumbele cha nane hapa kwa tisa yaani kiufupi hivi vipaumbele vyote vinaendana malengo yake ni mamoja ni kujenga na kuimarisha nchi yetu, lakini hususan kuwapatia vijana wetu ajira kwa asilimia mia moja, kuna kipaumbele kinasema; "kuimarisha ajira kwa vijana kwa kuwezesha pamoja na kuwapatia taaluma na ujuzi stahiki".

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba vijana wetu wengi wao sasa hivi wameona umuhimu wa ajira lakini wameona umuhimu wa ile elimu yao ambayo wanaifanyia kazi muda wa miaka si chini ya ishirini au ishirini na tano na kuendelea. Mhe. Mwenyekiti, ni wachache ambao hawapendi maendeleo na hawapendi kujituma, lakini kwa sasa hivi vijana wetu wengi wanaonekana kuwa na hamasa lakini kuwa na umuhimu wa kufanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niwapongeze vijana wenzangu wote ndani ya nchi hii kwa kuwa tu wanapenda elimu, na sababu ya kusema kwamba vijana wanapenda elimu mimi mjumbe wa kamati ya Ustawi wa Jamii ambae tumefanya ziara ndani maskuli yote mfano ya Unguja na Pemba, lakini hakuna skuli ambayo tunakwenda tukaambiwa hapa vijana hawataki kusoma. Kwa kweli vijana wanataka kusoma

wanaohitaji kusoma wanasoma lakini changamoto zipo na wanakabiliana nazo kwa sababu tumeona mambo mengi tu, tumeona maskuli ambayo yanavuja, hayafahamiki kiukweli lakini vijana wale hawavunjiki moyo bado wanashirikiana na walimu wao wanaendeleza masomo.

Lakini vijana hawa hawa wanapofika *stage* za juu kufika vyuo na kwenda kuchukua stashahada tofauti vijana hawa wanaonekana kuvunjika moyo kiupande mmoja kutokana na suala la ajira, kwa sababu kijana anajiuliza hivi mimi nasoma nikisha maliza kweli najikita kwenye ajira za aina gani. Mtu pengine anakwenda kusomea kitu lakini unakuta ile ajira inakuwa ni mtihani kwa upande wake, kwa hiyo tu mimi hapa kutokana na vipaumbele hivi ambavyo vimeorodheshwa hapa ningeshauri sana serikali yangu Mhe. Mwenyekiti, pamoja na Mhe. Waziri akawaangalia vijana kwa nyanja tofauti. Kwa sababu hapa pia kwenye vipaumbele kuna kipaumbele kinachosema kuimarisha kilimo kwa kujenga miundombinu lakini pia kuna kipaumbele kinasema kuimarisha ubora wa huduma za kijamii, lakini pia kuna utawala bora na uimarishwaji wa taasisi na uwekezaji, lakini mpaka suala la uimarishaji wa viwanda vidogo vidogo pia limeonekana kama ni kipaumbele.

Mhe. Mwenyekiti, tukiviangalia vipaumbele hivi vyote vinawahusu vijana lakini na wafanyakazi wote. Kwenye kuimarisha viwanda vidogo vidogo lakini pia kuimarisha kilimo hapa sana inaonekana walengwa hasa ni vijana kwa sababu hizi kazi zote ni za vijana. Lakini vijana hawa hawa endapo kuwa wapo kule maskulini wamo ndani vyuo ukaanza kuwapa zile taaluma mapema wakaweza kujiajiri wenyewe wakaweza kuwa na ile miundo mbinu tofauti ya kuweza kufanikisha masomo yao au na ajira zao wakaweza kupata taaluma mbali mbali, vijana hawa endapo watatoka kule maskulini au kule vyuoni hutowakuta wakalalamika kwa sababu wengi wao watakuwa tayari weshakuwa na ule muelekeo mmoja wapo weshakuwa na njia mbadala au njia tofauti za kuweza kuwasaidia wao katika kujiajiri wenyewe siyo kusubiri ajira za serikali au ajira za taasisi au ajira za watu wengine.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli vijana wanahitaji kuimarishwa na wanahitaji kuangaliwa kwa asilimia mia moja katika suala la ajira na kujiendeleza kimaisha. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa ningemuomba sana Mhe. Waziri lakini na serikali kwa ujumla wakishirikiana na Mawaziri wote, katika vyuo ambavyo vinatolewa taaluma mbali mbali basi kuna mambo muhimu yangezingatiwa na katika hayo mambo muhimu ambayo yangezingatiwa, basi vijana hawa wangepatiwa taaluma ya kuwabadilisha mitazamo yao ili tu kijana atakapotoka pale basi asiende kubweteka kule mitaani na akasema mimi nasubiri ajira ya serikali au sehemu nyingine bila yeye mwenyewe kuweza kujiendeleza na kujiajiri mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, atakapotoka kule kijana akishakuwa na taaluma yake basi anaweza akafanya vitu tofauti, kwa sababu tunajua vijana wetu wa Zanzibar wengi ni wajasiriamali pia ni wabunifu kuna vijana wana vipaji mbali mbali. Kwa hivyo, vile vipaji vyao vikiendelezwa tangu kule vyuoni au tangu maskulini kutakuwa na njia rahisi kwa upande wao kuweza kuwasaidia.

Mhe. Mwenyekiti, pia taaluma ya ujasiri amali vyuoni iwepo ili vijana hawa wazidi kujiona kwamba wao kweli wanaweza kujiajiri wenyewe, ujasiriamali ni kitu muhimu

sana kwa kila binaadamu, siyo kama siku zote wewe utapata kazi ya kuajiriwa, lakini mwenyewe unapoweza kufanya mambo yako yakakusaidia ukawezeshwa na zile nyenzo ukawa unazo, kwa sababu hapa kitu kinaangaliwa ni nyenzo bila ya kuwa na nyenzo hata uwe mjasiriamali wa aina gani basi utashindwa na hatimae ndio utakaa mitaani ubweteke halafu baadae uilaumu serikali yako.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuimarishwa mfumo wa ufundi ndani ya vyuo, ufundi kuna wa aina mbali mbali kila kijana ana ujuzi wa aina yake, kwa hivyo kama mwalimu basi ana fursa ya peke yake ya kumtizama huyu mwanafunzi wangu labda ana kipaji cha aina gani, ili waweze kuwawezesha baadae vijana wale watakapotoka kule hapa kinachosisitizwa zaidi ni wale vijana kukaa mitaani wakawa hawana kazi na wakaanza kuzurura.

Kwa sababu tunaona kwamba hawa vijana ambao wanafika kule mitaani wakishakuwa hawana kazi lakini huku wametoka wanajiona tayari wao weshakuwa na elimu, basi ndio wanaofika mitaani wakaanza kuwaburuza wale wenzao ambao hawana elimu na kuweza kuwavunja moyo na vijana wale wadogo ukawakuta wanakwambia mimi siendi skuli niende skuli nikafanye nini. Wenzangu kaka zangu wapo wamesoma wamefika wapi na hawana kazi. Kwa hiyo hapa tunaona kwamba vijana wakati mwingine na wao wanaweza kuwaburuza wenzao kutokana na kwamba wameshasoma wamekaa mitaani hawana kazi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nisingependa nizungumze mengi juu ya suala hili, lakini hapa pia ningemuomba sana Mhe. Waziri akawaangalia vijana kwa kila hali, kuna suala la kiutalii hapa limezungumzwa masuala ya utalii linalohusu pia hao hao vijana. Utalii chuo kipo na kinasomesha utalii wa aina tofauti na katika vyuo vilivyopo hapa ndani ya Zanzibar yetu hii mimi nafikiri chuo cha Maruhubi ni chuo ambacho kinatoa vijana bora na chuo ambacho kinatoa vijana wajasiri na waliobobea wakitoka pale ambao tayari wameshasoma hata mafunzo ya miezi mitatu basi vijana wanatoka pale wakiwa wako vyengine.

Kwa hivyo, vijana hao hao wanapotoka pale wanakuwa uwezo tayari wameshakuwa nao siyo kama yule ambae yuko mitaani hafanyi kazi yoyote na yupo tu katulia, ni tofauti na vijana hawa wakuwa na uwezo wa kuweza kujiajiri wenyewe kwa hiyo ningemuomba sana Mhe. Waziri ikazingatiwa suala la ajira kwa vijana, lakini na hivi vipaumbele vilivyopo hapa ambavyo vimeorodheshwa vikaweza kupewa kipaumbele zaidi kama vilivyoandikwa hapa kwamba ni kipaumbele vikazidi kupewa kipaumbele ili hii miundo mbinu , huu uimaishwaji wa mambo ya utalii na mambo ya viwanda vidogo vidogo kila kitu kikaweza kukaa sawa. Kwa sababu bajeti inapangwa inatungwa lakini pia hiyo bajeti hata ikiwepo kama kutakuwa hakuna wasimamizi au hakuna washughulikiaji wa hili tunaweza kila siku tukaja hapa tukaweka vipaumbele, kwa sababu kama tutaangalia ndani ya kitabu hiki kina vipaumbele tisa lakini kitabu cha mwaka jana kilikuwa kina vipaumbele vitano tu ambavyo vipaumbele hivyo hivyo mpaka leo kuna vingine bado havijaweza kutekelezeka.

Mhe. Mwenyekiti, bila mipango imara hakuna kitakachowezekana hata kimoja na hakuna kitakachofanikiwa, mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri akazidi kusimamia watendaji wake na kuzingatia juu ya maslahi ya vijana na kuitendea haki bajeti ambayo inapangwa kwa ajili ya kuendeleza shughuli za kijamii na shughuli za kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: nakushukuru Mhe. Hidaya kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe. Hussein Ibrahim atafuatiwa na Mhe. Miraji na Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Ajiandae.

Mhe. Hussein Ibrahim: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa jioni hii kufika hapa salama sote katika Baraza lako tukufu, na nikushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi hii kuchangia bajeti yetu muhimu sana hotuba ya Makadiro ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo ya mueleko wa bajeti kwa mwaka 2018/19.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianzie haraka haraka katika bajeti hii muhimu sana, muelekeo ni roho yetu ya nchi yetu na kwa Zanzibar kwa ujumla wake. Kwanza mimi nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kazi yake nzuri anayoifanya na hasa nimesema mwanzo ni roho ya nchi yetu kwa sababu yeye ndio mwenye mambo yote, haya mambo yote hayawezi kufanyika bila ya yeye. Bajeti hii, mambo ya maendeleo, mambo yote tunayopata katika nchi yetu yeye ndio namba moja nampa nafasi yake. Kwa hiyo, mimi nimpongeze kwa kazi yake nzuri na juhudi yake nzuri sana kubwa pamoja na watendaji wake wote kwa kukusanya kodi ambazo zinaweza kutusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa huu wa ishirini na moja kifungu namba 53 hapa Mhe. Waziri katuandikia pia asilimia 5 ya makusanyo inabaki *ZRB* inatarajiwa kuwa ni bilioni 20 hili nimpongeze sana Mhe. waziri kwa sababu hii asilimia 5 anaibakisha nafikiri kwa ufahamu wangu kidogo hiyo ni katika kuwapa motisha wafanyakazi wake wanaokusanya kodi, hili jambo zuri kwa sababu tukiangalia huu mfumo mzima wa kukusanya kodi hapa pana vishawishi vingi kama hawa wafanyakazi wetu wa ZRB hawajakuwa makini hawajakuwa na moyo na uzalendo kwa kweli inakuwa hata hizo kodi hatuwezi kukusanya watakuwa wao kama ni mwanzo wa kupokea rushwa, lakini Mhe. Waziri akiwapa motisha na akikaa nao vizuri watafanya kazi vizuri.

Mimi niwapongeze sana watendaji wa *ZRB* wanafanya kazi vizuri kweli mwisho jana mimi nilikuwepo ile huduma yao imekuwa *fantastic* sasa hivi kama tuko ulaya mambo yao yote yako kwenye mitandao. Kwa kweli mimi nimpongeze sana Mhe. Waziri tumepiga hatua kweli kweli maana yake mambo mengi nimeyaona pale ya kileo yanafanyika bila muda kuchelewa wananchi wanafaidika na wanafurahia sana huduma zetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niendelee katika ukurasa huu wa nne wa kitabu cha Mhe. Waziri katika kifungu namba 9 katika kuingia kwa watalii katika nchi yetu. Kwanza mimi niipongeze serikali kwa ujumla, wote serikali kwa kazi yenu nzuri hasa watendaji wakuu wa serikali kwa kuimarisha sekta ya utalii kwa sababu hii ilikuwa ni wimbo wa taifa wetu, miaka yote ya nyuma tulikuwa tunataka watalii waje hapa ili waje kutembelea mji wetu tupate pato kubwa katika sekta ya utalii na sasa hivi tunaona matunda yake, wageni wengi wanakuja na serikali yetu inajitahidi sana kuwakaribisha vizuri na kuwapa nafasi nzuri katika historia zetu kwa kweli wageni wanafurahi wakija mpaka wakiondoka kwa kweli wanaridhika walichokijia Zanzibar kutizama wanafurahi sana.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kitabu cha Mhe. Waziri kifungu namba 9 kimesema hapa kutoka Januari na Juni 2017 uingizaji wa wageni karibu watalii 143,000 wameingia kutoka nchi mbali mbali na ukiangalia kwa januari mpaka juni ukipiga mara mbili tuna wageni karibu laki tatu na wataingia Zanzibar. Kwa hivyo, mimi nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kazi yake nzuri kwa sababu hii ni sekta muhimu sana Mhe. Waziri kaweka hapa kwa sababu tunakusanya kodi katika sekta hii, kama hawa wageni watakuwa hawaji hata haya malengo ya Mhe. Waziri yatakosekana.

Kwa hivyo, tuwe sote katika nchi yetu ya Zanzibar dhana ya kujenga utalii, utalii ni kwanza wageni waje ili watumie tupate. Ukiangalia hawa wageni watakapokuja Zanzibar watakaa kwenye hoteli zetu watatumia katika hoteli, watakula vijana wetu watapata ajira utakuta mambo ya magari haya *transport private hire* watapata wote ajira. Kwa hivyo, mimi namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kazi yake nzuri sana kuweka hapa katika kipaumbele chako na mambo mengine. Lakini ukitizama pia kiasi ambacho kuongezeka kwa jumla ya Tshs 92 bilioni katika mwaka 2016 lakini 2017 kufikia jumla karibu Tshs 123.8 bilioni Mhe. Waziri mimi nikupongeze sana kwa malengo yako haya na kwa kufahamu huu umuhimu wa utalii ili wageni waje.

Mhe. Mwenyekiti, nije hapa katika ukurasa huo huo wa nne kitabu cha waziri uwekezaji wa kupitia *ZIPA*, ukiangalia miradi iliyowekezwa hapa vitega uchumi kupitia sekta mbali mbali hii imeongezeka karibu dola za kimarekani Milioni mia moja na themanini na sita idadi ya ajira imeongezeka. Kwa hiyo mimi niipongeze sana sekta hii *ZIPA* kwa kujitahidi sana ukiacha mbali ya changamoto. Kuna changamoto moja katika ripoti ya kamati ilikuja hapa, sekta hii ya *ZIPA* kuna muwekezaji mmoja mkubwa lakini mpaka leo kidogo mambo yake hayajenda uwekezaji huu haujakaa vizuri. Ule mradi mkubwa sana ulikuwa ufanyike hapa kwa nia njema ya serikali na kwa kupitia kwa Rais wetu wa Zanzibar Dr. Ali Mohammed Shein kwa kujitahidi sana kukuza hii sekta ya utalii na hawa wawekezaji wanakuja kwa sababu nchi yetu ina amani na utulivu, na ukitizama sekta hii hapa kuna mradi huu mmoja mkubwa mpaka leo haujafanyika.

Mhe. Waziri nilikuwa naomba mradi huu kwa nini kwa sababu mimi nasikitika huu mradi mkubwa karibu dola bilioni mbili unatumika na haujafanyika mpaka leo unakuta wawekezaji wanachukua fidia kubwa kwa mazao. Hata kwenye ripoti ya kamati mnazi mmoja wanataka milioni nne kitu cha kusikitisha sana. Na malengo yako Mhe. waziri mimi nayajua naona kukusanya kodi kupitia hawa wawekezaji wakija wakiwekeza tutapata ajira sisi lakini pia ukitizama idadi mpya imeongezeka kwa asilimia nane sawa na *point* nane tizama kufikia watu karibu 1245 kipindi hicho cha mwaka. Kwa hiyo Mhe. mimi nikupongeze sana kwa hii ajira mpya ambayo itaongezeka Zanzibar kwa ajili ya miradi hii ya kupitia *ZIPA*.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana msanii mmoja kutoka Dar-es-Salaam, mkubwa sana wa kimataifa Daimond Plutnum yupo hapa Zanzibar kutafuta vipaji vya watangazaji wetu kafanya leo *audition* ya kutafuta mtu mwenye kipaji kupitia Zanzibar na nimshukuru sana Waziri wa Habari, kitendo alichofanya jana pale Baraza la Wawakilishi la zamani kumpa msanii yule leseni ya TV na Redio kitu ambacho nimefarajika sana sana. Kwa sababu hizi leseni zinakuwa zina usumbufu mkubwa kuzipata kuna mambo mengi lakini Mhe. Waziri kajitahidi sana kaona muwekezaji huyu kaja na nia njema kutoka Bara kaja hapa na huyu msanii ni mkubwa, Msanii

huyu yuko hapa leo anafanya *audition* pale Ngome Kongwe dunia nzima inajua kwa sababu Diamond yuko Zanzibar kuna jambo fulani linafanyika. Hili mimi naomba sana Serikali kupitia Waziri wetu tuwe makini sana kwa watu kama hawa kwa sababu hawa ni kivutio pia kwa wageni na watalii kuja kuona mambo kama hayo.

Hii redio ikiweza kufunguliwa, kama alivyosema mwenyewe anatafuta Wazanzibari wakafanye kazi, mimi nampongeza sana msanii huyu kwa nia yake njema kwa sababu zipo nyingi sana katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akienda Arusha, Mwanza, Dodoma lakini kaamua kuja Zanzibar kwa nini.

Kwa hivyo mimi naomba sana tumpe imani nzuri kama ulivyompa Mhe. Waziri jana tumuengezee kuja kuangalia studio zetu kenda *ZBC* kuangalia, kwa hivyo tushirikiane nae huyu msanii ukiacha mbali msanii lakini ana mvuto mkubwa wa vijana na watu mbali mbali kumuangalia, kwa hivyo mimi nakupongeza Mhe. Waziri kwa juhudi zako hizo na kuongeza ajira pia katika nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nije ukurasa wa kumi na tisa, hapa katika kifungu namba (h) Kuimarisha ajira kwa vijana kwa kuwawezesha pamoja na kuwapatia taaluma. Hili jambo zuri sana na umeliona kwamba vijana wetu wengi hawana ajira na kweli ukitizama sekta hii ya ajira Serikali haiwezi kuajiri vijana wote na vijana ndio nguvu kazi, vijana ndio taifa la kesho. Sasa tukiwaona tukiwapa vipaumbele vijana wetu kuwapatia taaluma na ujuzi jambo zuri sana kwa serikali yetu na mimi naipongeza waendelee kufanya hayo.

Lakini tukiangalia pia katika matarajio ukuaji wa uchumi wetu unaonyesha hapa katika kitabu cha Waziri wetu kwa kweli matarajio yanaonyesha mazuri karibu asilimia sabiini na moja 2018, jambo zuri na la kupigiwa mfano sana kwa mwelekeo mzuri tunaokwenda huko mbele.

Vile vile, ukurasa wa 19 nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuongezeka kiwango cha idadi ya watalii wanaoingia nchini kutokana na kupatikana kwa masoko mapya, hili jambo ni zuri sana kwa sababu kila wawekezaji wakija Mheshimiwa masoko yanaongezeka ajira zitaongezeka. Kwa hivyo hili jambo zuri sana kila watalii wakija mimi nashukuru na tupate pato kwa taifa. Lakini Mhe. Waziri umetuwekea hapa vipaumbele katika mwaka 2018/19 hili jambo zuri sana na mwelekeo wako ni mzuri wa kuimarisha kwa mfumo huu kujua tunakwenda wapi katika 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kuimarisha hapa umetwambia kuimarisha miundombinu ya maeneo ya uingiaji nchini barabara na nishati ni jambo zuri sana, ukiangalia hawa wawekezaji wanapokuja wakiona barabara zetu haziko vizuri wanaweza hata kukata tamaa wakaamua kuahirisha uwekezaji wao. Kwa hivyo, naomba sana hiki kipaumbele chako ulichokiweka basi kiwe kipaumbele cha kweli kweli. Ukitizama kama Kaskazini kwetu kuna mahoteli mengi huku Nungwi lakini kuna sehemu za kuingia ndani njia ndogo tu lakini mbovu na ukiangalia Mhe. Waziri hawa wanalipa kodi kubwa wawekezaji, kwa hivyo tuwatengenezee sisi miundombinu ya njia ili waweze kufanya kazi zao vizuri. Pia tuangalie suala la umeme tuwawekee umeme imakuwa kidogo tatizo kwa sehemu za shamba kwa hivyo tuwavutie ndugu zetu wa *ZECO* wafanye kazi kwa haraka kupeleka umeme maeneo hayo, kwa sababu wawekezaji watakuwa na moyo zaidi kuwekeza katika nchi yetu.

Lakini jambo jengine hili suala la mafuta linasikitisha sana sana hawa wanakuja wazungu na pesa zao wanataka kuwekeza Zanzibar lakini unakuta hii wiki moja nzima mafuta yalikuwa hamna Zanzibar. Kwa nini inakuwa mafuta hamna kwa sababu jambo la mafuta ni muhimu kwa kila mwananchi anayeishi hapa ukikosa mafuta siku moja kwa kweli mambo mengi yanaharibika. Sasa mimi naomba sana Mhe. Mwenyekiti tujipange mapema na *stock* yetu ya mafuta hichi ni kisiwa kitakapokosa mafuta inakuwa hatari sana. Sasa mimi naomba tujipange mafuta isiwe kila baada ya mwezi mafuta shida hapa Zanzibar jambo la aibu sasa hivi tunapiga hatua za mwelekeo wa 2018/2019 ni mambo mazuri kabisa, naomba suala la mafuta tujipange zaidi huyu muwekezaji aliyewekeza yale mafuta basi aangaliwe kwa undani kabisa afanye kazi zake kwa umakini.

Kwa kweli, amesema nafasi ya mwanzo ameimarisha sana sekta ya utalii na hii ni uti wa mgongo wa nchi yetu asilimia sabiini au thamanini ya kodi tunaipata kwenye sekta hii ya utalii, kwa hivyo nakupongeza sana Mhe. Waziri kwa kazi yako nzuri, lakini pia kuimarisha viwanda vidogo vidogo kwa kuongeza thamani ya bidhaa ubora na vifunganishio. Lakini nasema hivi viwanda kuna changamoto moja ukiangalia kama haya maji yetu haya ya *Drop of Zanzibar* na *Zanzibar Kool* mimi naangalia sana kule Dar-es-Salaam kwenda Tanzania Bara siyaoni maji haya kwa nini.

Sasa huyu muwekezaji akianzisha kiwanda hapa hutegemea soko la Zanzibar tu, hichi kiwanda kitamshinda Mheshimiwa lazima sisi tuangalie kwa nini haya maji yetu yasiende Bara yakauzwa kule mikoani kote. Kwa sababu kama mimi natoka Zanzibar nakwenda Mikoani nitanunua maji yetu kutoka Zanzibar natumia uzalendo wangu nitatafuta maji yangu ya *Kool* maji yangu ya *Drop* lakini leo maji yale huyakuti kwa nini. Mheshimiwa naomba hilo hebu nipe ufafanuzi kidogo nijue kwa nini inakuwa changamoto hayo maji yetu hawa hawa wafanyabiashara wanashindwe kupeleka bidhaa zao Tanzania Bara.

Mhe. Mwenyekiti, pia kipaumbele chengine umeweka ni kuimarisha ubora wa huduma za kijamii zikiwemo elimu, afya, michezo upatikanaji wa maji safi na salama. Mimi niseme kitu kimoja haya mambo ni mazuri sana, lakini jambo la kusikitisha kidogo hapa Mheshimiwa haya maji safi na salama kila siku tunayazungumza Mheshimiwa, tangu mimi kuingia Baraza hili Mheshimiwa nimekuwa mjumbe wa kamati ya Mawasiliano na ujenzi na ardhi kwa pamoja katika kipindi kile ukiangalia kwenye ripoti ya changamoto ya ripoti ya kamati, tatizo kubwa la maji lipo ukiangalia Ras-al-Khaimah ndugu zetu wametusaidia kuchimba visima. Mimi nilikuwa mjumbe wa kamati kipindi kile, visima 150 tumechimbiwa lakini Mjini Magharibi visima 50 lakini mpaka leo visima vinne (4) ndio vinavyofanya kazi. Hili jambo sasa hivi tutafuteni hatua kwa sababu kama haya mambo ya maji hayapatikani vizuri itakuwa shida. Kwa hivyo mimi naomba sana hivi vipaumbele tuloviweka basi tujitahidi sana kutimiza azma yetu na Mheshimiwa Waziri uangalie kwa nini maji mpaka leo shida hili tatizo ni kubwa sana. Visima vinne tu katika visima hamsini Mkoa wa Mjini na Magharibi hiyo haiwezekani lazima kuna kitu na sabotaji inafanyika maji yasipatikane hapa Zanzibar.

Mheshimiwa lakini nipongeze sana katika kurasa wa 23 Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuamua kuweka elimu bila ya malipo hadi Sekondari hili jambo nimpongeze sana Waziri, nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar kwa juhudi zake kubwa kuamua kufanya hivyo….

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa samahani kidogo Waheshimiwa Wajumbe minon'gono imezidi sana kwa hivyo nawaomba sana tena sana sauti zinapanda anayechangia hasikilikani sauti zenu zimekuwa ziko juu, kwa hivyo nawaomba tuwe taratibu endelea Mheshimiwa.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, ni hili la ununuzi wetu wa madawa ukitizama sasa hivi hospitali Mnazi Mmoja hospitali ya rufaa utakuta unaandikiwa dawa, lakini dawa hamna utaambiwa ukanunue. Sasa mimi naomba sana tukisema Serikali itoe dawa bure kwa wananchi wote wanaokwenda pale itakuwa ni uongo itakuwa shida haiwezekani hatuwezo ku- *afford* hakuna kitu ghali kama dawa. Juzi Mhe. Waziri kasema serikali imetoa bilioni tatu kununua dawa juzi tu, sasa hizi dawa zinatumika baada ya miezi sita hamna dawa. Sasa mimi naomba sana kuna huu mfuko wa bima huu mimi naomba sana tutoe elimu kwa wananchi wetu au wananchi wawe na bima, bima wakiwa nayo itawasaidia ile bima kum-*cover* kuwa anaumwa na bima ukiangalia sasa hivi bima yetu hii tunayotumia sasa hivi elfu kumi tu kwa mwezi kwa hesabu inayokuja haraka haraka.

Sasa mimi naomba tuwape elimu wananchi wetu kwa sababu pale huduma serikali inajitahidi sana kununua dawa lakini itakuwa haiwezi itafika pahali itashindwa, sasa mimi naomba sana Serikali kupitia Wizara ya Afya itoe elimu kwa wananchi wakate bila za afya ili wanapokwenda kutibiwa watibiwe bure lakini bima i-*cover* pale isiwe bure bure serikali yetu itakuwa haiwezi ingawa kipaumbele waziri katuwekea lakini jambo hili tuiangalie sana pia na serikali.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa tano uchambuzi na matokeo ya hali ya rasilimaliwatu katika utumishi na ajira, ukiangalia katika ripoti ya Mhe. Waziri ripoti yake nzuri lakini ukisema kundi lenye umri wa miaka 20 mpaka 24 ndio kundi kubwa ambalo lilokuwa halina ajira, ukitizama hapa katika ripoti wamesema katika miaka 15 mpaka 35 wasiokuwa na ajira imefikia karibu asilimi ishirini na moja. Mhe. Mwenyekiti, hili tuangalie sana kwa sababu ukitizama vijana ndio taifa nilivyosema mwanzo lakini kama watakuwa hawana ajira na ukitizama Mkoa wa Mjini Magharibi ndio una watu wengi kwa Zanzibar ukisema asilimia arobaini na sita ya Zanzibar watu karibu laki tano tisini na tatu Mheshimiwa.

Lakini mimi pia nimpongeze sana Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi kwa kazi yake nzuri sana anayoifanya, ukitizama hata kwenye ripoti ya Kamati Mheshimiwa imekuja hapa ripoti ya Mkoa wetu huu wa Mjini Magharibi, ukiangalia pia ushirikiano mzuri wa raia katika shughuli za kijamii mafanikio katika Mkoa wa Mjini. Lakini pia ukitazama mafanikio, kudhibiti, usalama wa raia na mali zao katika Mkoa wa Mjini, hili jambo zuri lakini ukizama pia tatizo kubwa la ajira bado lipo Mkoa wa Mjini Magharib ni tatizo kubwa sana na ajira kama itakuwa hamna kwa vijana hawa ndio itapelekea kwenda kwenye madawa ya kulevya. Kwa sababu ukitizama sasa hivi Mkoa wa Mjini imepungua Mhe. Mkuu wa Mkoa kajitahidi sana kupunguza hili tatizo la wimbi wa madawa ya kulevya. Lakini hawa vijana wetu wakiwa hawana ajira ni changamoto kubwa na inampelekea mtu chanzo cha kuingia kwenye madawa ya kulevya. Kwa sababu mtu unapokuwa huna ajira huna pesa ufanye nini familia inakusubiri nyumbani, mtoto anakusubiri nyumbani anataka kwenda skuli, mtoto anaumwa, mke anaumwa wee huna cha kufanya unaanza kuingia kwenye madawa ya kulevya.

Sasa mimi naomba sana Mhe. Waziri kama ulivyosema mwanzo kipaumbele ajira kwa vijana hawa hawa wawekezaji tuwape kipaumbele zaidi waweze kuwekeza na hii kama nilivyosema changamoto *ZIPA* kuna miradi inazorota ya hawa wagani kuja kuwekeza kuna kitengo kile cha *One Stop Centre* mpaka leo hakijafanyika kwa nini Mheshimiwa hichi ndio kinapokea wageni kutoka nje wakija wakifika hapa *One Stop Centre* itawasaidia.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie tu mimi niunge mkono hii ripoti asilimia mia kwa mia na ripoti nzuri sana Mhe. Waziri wetu na niseme ahsante sana nashukuru.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hussein Ibarahim Makungu kwa mchango wako sasa naomba nimuite Mhe. Miraji Khamis Mussa, atafuatiwa na Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame na Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi ajiandae.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia hotuba iliyowasilishwa na Mhe. Waziri wa Fedha ya mpango wa maendeleo na mwelekeo wa bajeti kwa mwaka 2018/2019. Kwanza nachukua fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri na watendaji wote wa Serikali walioshiriki katika kutengeneza mpango huu wa maendeleo, ni mpango mzuri sana mwelekeo umetuonesha wazi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba niende moja kwa moja katika kuchangia mpango huu wa maendeleo kunako vipaumbele vya kitaifa kwa mwaka 2018/2019, (a) hapo kuna kuimarisha miundombinu ya maeneo ya uingiaji nchini barabara na nishati, mimi naomba niongelee suala la nishati. Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili tunawashukuru wenzetu wamepiga hatua nzuri katika kutafuta mwelekeo tulikuwa tunashauri mara nyingi sana kunako eneo hili basi katika sura ya kuliwezesha Shirika letu tuondoke hapa tulipo tuelekee katika mpango ambao unaweza ukawapunguzia wananchi wetu kasi ile ya kulipa umeme kwa gharama kubwa. Kwa hivyo tunaishauri Serikali mwelekeo ambao tutaridhika nao mzuri katika eneo hili basi Serikali yenyewe ianze na utaratibu wa kupitisha sera lakini pia kuanza na utaratibu wa kufanya *installation* ya *power generation* kwa ile *study* ambayo watakuwa wenzetu wameifanya wakatupeleka kwenye *waste* tu *energy* hatuna tatizo lakini wakitupeleka kwenye *solar* hatuna tatizo.

Lakini kitu kizuri ambacho tunataka kuwashauri wenzetu tukiwa tuna kianzio chetu wenyewe tutakuwa tuna uwezo basi wa ku-*control* hata zile bei ambazo kila muda zinakuwa zinapandishwa kwa sababu kianzio hasa cha umeme tunapokea kwa wenzetu kutoka Dar-es-Salaam, kila mara tunapata hapa leo imeongezeka bei hii utaratibu wa ku-*control* hili ni gumu. Serikali yetu tunaiomba sana iondoke katika utaratibu huo iende katika utaratibu wa kawaida ambao tuta-*install* wenyewe na tutakuwa tuna *power generation* yetu ambayo itaongozwa na Serikali yetu, itaindeshwa na Shirika letu la *ZECO* kuna uwezo pia wa kuongeza mwelekeo mzuri wa kiuchumi tukielekea huko.

Lakini eneo la pili la kuimarisha zaidi utalii nchini nilikuwa naangalia bajeti ambayo ilikuwemo katika *program* ile ya kuimarisha utalii na nilipoisoma katika kitabu cha bajeti tulichonacho ilikuwa ni shilingi milioni 425,293,000/= *program* hii tukisema tunauendeleza utalii si rahisi na hatuwezi kufika na ukisoma vizuri ripoti ile unakuta

karibu vipindi 72 mwaka uliopita ndio walienda navyo katika kutangaza utalii na majarida mbali mbali. Lakini lazima tukubali kuutangaza utalii hapa nchini kwetu hatuwezi kuongeza kasi ya ukuwaji wa sekta ya utalii nchini lazima tuutangaze nje ya nchi, hatuwezi kutangaza kwa pesa hii ambayo tumeiweka hapa na tulisema, lakini na mara hii wenzetu mkituletea milioni 425 tutakuwa tunawauliza mwelekeo huu wa kuusogeza utalii ni kweli tuko *serious* kwa hivyo kwa vyovyote bajeti ya kuutangaza utalii kama kweli Kitengo cha *Marketing* kinafanya kazi vizuri hatuwezi kwenda na milioni 425 kama mwaka wa fedha tuliotoka.

Sasa kwenye eneo hili nimuombe tu Mhe. Waziri wa Fedha watakapokuja kutengeneza bajeti tuangalie eneo muhimu ni eneo hili la utalii, tuliingizie fedha katika kuutangaza utalii katika nchi za kigeni kama Itali na nchi nyengine, sasa tukenda na utaratibu wa kawaida tu kuwa tunasema tunaimarisha utalii ni program na kipaumbele cha kitaifa lakini tunawatengea milioni 25 hatuwezi kufika na hatuwezi kuutangaza utalii, utalii hatuwezi kuutangaza hapa *ZBC* wala *TBC* tukaja tukasema tumeshatangaza utalii na vijarida tunaunda vipo mia mbili tunavipeleka nchini, utalii lazima program yake ya kutangaza kitengo cha *Marketing* kiondoke hapa kikatangaze utalii tuwe *serious* kunako eneo hili.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kuiweka katika mwelekeo na kipaumbele mimi naridhika nayo, lakini nitakujakuwa siridhiki maana yake tukaja tukaingiza milioni 400 hatutokuwa *serious* katika eneo hili. Eneo moja muhimu linatuingizia fedha tunaona mambo mengi ambayo tunafaidika katika sekta ya utalii kwa hivyo katika eneo hili basi mara hii bajeti yake ikue.

Lakini katika huu huu utalii tumejenga mahoteli mengi na yana madaraja tofauti lakini mikataba ukifuatilia kwa undani zaidi unakuta wote karibu *rate* zao zinalingana, sasa hebu tu-*review* mikataba yetu na tuunde madaraja. Zipo hoteli tuzipe daraja la kwanza, daraja pili na daraja la tatu ili hata zile *rate* watu waweze kutofautiana katika mwekeleo mzuri wa kukusanya mapato katika eneo hili, naamini tutakuza uchumi vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kipaumbele cha kuimarisha kilimo na kujenga miundombinu ya umwagiliaji bajeti na mwelekeo tuliotoka nao tulitenga karibu milioni 27 sasa ziko ahadi tulikwenda nazo kwa mradi mkubwa ule wa *irrigation* tutautekeleza katika mwaka ule wa fedha, lakini mimi nafuatilia sana hizi tenda za Serikali ili kutafuta wale ambao watakuja kufanya kazi kubwa kama hizi sijaona hilo tangazo. Kwa maana huo mradi ambao katika bajeti iliyopita ulikuwa na fedha kutoka *Exim Bank* na unakwenda moja kwa moja na wenzetu wa Wizara ya Kilimo, mara ya mwanzo ulikuja tukenda kwenye *re-tendering* lakini mara ya pili hatujasikia chochote. Mimi nalizungumza hili kunako suala la kilimo kipaumbele, tumeweka lakini lazima tuingize fedha katika uwekezaji katika eneo la kilimo. Tutakapozalisha vizuri, tutakapokuwa na mazao yetu nchini tunauza ndani basi hata ule uchumi wetu na kile tunachoingiza tutakuwa hatuwezi kuagziza tukatumia fedha za kigeni.

Kwa hivyo, kunako eneo hili hatujaingiza pesa hatujaona lakini tutakuja kuona kwenye bajeti lakini huu mwelekeo nakubaliana nao, lakini lazima jitihada na hali ya Serikali ielekee katika kuiendeleza eneo hili la kilimo tukifanikiwa hapa basi ile ahadi aliyokuwa ameiweka Waziri wa Kilimo hatutaagiza vyakula basi itakamilika, lakini kama hatukuelekea tukawekeza vizuri kunako eneo hili tutaendelea kumdai na

tutaendelea kumkumbusha siku zake zinaisha katika utaratibu wa kuturejeshea nafasi ndio itabakia hilo tu. Mhe. Mwenyekiti, maana aliahidi hilo.

Mhe. Mwenyekiti, katika eneo jengine ninalotaka kuchangia ni eneo la uvuvi, katika eneo la uvuvi kipaumbele hichi nakubaliana nacho lakini lazima tukubali katika uvuvi wa bahari kuu hatuwezi tukategemea kuengezeka kwa uchumi wetu, kwa sababu wenzetu hawa walioingia katika uvuvi wa bahari kuu kama hatujaweka *port of discharge* hapa tukajua kile kinachovuliwa na kinachoondoka na wakalipa kodi hatuwezi ku-*control* suala hili la uvuvi wa bahari kuu. Kwa hivyo katika suala la kukuza uchumi tunaliacha hili maana uwezo wa kuli-*monitor* mpaka sasa hivi serikali haijakuwa *serious* kunako eneo hili, lakini niseme uvuvi wa kati kwenye *middle water* na *surface water*.

Mhe. Mwenyekiti, uvuvi huu kama tutawekeza vizuri tutatunga sera ambayo itakuwa ina uwezo wa kuwasaidia wananchi wetu kutafuta wawekezaji katika eneo hili ambalo tutaingia kwa kutengeneza *share*, tutafika pahala tutawawezesha wavuvi wadogo wadogo, uchumi wetu utakwenda vizuri kunako eneo hili. Eneo hili la maji madogo na maji ya kati haya yote yako ndani ya mamlaka yetu na tunayo uwezo nayo, lakini kuwawezesha na kutunga sera ambayo tunaweza watu wetu wakaingia ubia na wawekezaji ambao wananguvu kutoka nje kunako eneo hili, angalau ule utaratibu uwepo na wananchi wetu waweze kufaidika katika eneo hili. Narejea uvuvi wa bahari kuu kwa sasa hatuwezi kuujadili kwa sababu utaratibu mzima katika eneo hilo hauko vizuri.

Suala jengine la udhibiti nataka kuliongelea suala la udhibiti wa mapato nchini. Katika jambo ambalo litaweza kukuza uchumi wetu na huu muelekeo uweze kutusaidia ili uchumi wetu ukuwe vizuri ni suala la udhibiti wa mapato nchini. Lazima tuimarishe mifumo ya ukusanyaji kodi. Mifumo tuliyonayo bado katika maeneo mengi tunakwenda *manual*. Tulisema katika bajeti zetu lakini tulisema katika muelekeo wetu tutakwenda kwenye EFD mpaka leo maana yake imekuwa ndogo hatujajua inaanza lini. Lakini *program* hii tukiiweza basi maeneo mengi ambayo mapato yetu yanapotea tutaweza kuyadhibiti katika kukuza pato kakini kukuza uchumi wa nchi yetu..

Naombe niende katika eneo ambalo nalo ni changamoto zinazotokea hapa. Karibu kila siku tunaona katika eneo la uingizaji wa mafuta nchini. Ilitolewa taarifa kuwa uchumi katika eneo hili au serikali haikuingia hasara yoyote katika eneo hili. Lazima tufike pahala katika muelekeo wa uchumi suala la mafuta likawa linayumba basi na huduma za kijamii nazo zitatetereka. Leo tunasema tu labda serikali tukiingiza mafuta tutakuwa tuna kodi ya moja kwa moja. Zipo kodi ambazo zinatokano na mzunguko wa wananchi wanapokwenda na shughuli zao. Leo hii unaweza ukakuta siku tatu dereva wa daladala ambaye analipa kodi kulingana na mizunguuko yake ya kibiashara kakaa sheli hajakutana na mafuta. Inafika pahala tunasema serikali katika eneo hili haliko sawa. Kuna madereva ambao wanafanya kazi katika *private hire* wanalipa kodi nchini na wao siku mbili hawajakutana na hayo mafuta, hili ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo la mafuta nchini sisi lazima tukiri, sisi wengine katika kufatilia tunayakuta labda wenzetu hawayaoni. Muagiziaji wa mafuta sisi tunakwenda na mtu mmoja ambaye hawa wenzetu wote watatu ambao tunawatumia hapa wanakwenda kuchukua kwake. Kwa hivyo kuwa tuna mtu mmoja anapotokea na

challenge kidogo tu ya uwezo wake labda kutetereka au labda mipango yake kutetereka huyu sasa anatuumiza sote. Kuwa na utaratibu huu kuendelea kutangaza tenda lakini tukiwa tuna mtu mmoja ambaye yeye ndiye tunayemtegemea au tumpa mkataba wewe tuletee mafuta baadaye hawa *GAPCO*, nani, wote wakachukue kwake yeye, huu si utaratibu mzuri. Sekali ifike pahali ilifikirie hili. Maana kuna kipindi anapotetereka yeye au anaposhindwa yeye maana yake tunachukua muda mpaka uitishe tender, umtafute mtu mwengine umpate, huku watu ile *massiveness* tuliyonayo ikiondoka maana yake mpaka unaingia mkataba na mtu mwengine tunaumia kwenye eneo hilo.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri eneo hili la mafuta siyo eneo ambalo tunaweza tukalichukulia hivi hivi tu tukasema serikali haikutetereka kunako eneo hili, lakini wananchi wanaotegemea shughuli zao za kiuchumi ziende kwa kutegemea na safari za ndani watakapokosa huduma kimsingi, maana yake siku ile hata ule ukuaji wake wa kuchangia uchumi nchini haupo. Nimetolea mfano watu wa daladala, lakini nimetolea mfano watu wa *tax*, lakini tumetolewa mfano sisi. Maana yake leo kama nchi hii ilikuwa iuze mafuta lita 400 kwa siku maana yake hukuziuza hizo lita 400 kama siku sita mafuta hayapo hukuuza wewe lita karibu 8000. Sasa leo hatukuingiza kitu wakati tukiuza mafuta yakiondoka serikali inapato lake. Mimi niombe tu kunako eneo hili tujitahidi sana wenzetu mtusaidie.

Mhe. Mwenyekiti, niende kunako vipaumbele, nilikuwa naangalia katika vipaumbele hivi nikaona labda serikali ilifanya jitihada kubwa na tuliwapongeza sana walipokuwa wameimarisha miundombinu ya *airport.* Lakini nikawa nasubiri labda na Bandari ya Mpigaduri ile, tuliisema sana, ujenzi wa bandari mpya, nikajua labda katika vipaumbele itaingia. Tunapokwenda leo hii tunaleta wafanyabiashara wetu wanakuja na kontena 600 tu hazina pa kukaa. Ukanda wetu siye huu ni ukanda wa bahari, ukiacha kwetu labda wenzetu wenye gati kama yetu labda uende Mombasa. Tutakapofika pahala tukaimarisha miundombinu ya bandari ikawa ni sehemu ya kipaumbele chetu, lakini humu sikuiyona. Tunaweza tukafika pahala tukaongeza ule uchumi tunaouhitaji sasa. Leo hii haipo, tukijenga bandari masuala ya *shipping harbor* yote unayafanya kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, nikuombe Mhe. Waziri wa Fedha katika eneo hili la ujenzi wa bandari ili tuone tukijenga bandari mpya wenzetu wanaweza kupitisha mizigo yao kama *transit* baadae wakasafirisha kwa meli ndogo ndogo ambapo huduma nyingi zikaimarika, mapato mengi yakaingia katika serikali yetu. Nikuombe katika mambo ambayo tuyaangalie ili yaweze kutusaidia kunakomuelekeo mzuri katika eneo hili.

Niende eneo la mwisho la utawala bora, nimeona katika vipaumbele hapa kunakipaumbele cha mwisho utawala bora, uimarishaji na taasisi za uwekaji katika hali ya usalama. Katika suala la utawala bora na kipaumbele kuwekwa ni nzuri na nadhani hili likitekelezwa vizuri watu wetu wale ambao, maana kuna baadhi wengine wapo vizuri maana unaweza ukenda katika Afisi zetu ukitegemea ule utawala bora wengine hawakupi ile *costumer care* hasa haipo, unaweza kupeleka maombi hata kujibiwa kama limefika huoni, Taasisi nyingi watu wanalalamika. Kwa hivyo katika eneo hilo la utawala bora naomba programu hii nayo ifike pahala ikiingiziwa fedha tu ili tuweze kuwaelimisha watendaji wetu lakini waweze kutusaidia katika maeneo mazuri ya kujenga nchi yetu.

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, nilizungumza katika bajeti siikumbuki ipi tu lakini naomba niliseme ambalo katika muelekeo wa uchumi linaweza likatusaidia suala la kufanya *transfer* kwenye *ownership* lakini na kwenye *cells agreement* ambazo zinafanywa na mahoteli yetu. Hapa kuna pesa nyingi zinapotea, lakini pia na watu wetu kuwa na uwezo wa kugundua wale wanaohamisha ule utawala hao wanaouziana katika eneo la mahoteli hatuwagundui na tunapigwa sana ndani ya nchi yetu. Niseme iko haja sasa ya kuanzisha kitengo ambacho kinaweza kikatusaidia katika kufanya utafiti na kufanya kazi ile ya kufatilia kwa ukaribu kabisa hawa wote waliokuja kuekeza hapa nchini katika eneo hili la kuhamisha *transfer* ya *ownership* lakini kuna masuala ya *cells agreement* na masuala mengine.

Mhe. Mwenyekiti, niseme mchango wangu nataka uelekee kunakoeneo hili kwa wenzetu wanaokushanya kodi wawe na ukaribu au wawe na utafiti au upembuzi yakinifu kuwagundua hawa watu, kwa sababu mahoteli mengi ukifuatilia ukanda wa Kiwengwa ambao siye tunapita wako waliobadilisha uongozi, wapo waliouza, lakini hatuoni ule mchango unaoripotiwa katika mapato yale yanayokuja moja kwa moja. Eneo hili lina mapato makubwa sana. Sasa tuombe wenzetu waandae kitengo cha *investigation* ili watu wetu wapewe elimu na wapewe nyenzo za kuweza kutusaidia katika kukusanya kodi katika maeneo haya.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi naona umeniwashia taa lakini niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Miraji Khamis Mussa, kwa mchango wako unasema unaona nimekuwashia taa sema pia na nimekuongezea na dakika. Sasa naomba nimwite Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame atafuatiwa na Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi na mchangiaji wetu wa mwisho kwa orodha hii niliyonayo atakuwa Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri kabla sijamwita Mhe. Waziri.

Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kwa kunipa wasaa huu kwa muda mchache tu niweze kuichangia hotuba hii nzuri sana ya Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, hotuba ambayo hii *title* yake tu peke yake ina maana kubwa sana, anasema Hotuba ya Mkabala wa Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Muelekeo wa Bajeti kwa Mwaka 2018/19.

Mhe. Waziri kataja mambo matatu mazito sana, mkabala wa uchumi, mpango wa maendeleo na muelekeo wa bajeti yetu. Haya mambo tuyatizame kwa pamoja, *vis a vis* uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa jumla kwanza niipongeze sana Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa nini nikasema hivyo. Mhe. Mwenyekiti, katoa takwimu za ukuaji wa uchumi amesema Januari/Machi mwaka jana au mwaka huu uliopita ulikuwa asilimia sita nukta tatu kutoka asilimia tano mwaka 2016, halafu April/Juni 2017 hapa kidogo kuna tofauti ndogo asilimia nane nukta nane kutoka asilimia nane nukta mbili. Kwa kweli, ukiacha hizi takwimu Mhe. Mwenyekiti, wewe iangalie picha ya nchi kwa ujumla ilivyo haitaki tochi, tunatembea nchi nyingi za Kiafrika, tunaona ukiteremka tu Uwanja wa ndege, mara nyingi uko nje ya mji, sasa unakuja zako mjini unaona hali ya mji harakati za mji, zile harakati za nchi zinakupa picha kamili, hutaki takwimu wewe, usiingie kwenye takwimu.

Mhe. Mwenyekiti, hii yote maendeleo haya ya kiuchumi yametokana na silaha moja kubwa sana ya umoja, amani na utulivu wa nchi yetu. Hili hapana budi tumpongeze sana Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti, wa Baraza la Mapinduzi pamoja na wasaidizi wake. Kwa kweli hii ni silaha kubwa sana, tunapozungumza uchumi mstakbali wa rasilimali watu au rasilimali fedha na mengineyo, amani na utulivu wa nchi ni kitu muhimu sana. Kwa hivyo mimi nimeona nianzie hapo kutoa pongezi maalum kabisa kwa serikali yetu kwa hilo.

Pili, naipongeza wizara kwa kweli huu muelekeo waliotupa leo ni muhtasari kweli, ukiingia ndani ukitafuta unajua kwamba kuna kitu kimetengenezwa lakini Mhe. Waziri kaona asitupe yote kabanabana, huu ni muhtasari. Sasa kuna masuala mengi utajiuliza unaweza ukawa unamchokoza Mhe. Waziri amwage vitu, na najua siku yake ya kumwaga vitu ni ile siku ya mfuko wa bajeti pale ndiyo anakuja na mambo ndiyo anatwambia, leo mengi kayabana bana, lakini hivyo hivyo tutamchokoza ili tupate muelekeo ule tunaoutaka.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa 5 umetajwa upembuzi yakinifu wa miradi mitano, ambao *ZIPA* wanasema wanaifanyia kazi miradi ya *PPP* ile. Mimi naomba imetajwa idadi ya miradi 11, ningeshauri sana Mhe. Waziri angetutajia hii miradi 11 ni ipi na iko wapi. Sisi kwa sababu ndio tupo majimboni, sisi ndio twenye wananchi, na hii miradi inatekelezwa kwenye majimbo yetu. Haitokuwa vyema unakuja mradi unakushtukia jimboni kwako huna habari nao, au pengine kuna mizozo unaombwa Mhe. Mwakilishi njoo utusaidia kutengeneza siasa. Ningemuomba sana Mhe. Waziri angetutajia na sisi tukaanza kufatilia wakati upembuzi yakinifu unafatilia na sisi tukazungumza na wananchi wetu kuitambua hiyo miradi huko iliko.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nahitaji kuchangia ni kwenye ukurasa wa 22/23, kataja kwenye ukurasa wa 23 namba ya kirumi (6), yaani vigezo na vya ugawaji wa rasilimali fedha kwa mwaka unaokuja wa 2018/19, anasema program na miradi yote iliyokuwa haijakamilika utekelezaji wa shughuli zake kwa bajeti ya mwaka 2017/18 hiyo itafikiriwa kupewa kipaumbele katika miradi au katika ugawaji wa rasilimali fedha. Ni wazo zuri, lakini ningemuomba sana Mhe. Waziri kwanza kabla hajaipa tena pesa, maana yake ishapewa sasa anaipa tena. Namuomba sana hii miradi ifanyiwe uchunguzi kwa undani zaidi kwa nini imekwama, pesa wamepewa kwa nini haikukamilika.

Tunapozungumza mradi siku zote tunajua una *target* fulani una *goal* fulani kwa muda fulani ndiyo mradi. Sasa kama mfano unajenga skuli, mnajua mnajenga skuli basi mnaipa pesa labda milioni 50 kwa miezi sita kama hawakukamilisha watwambie kwa nini, lakini sio skuli haikukamilika pesa imetoka, hatujui zimekwenda wapi. Sasa ningemuomba sana Mhe. Waziri ni wazo zuri, miradi ya program zile ambazo zilianzwa zimalizwe. Ningeomba watu wa Tume ya mipango wafanye uchunguzi kwa umakini kabisa kwa nini miradi ile haikukamilika, iwekwe wazi kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa 18/19 Mhe. Waziri ametaja vipaumbele mbali mbali (a), (i) mpaka (j), vipaumbele hivyo mimi naviunga mkono kabisa, sina matatizo navyo lakini ningeomba sana tuzingatie *program* au kipaumbele cha (e) kinachozungumza kuimarisha ubora wa huduma za kijamii zikiwemo elimu, afya, michezo na upatikanaji na maji safi na salama. Hili lengo ni kubwa sana ni pana na

lina nyanja zake tofauti, Waheshimiwa wengi nimewasikiliza walikuwa wakizungumza kwa upana sana suala la maji safi na salama. Hili sote tuna imani na tunataka lipewe kipaumbele kinachostahiki kwa mwaka ujao wa fedha. Mimi ningeshauri hebu twendeni mfano Kiwilaya. Leo tuseme tuivamie Wilaya ya Magharibi "B" *resources* zote, tunajua tunaanza (a) mpaka (z) nini tatizo, tufanye nini, tufanikishe nini, tumekamilisha tuondoke twende zetu Micheweni kuna tatizo gani, tuingie vipi, tupige vipi tuondoke, turudi Kaskazini "A" nafikiri hivyo Mhehimiwa tutajua tumefanya nini kwa wakati gani na tumefanikiwa vipi. Lakini tukijigawa hivi *resources* zile na *resources* zenyewe ni chache naona hatumakilishi matokeo yake siku zote matatizo yapo na nafikiri Mheshimiwa alizungumza sana hebu tutafute nini tatizo *what is the route course of the problem* pengine kuna mambo labda yako ndani yetu lakini hatuyaoni na zaidi ningeomba sana Mhe. Waziri ningemuomba hawa *planners* wake wateremke hasa.

Wateremke *grass root* wakakutane na wananchi, wakakutane na mafundi bomba wale walioko mitaani wale wanayajua matatizo *okay fine,* tunakubali kuna upungufu wa maji kwa kipindi cha kiangazi kama hichi, lakini masika keshokutwa yanakuja yakija masika keshokutwa vianzio vyote vinanyanyuka bado lakini tatizo linakuwa pale pale. Sasa mimi ningeomba sana Mheshimiwa mwenyewe mimi namkubali kabisa ni *scientist* mzuri sana anajua *fact find* inatafutwa vipi, twendeni chini tukaone nini tatizo naamini bado kidogo hatujalijua tatizo, utaalamu, maji hayapo au vitendea kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema hii niikazie lakini niongeze (j) tumeanza vyema zoezi la ugatuzi lakini katika vipaumbele sikuiona Mheshimiwa kulitaja kwa hiyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri aongeze (j) nimesema uimarishaji wa zoezi la ugatuzi hasa kukamilishwa kwa miongozo bado tulipokwenda *field* tumeambiwa miongozo inatayarishwa na itakamilishwa, itaremshwa. Sasa hili tusilisahau kwa mwaka ujao wa fedha ili tupate ile *continuity* lile zoezi liwe endelevu miongozo ile ipelekwe Mabaraza ya Manispaa, ipelekwe Mabaraza ya Miji, ipelekwe na Halmashauri ile miongozo ni muhimu sana kwa sababu bado wizara mama kwenye zile *section* za ugatuzi bado wizara mama zina sauti na matatizo madogo madogo sio makubwa madogo madogo tu lakini haya sasa yanatakiwa yawe *iron out* ili tupate njia safi ya kutuongoza ili ugatuzi ukamilike.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niendelee haraka haraka kwenye ukurasa wa 30. Ukurasa wa 30 Mhe. Waziri ametupa jadweli au kiambatanisho namba 4 kinachosema utekelezaji wa miradi wa maendeleo kimafungu. Mheshimiwa nasoma *page* hiyo kwa kulinganisha wakati huo huo na *page* 14 kwa ruhusa yako naomba niinukuu kidogo, kwa ufupi *page* 14 anazungumzia Matumizi ya Kazi za Maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, anasema kipindi cha mapitio jumla ya Matumizi ya Kazi za Maendeleo yalikuwa Shilingi 165.5 bilioni sawa na asilimia 67.8 ya lengo la shilingi 244.1 bilioni kwa miezi sita. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani zilikuwa shilingi 48.3 bilioni sawa na asilimia 89.8 ya makadirio ya shilingi bilioni 53.8 na fedha za nje zilikuwa shilingi 117.2 bilioni sawa na asilimia 61.6 makadirio ya shilingi 190.3 bilioni kwa miezi sita. Sasa Mhe. Mwenyikiti, *paragraph* hii njoo ulinganishe na jadweli hilo nilosema liliopo ukurasa wa 30. Ukurasa wa 30 pana utekelezaji wa miradi ya maendeleo umeonesha *program* na mradi halafu pesa zilizokisiwa na zilizotiwa na asilimia wa utiaji wa zile pesa.

Mhe. Mwenyekiti, hapa pana tatizo sasa sijui maana nalinganisha na huku *paragraph* kipesa zimetolewa vizuri sana, lakini huku kwenye jadweli kidogo hairidhishi, Mheshimiwa jadweli hili ukilitazama kuna *program* au *project* kama arubaini hivi sikuzihesabu vizuri kama arubaini lakini zilizopata pesa zaidi ya asilimia hamsini ni tano tu kati ya arubaini, nimezisoma naomba niwatajie kwa ufupi *Program* ya Afya ya Jamii ya Uzazi ya mama na Mtoto umepata asilimia 93.5 halafu kuna *Program* ya pili herufi zake ndogo sana kutelekeza visima vya Ras Khaimah *no* Uchimbaji wa Visima na Usambazaji Maji asilimia 58.9, halafu ya tatu Mheshimiwa ni Utafiti wa Nishati Mbadala asilimia 51.2. nyengine Mhe. Mwenyekiti, ni Ujenzi wa Jengo Jipya la Abiria Zanzibar asilimia 168.9 na mwisho Mhe. Mwenyekiti ni Mradi wa Kilimo cha Biashara na Kutolea Ujasiria mali asilimia 51.2.

Mhe. Mwenyekiti, miradi mengine yote iko chini ya asilimia 50 na baya zaidi mengine ina zero ina asilimia zero sasa mradi tumeupitisha, tumeukubali kwanini uwe na asilimia zero ulikuwa hau-*qualify* kuwa mradi huu ndio maana haukupewa pesa na sio mmoja tu Mheshimiwa miradi mingi sana ina asilimia tatu, ina asilimia nne, asilimia tano ndio pale niliposema kama miradi haifai isitiwe mwenye Mpango wa Maendeleo. Bora wana lengo fulani basi wapewe pesa kwenye *OC* walimalize lile lengo. Lakini kuwekewa maradi halafu pesa usipewe hakuna *justification* kwanini usipewe, Mheshimiwa ukiangalia jadweli linasikitisha zaidi kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tunazungumza Mheshimiwa kuweka misingi mizuri ya elimu watoto wetu wapasi vizuri, lakini leo kwenye *Program* ya Kuimarisha Miundo mbinu ya Elimu anasema Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi asilimia 0.5, Uimarishaji wa Elimu ya Msingi asilimia 36.9 Mheshimiwa Umarishaji wa Elimu ya lazima, elimu ya msingi tayari asilimia 6, Uimarishaji wa Elimu ya Lazima asilimia 3.4 na Uimarishaji wa Elimu ya Mafunzo ya Amali 13.3.

Mhe. Mwenyekiti, wewe ni shahidi mzuri tulipotembelea tunapozungumza umuhimu wa elimu bora lakini kwenye elimu ya msingi hatukupi pesa sasa kidogo mheshimiwa kidogo hapa kuna unatukwaza nini tatizo, lakini huku kwenye maelezo ya Mhe. Waziri pesa nzuri imetoka jadweli hili linaonyesha pesa haikupatikana huku kwenye *grass root.* sasa hebu tutafute tatizo liko wapi na kinachofurahisha Mheshimiwa sasa wizara hii wameka pamoja, Wataalamu wa Bajeti, Wataalamu wa Fedha na Wataalamu wa Mipango nchi nyengine ni Wizara mbili tofauti lakini kwetu tunashukuru wako pamoja, wanabadilishana mawazo pamoja, wanakwenda pamoja. Sasa tatizo kama hili Mheshimiwa hii jadweli ukipitia *item* moja kwa moja kidogo haifurahishi sasa namuomba sana Mhe. Waziri ili alifanyie *critical analysis* nimetumia maneno mawili haya mwenyewe anayafaahamu vizuri Mhe. Waziri *very critical analysis worth* undani hasa atizame kwa undani nini tatizo, elimu yetu inaposema watoto hawapasi hapa ndio tatizo. Unawapa tu asilimia 6 Elimu ya Maandalizi, Elimu ya Msingi unatarajia watoto kweli watajua kuandika na kusoma, matokeo yake ndio wataanguka tu.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri ndio pale niliposema Mheshimiwa anakuja kuzungumza Mkabala wa Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Mwelekeo wa Bajeti sisi tunamuomba sana sasa kwenye huu mwelekeo kwa mwakani atizame kwa undani kidogo hili suala likoje, sisi sote tunataka vijana wetu waende vizuri na nchi yetu ipate sifa kabisa katika elimu kama huko tulikotoka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimalizie tu kwa kusema kwamba hotuba hii ni nzuri ningemuomba sana Mhe. Waziri zile ripoti zilizowasilishwa hapa na kamati mbali mbali basi zile ziwe *working document* zake na watu wake, kwa sababu mambo yaloibua ni matatizo ya kijamii watu wamekwenda *field* wameyaona isiwe maana yake sasa hivi wanapanga lakini wana vipaumbele vyao vile wakaviacha, itakuwa kidogo hatutendei haki Waheshimiwa Wajumbe. Nashauri sana na namuomba sana maafisa wake watafute hasa yale mambo yalioibuliwa hapa wanzie pale naamini Mheshimiwa tukianzia hapo tutafika tunapokwenda.

Mhe. Mwenyekiti, zaidi sina naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na namtakia kila la kheri Mhe. Waziri. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi na baadaye atafuatia Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii kuchangia katika hotuba hii adhimu inayohusiana na bajeti kama alivyozungumza mwenzangu aliyetangulia Dkt. Mwinyihaji amesema bajeti hii ina mambo matatu na ni kweli na mimi sina haja ya kuyarudia kwa sababu amekwisha yataja na hapa yameandikwa.

Kwa kweli niseme hii hotuba ni nzuri sana tena nzuri sana waliotayarisha hotuba hii pamoja na waliotayarisha bajeti wamefanya vizuri sana hivyo nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa uwezo wake mkubwa unaoneka kwa kipindi kifupi tu alichoanza wizara hii kumekuwa na mabadiliko. Ni mategemeo yangu kwamba mabadiliko haya yataendelea *pace by pace* yaani kila siku na yatafikia na kule tunakokutaka kuwe na uchumi wa kimaendeleo unaotosheleza mahitaji yetu yote nchini na nasema Inshaallah Mwenyezi Mungu ambariki sana.

Sasa nikiendelea mimi leo mazungumzo yangu yatakuwa ni mafupi sana kwa sababu watu wote washangia tangu asubuhi watu wanachangia bajeti hii, kwa hiyo naogopa sana kurudia yale kwa yale, sasa basi niseme tu kwamba mimi sitakuwa *critic* sitakosoa kosoa kwa sababu mambo yako vizuri, lakini kidogo nataka kuwa *analytic* yaani nitakuwa nafanya uchunguzi kidogo na kuweza kuongezea hapa na pale ili bajeti hii iende vizuri na katika *analysis* zangu nitakazozitoa zinafuzatia na mapendekezo ya aina fulani ili tupate huu mkabala uliotajwa hapo juu wa uchumi unaostahiki.

Kwanza kabisa uchumi Zanzibar umekuwa na umekuwa kwa asilimia hiyo iliyotajwa sita *point something* ni kwamba nataka ijulikane kwamba umekuwa sasa kwa sababu kwamba umekuwa, ningependa kusema katika uchunguzi wangu nimeona kwamba sawa uchumi unakuwa tena unakuwa kwa kasi hiyo. Lakini kukua huko tunajitahidi kuwe sijui niseme maradufu au mara ngapi ili tuweze kutosheka na matumizi na mapato ambayo tunayafanya. Kwa mfano uchumi wa nchi yetu sisi ukikua kwa asilimia saba, nane, tisa hata kumi hata kumi na mbili hatuwezi kulinganisha na uchumi wa nchi zile zilizoendelea kwa kukua kwa asilimia mbili tu, kwasababu wao tayari uchumi wao ni mkubwa sisi ni mdogo. Kwa hiyo ili tuweze kutoshelezeka kwa mahitaji yetu basi uchumi huu unahitaji ukuwe. Tusi *flat weight* kila siku leo umekuja umepanda kidogo, mishahara imetosha lakini kesho yake umeshuka hatuna mshahara

wa kutosha wala hatuna matumizi ya mambo ya maendeleo, hii itatufikisha pahala ambapo kwa kweli itakuwa hatufiki tunakotaka kwenda, sasa katika uchunguzi wangu pia nimeona kuna mambo ya maendeleo viashiria vya maendeleo na vihusishi vya maendeleo.

Sasa vihusishi vya maendeleo na viashiria vya maendeleo wamevibainisha vizuri sana vimebainika hapa vipo na kwa kuvitaja tu kwa ufupi kukumbusha tu huwezi kuviona hapa kwenye vitabu lakini vimo, cha kwanza kabisa wametumia ile *factor* moja kihusishi kimoja kikubwa sana ambacho kimataifa kinajulikana kinaweza kika-*affect* au kinaweza kikarudisha nyuma maendeleo au kikapeleka mbele maendeleo.

Cha kwanza ni *social* wametumia *social aspect* hapa vizuri sana ya pili wametumia *economic* wametumia mipango ya uchumi vizuri kiasi kwamba hiki kitabu kimetengema vizuri. Lakini pia wameingiza mambo ya *culture* yamo ukiyachunguza yamo mambo ya *culture* ambayo ni muhimu sana katika mambo ya uchumi, lakini pia wameingiza masuala ya *institutional development* kwa maana ya mambo ya *infrastructure* na kadhalika yamo. Halafu kuna mambo ya *communicational* yote hayo yameingizwa kwenye bajeti hii, la mwisho ambalo ni muhimu *mindset* ya watu pia wameziingiza huku kwa maana nyingine zinaitwa *psychological aspect* ya bajeti yao hii.

Kwa hivyo mimi nawapongeza kwa haya sasa kutokana na sababu hiyo sasa niingie kwenye vipaumbele. Vipaumbele vimetajwa hapa vilivyotajwa nadhani nisivirudie sana ila kuna vipaumbele vya kuimarisha hivi vipaumbele vipo kwenye hivyo viashiria nilivyovitaja au vihusishi nilivyovitaja lakini kwa uchungu wa ndani kabisa unakuta tumekosa kitu cha muhimu sana. Tumekosa masuala ya *population* kwa sababu unapofanya bajeti lazima uangalie *population*, tumekosa kueleza namna gani tuta-*deal* na hii ongezeko la *population* linaloendelea kila siku na *population* yetu inaongezeka si kwa kuzaana tu lakini inaongeza kwa wageni kuingia katika nchi. Sasa hizi zinatakiwa ziratibiwe vizuri ili masuali ya elimu, masuali ya afya na kadhalika yaweze kuwa *budgeted* vizuri ili yale mahitaji ya watu kwenye mambo haya yaweze kufikiwa.

Sasa nasema kwamba kuna suala hilo nililolitaja ambalo la *population* halikuingia halafu kuna suala jengine zito sana ambalo pia ni *challenge* limegusiwa kidogo lakini linahitaji pia ufafanuzi mzuri sana ni suala la *ecology* hali ya mazingira yetu tuliyaonayo *ecology*. Kwa kweli mazingira yetu yako katika hali hatarishi sana lazima bajeti zetu ziangalie hilo. Nilisema juzi hapa katika kuchangia nisema kwamba mwaka 1980 miaka ya thamanini hapo palitokezea ukame au jua kali sana nchi hii hapa Zanzibar, mikarafuu ikanyaukanyauka, migomba ikanyauka na miti mingi mimea midogo midogo yote ikanyaukanyauka joto likapanda sana na maji ya bahari yakapanda kwa *mega* nane sijui ambayo sawa sawa na pengine na sentimita nane na kuendelea.

Wataalamu wa hali ya hewa ukienda pale ukifanya *reference* watakupa mambo haya sasa wasiwasi ni kwamba hali ya hewa kama *leakage* ingeendelea siku zile kwa siku tatu au wiki kupanda kwa bahari kuongezeka na maeneo mengi tungeyakosa. Sasa hili ni tatizo ambalo kwa kweli linahitaji kuwa-*address* tunafanya mambo ya *social* haya yote lakini hii nchi tuliyoikalia nayo inaharibika kwasababu ya kitu kinaitwa *climate change* ambayo tunaisababisha sisi yaani mabadiliko ya tabia ya nchi ambayo

tunayasabisha sisi wanadamu kwa kukata miti ovyo, kwa kuharibu mazingira kuchimba michanga ovyo, siku hizi ndio utaratibu umepangwa mzuri nausifu sana lazima kuwe na utaratibu huo hatuwezi kuchimba kiholela tu kwa sababu tutaacha ardhi nyengine itoke maji hapa na hapa ikija kutoka maji ya chumvi si rahisi kuyazuiya.

Tumeona tumekosa ardhi hapa Mwanakwerekwe hapa lile bwawa halikuwepo palikuwa na miembe nasikia hapo mimi sijaiona. Lakini nasikia kulikuwa na miembe, kulikuwa na miti mingi tu na hata nyumba pakachimba pale. Pamechimbwa sasa hivi panaleta maafa watu wameshakufa pale na sasa hivi hapawezi kufanyika lolote kila mwaka yanapokuja mafuruko pale panajaa hata gari hazipiti. Kwa hiyo, hizo ni athari za mabadiliko ya tabianchi ambazo lazima tuzi-*budget* vizuri, tupigane vita na matokeo hayo ili yasituharibie nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea tena kuna suala jengine ambalo ni muhimu sana tunapaswa tuliendeleze sana, ni hili la kiuchumi ambalo nimelitaja hapo nyuma, lakini tukizingatia na *population* inayoongezeka hali ya uchumi pia tunahitaji ku-*budget* vizuri kwa sababu kuna wanafunzi wanaozaliwa sasa hivi ambao wanastahiki waingie skuli wako wengi mno. Majimboni huko usishangae ukakuta darasa moja lina wanafunzi wadogo wadogo wasiopungua 200 kwenye darasa moja, mahitaji ya kielimu yanaweza kuwa hayatoshi. Kwa hivyo, kama tuta-*budget* vizuri tukaweza kukisia bajeti zetu vizuri ongezeko la wanafunzi watakaokuwepo, ongezeko la watu watakaokuwepo tukaji-*budget* vizuri matokeo kama haya tunaweza tukayapiga vita kabisa kabisa yasiwepo.

Kuna suala jengine hapa limezungumzwa la utalii. Utalii tunasema ni muhimu katika uchumi wetu, nafikiri ni ya kwanza au ya pili katika kuchangia uchumi wa taifa. Sasa nitasema utalii wa ndani nao una umuhimu wake, wa nje waache waje lakini na wa ndani hapa nchini una umuhimu wake wananchi wakihamasika wakaaza kufanya utalii na wao wakatembelea maeneo basi tunaweza tukaongezea pia pato, tusiwa-*charge* sana lakini wanaweza kuchangia kabisa katika kukuwa kwa uchumi huu.

Sasa ili tuyaweke vizuri mazingira ya elimu kwa wananchi wetu hapa nchini, basi nadhani naona kama ndoto lakini sio ndoto tukajenga barabara ambazo pengine zinazunguka kisiwa iwe mtu anakwenda kuangalia sehemu fulani, sehemu fulani anarudi siku hiyo hiyo. Kwa hiyo, barabara kama hizi nazo ni muhimu hata ukiweka treni basi sio vibaya kwa sababu pale Dubai ni mahala padogo sana.

Dubai ni mahala ambapo padodo hapahitaji treni, lakini wenyewe wameweka treni kwa sababu watu wanaweza na hamu ya kutembelea mahala fulani kwa treni wakarudi kwa treni wakaona wanavyokwenda. Kwa hiyo, kama na sisi tunataka kujenga miundombinu kama ile ikawa kuna treni zinazunguka zunguka basi utalii wa ndani utaweza kui-*encourage*. Kutoa pendekezo hilo sisemi kwamba hakuna pendekezo jengine linaweza kuwa zuri zaidi ya hilo, na litolewe jengine zuri zaidi ya hilo nitaliunga mkono lakini lengo nililolikusudia mimi ni kuimarisha utalii wa ndani ili nao uweze kuleta faida katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, halafu jambo jengine ambalo ningependa niligusie kwa kurudi nyuma tena kule kwenye mambo ya mapato na matumizi ambayo nimesema tunahitaji kuyaongeza zaidi ya hapo ili tuweze kukidhi haja, kwa sababu kama mapato

yatakwenda kidogo kidogo hivyo hivyo kuna suala la *redundancy* linaweza likatokezea, hatulazimishi itokezee hivyo na hivi sasa sisi tuna mpango wa kuajiri watu kwamba tuna *shortage* ya watu. Sasa kama tuna *shortage* ya watu tunataka kuajiri wakati fedha hazitoshi mapato ni kidogo, sasa hao tunaowaongeza tutawalipa nini, pia hao waliopo watalipwa nini, matokeo yake nini sasa? Matokeo yake kama tunachokipata hakitoshi hata kuendesha mambo ya maendeleo hata kulipa mshahara ndio hilo moja nililolitaja la *redundancy* halafu inawezekana watu wakachelewa kupata mshahara, inawezekana pia kukawa na utekelezaji wa kazi za maendeleo zikadumaa, kuzidi kukopa itabidi tukope ili tufidie mambo hayo na kuchelewa kwa malipo, yaani mishahara hiyo imesemwa, lakini pia kupungua kwa huduma za jamii.

Kwa hivyo, mimi bado nasisitiza Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana Wizara ya Fedha na Mipango najua ni watu waadilifu, waziri ni mahiri na makini sana aliangalie suala la kuongeza mapato na kutanua wigo. Maana yake kutanua wigo ni vianzio vile vile unavitanulia wigo unapata mapato zaidi. Lakini kuongeza sasa vianzio, kuongeza zile *source* za mapato nazo pia ni muhimu sana ili kupata mapato makubwa ya kutuendesha. Vyenginevyo nasema hotuba hii kwa kweli ni nzuri sana na tunaichangia kama hivi ninavyoichangia kwa sababu imeeleza mambo mengi mazuri, na ingekuwa haikueleza mambo mengi mazuri mazuri pengine hata tusingeweza kuichangia hapa. Lakini imeeleza vizuri sana na mimi narudia kuwapongeza na nasema naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na nitampa nafasi Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa muda huu, nitazungumza kwa uchache sana mambo mawili.

Kwanza, nitazungumzia kipengele hiki cha vipaumbele vya kitaifa hasa katika nukta (f), ukurasa wa 18. Hili ni suala linalohusiana na utafiti ni kwamba kwa mujibu wa warka huu utafiti utatiliwa mkazo sana, na hilo ni jambo muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenyewe ningetamani kwamba sentensi hii isimalizikie hivi kwa sababu inaweza kupelekea baadhi ya vipengele vya utafiti vikasahauliwa. Kwa maana hiyo ningeshauri kwamba iwe pia baada ya kuendeleza tafiti mbali mbali za kiuchumi na kijamii basi tuongeze maneno pia na kusambaza taarifa hizo za utafiti kwa wadau mbali mbali ili isaidie katika masuala ya maendeleo. Ukiacha kauli hii peke yake huenda baadhi ya watu wakapuuza na kwa maana hiyo taarifa za utafiti zikakosekana kutumika ilivyo. Kwa hivyo, nashauri kwamba katika kufanya hilo huu ni wakati muafaka wa kuanza kujenga utamaduni wa kufanya tafiti, lakini pia utamaduni wa kusambaza taarifa zinazotokana na utafiti.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wetu wengi sasa hivi wanakuwa wagumu kutoa taarifa za utafiti kwa sababu wanasema wanafanyiwa tafiti nyingi lakini hawaoni matokeo yake. Kwa hivyo, nadhani ni muhimu kuliandika ili kila anayehusika aweze kuwajibika kwamba kutoa taarifa za utafiti ni muhimu. Lakini ni vyema pia tukaelewa kwamba na tukaanza kujenga utamaduni wa kufanya maamuzi yetu kwa kutegemea

utafiti, na hapa ndipo patakapopatikana hasa ile fikra ya kwamba hatufanyi kazi kwa mazoea.

Mhe. Mwenyekiti, nchi inapoingia katika kufanya utafiti ndipo inapoanza kubadilika katika kufanya kazi zake. Kwa hivyo, mara nyingi tunashindwa kubadilika kutokana na kwamba hatujafanya tafiti za kutosha. Nadhani ni muhimu tufanye tafiti za kutosha na zitusaidie katika kutoa maamuzi yetu ya ngazi mbali mbali ikiwa pamoja na sisi wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, nukta ya pili ambayo nataka kuizungumzia inahusu vigezo vya ugawaji wa rasilimali fedha. Kwa kweli hapa Wizara ya Fedha na Mipango imepatia sawa sawa. Nasema hivyo kwa sababu hakuna kipengele ambacho hakijatajwa kinachohusiana na maendeleo. Kuna vyengine vimetajwa umahsusi na vyengine vimetajwa ndani ya programu. Kwa mfano, vilivyokuwa havijatajwa mahsus utavikuta katika programu ya MKUZA, MKUZA imetaja mambo mengi kule kwa hivyo utaikuta. Iliyokuwa haijatajwa katika MKUZA unaweza ukaikuta katika programu na miradi yote ya serikali ambayo ina-*commitment* unaweza ukakuta huko miradi ipo. Nyengine unaweza ukaikuta katika ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ambayo serikali hii inatekelezwa. Kwa hivyo, kwa namna fulani hakuna kitu kilichoachwa, kuna vitu mahsus vimetajwa lakini vyengine vya ujumla jumla utazikuta katika nyaraka nyengine ambayo serikali hii inatekeleza.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo na mimi niunge mkono moja kwa moja suala la hotuba hii. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa fursa hii ya kutoa maelezo ya ufafanuzi katika baadhi ya maeneo, lakini kabla ya kufanya hivyo nichukue fursa hii kuwashukuru sana wajumbe wote na hasa wale waliopata fursa ya kuchangia katika Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo na Mwelekeo wa Bajeti kwa mwaka 2018-2019.

Mhe. Mwenyekiti, nilichokiwasilisha ni Mkabala wa Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Mwelekeo wa Bajeti kwa 2018-2019. Kwa maana tumewasilisha ile bajeti *framework*, kwa hiyo maelezo ya kina hayamo humu, lakini maelezo ya kina yatakuja wakati tutakapowasilisha bajeti wakati ukifika.

Madhumuni ya kuwasilisha hii bajeti *framework* katika kikao hiki Mhe. Mwenyekiti, ni kupata maoni ya Waheshimiwa Wajumbe. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wametoa maoni yao kwa kuanzia tumepata maoni ya Kamati ya Bajeti, ambayo tunashukuru sana lakini na leo Waheshimiwa Wajumbe nao wamepata fursa ya kuangalia mwelekeo wetu wa bajeti 2018-2019 na wao wametoa maoni yao. Sasa kwa ujumla niseme kwamba maoni yaliyotolewa na michango iliyotolewa tunaichukua tutakwenda kuifanyia kazi, tutaizingatia na baadae *inshaallah* tutaileta kama bajeti kwa mwaka 2018-2019. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, wajumbe waliochangia hotuba hii kwa ujumla ni 16, naomba niwatambue kwa kuanza na wale waliochangia moja kwa moja, nianze na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ni.

1. Mhe. Mohamed Said Mohamed

2. Mhe. Suleiman Sarahan Said
3. Mhe. Ali Suleiman Ali
4. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil
5. Mhe. Rashid Makame Shamsi
6. Mhe. Asha Abdalla Mussa
7. Mhe. Machano Othman Said
8. Mhe. Abdalla Ali Kombo
9. Mhe. Hidaya Ali Makame
10. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
11. Mhe. Miraji Khamis Mussa
12. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini
13. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi

Kuna waheshimiwa 3 walichangia kwa maandishi ni.

1. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
2. Mhe. Suleiman Makame Ali
3. Mhe. Ussi Yahya Haji

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utambuzi huo sasa nitoe ufafanuzi katika maeneo machache. Kwa ujumla kama nilivyosema michango tunaichukua tutakwenda kuizingatia kikamilifu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini suala moja lilizungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe wengi, suala la kuwawezesha wakulima. Hili suala la kilimo lilizungumza na waheshimiwa wengi ,na wengine kuzungumzia hasa mkazo katika kilimo cha umwagiliaji maji. Niseme kwamba suala hili serikali kupitia wizara inayohusika, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi inafanya juhudi kubwa sana katika kuhakikisha wakulima kwanza wanawezeshwa lakini vile vile uwekezaji mkubwa unafanywa katika kilimo cha umwagiliaji maji ili kuongeza uzalishaji.

Mhe. Mwenyekiti, na katika uwezeshaji wakulima wanapata taaluma, wafugaji wanapata taaluma juu ya matumizi ya mbinu bora za kilimo. Vile vile serikali inatoa ruzuku kubwa sana kwa wakulima. Ruzuku ya pembejeo, mbolea inatolewa kwa ruzuku, mbegu za kisasa zinatolewa kwa ruzuku na huduma za ukulima wa matrekta nazo zinatolewa kwa ruzuku. Ukichukua mfano wa gharama za kulima ekari moja ya kilimo cha mpunga, mkulima angehitajika kutumia shilingi 480,000/- ili aweze kulima mpunga kwa ukulima wa kisasa ambao utakuwa na tija. Lakini serikali inafidia gharama hiyo kwa asilimia 75, na mkulima badala yake analipa shilingi 120,000/- tu kwa eka moja.

Gharama kamili zingekuwa karibu 480,000/-, lakini serikali inafidia asilimia 75 na kwa namna hiyo mkulima anatumia wastani wa gharama ya shilingi 120,000/-. Hiyo ni katika juhudi ya serikali ya kuhakikisha inawasaidia wakulima, lakini inaongeza kasi ya uzalishaji katika sekta ya kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa yapo mazungumzo yanayofanyika baina ya serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwa ajili ya uwezekano wa utoaji wa mikopo kwa wakulima wadogo wadogo. Mazungumzo yanakwenda vizuri na kuna mahala na sisi kama Wizara ya Fedha na

Mipango tutahusika katika mazungumzo hayo. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba wakulima wetu mbali ya kupata ruzuku hii lakini vile vile wanapata fursa za mikopo ili waweze kumudu gharama za kilimo, waweze kuzalisha zaidi kwa kilimo chenye tija lakini vile vile waweze kufaidika na kilimo wanachokiendesha.

Mhe. Mwenyekiti, kuna *NGO's* nyengine zinasaidia juhudi za serikali na ni muhimu nazo kuzitaja. Kwa mfano, *TAHA* nao wanatusaidia sana hasa katika kilimo cha mboga na matunda wanafanya kazi kubwa sana ya kuwasaidia wakulima wetu, na ziko *NGO* nyengine vile vile zinasaidia katika harakati hizo.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala la kilimo cha umwagiliaji maji nako serikali inafanya juhudi kubwa sana. Hivi sasa kuna mradi wa uendelezaji mpunga ambao unaitwa *ERPP* (*Expanding Rice Production Project*) ni Mradi wa Benki ya Dunia sasa hivi unatekelezwa uko karibu mwaka wa tatu na unasaidia katikaa kilimo cha umwagiliaji karibu maeneo tisa Unguja na Pemba. Kwa kuyataja maeneo hayo kuna maeneo yanaitwa Kwale Mpona wanaolijua eneo hilo mradi huo upo, kuna eneo linaitwa Dobi, Ole Dodeani, Machijini, Bandamaji, Mchangani, Koani, Mtwango na Kibonde Mzungu mradi huu unafanya shughuli za kusaidia wakulima katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kupitia mradi huu huu wanasaidia katika uzalishaji wa mbegu za kisasa hasa za kilimo cha mpunga, na kazi hiyo inafanyika katika bonde la Bubwisudi na Ole Dodeani. Ziko juhudi zinazosaidia katika kilimo cha umwagiliaji maji, ile wanaitwa *drip irrigation* kwa mazao ya matunda na mazao ya mboga mboga. Vile vile wizara hii iko katika juhudi ya kuhakikisha inafanya uvunaji wa maji ya mvua kwa ajili ya umwagiliaji maji, na tayari wameanza katika baadhi ya *site* kwa majaribio. Kuna *site* ya Muyuni, *site* moja ipo ya Kisima Mchanga inafanyika kazi kubwa sana katika eneo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kama Mhe. Waziri wa Kilimo alivyowahi kusema katika Baraza hili kwamba tuko katika hatua nzuri sana sasa hivi, kutumia mkopo nafuu kutoka Serikali ya Korea ya Kusini ambayo itatuwezesha katika kuimarisha miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji maji na jumla ya hekta elfu moja mia tano ishirini na nne zitawekewa miundombinu katika maeneo matano Unguja na Pemba, kuna eneo la Makarani Pemba, Mlemele Pemba, lakini Cheju vile vile Kibokwa na Bumbwisudi na mradi huu ni mkopo nafuu wa karibu dola za kimarekani milioni hamsini.

Mhe. Mwenyekiti, lilikuweko suala la uwekezaji kushajihisha uwekezaji wa nje na ndani kuendeleza viwanda vidogo vidogo nchini na hili niseme limewekwa hasa katika muelekeo wetu wa Bajeti 2018-19 serikali imeliweka hili kama ni eneo la kipaumbele kwa kujua umuhimu wake. Tukiwa na viwanda tutaongeza fursa za ajira kwa vijana wetu. Lakini tukiwa na viwanda hasa vinavyotegemea malighafi za ndani tutaongeza kuchochea uzalishaji hasa katika Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Lakini vile vile utatusaidia katika kuongeza usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi ya hivyo kusaidia kupata mapato ya fedha za kigeni katika nchi yetu. Kwa kuelewa umuhimu huo na katika kutekeleza sera ya viwanda *Industry Policy* yako mambo ambayo tayari yanafanywa.

Moja ni kuundwa uwakala wa kuendeleza viwanda nchini ambayo sheria yake tumeipitisha katika Baraza hili.

Sasa hayo ni katika mambo ambayo serikali inayafanya lakini vile vile inashajihisha uwekezaji hasa wawekezaji wadogo wadogo kuekeza katika mitambo masoko. Lakini pia hii kupitia *SMIDA* itasaidia pia katika kushajihisha *joint venture* na wawekezaji kutoka nje kushirikiana na wawekezaji kutoka kushirikiana na wawekezaji waliopo hapa nchini.

Lakini ziko jitihada ambazo zinafanyika za kutangaza fursa za uwekezaji katika Sekta ya Viwanda na hiyo inafanyika kupitia *ZIPA*. Yako maeneo maalum yametegwa Fumba katika Maeneo Huru kuna eneo maalumu limetengwa la *Industry Park* na juhudi zinafanywa sana kujaribu kulitangaza eneo hilo ili wawekezaji waweze kuja na vivutio maalum vimewekwa vivutio vya kodi na vivutio vya kifedha visivyo vya kifedha ili wawekezaji waweze kuekeza katika maeneo haya. Kuna eneo la *Aman Industry Park* juzi tu kama muekezaji mmoja tumempeleka kuangalia. (*Makofi*)

Lakini pia sasa hivi tunafanya *Master Plan* katika eneo la Micheweni nako pia kuna eneo la *Industry Park*. Kwa hivyo, juhudi kubwa zinafanywa na serikali katika kuhakikisha tunashajihisha wawekezaji kuja kuekeza katika viwanda vidogo vidogo na viwanda vya kati hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, lilizungumzwa suala la Sera ya *PPP* na Sheria pamoja na Kanuni na ilielezwa kwamba labda zingehitaji mapitio. Mimi sifikiri kwa wakati huu kwamba tunahitaji kufanya mapitio ya Sera, wala Sheria, wala Kanuni. Hii ni sheria iliyopitishwa si muda mrefu na Sera imepitishwa si muda mrefu pamoja na Kanuni zake. Sasa kuna haja ya kutekeleza Sera na Sheria zilizopo. (*Makofi*)

Miradi ya *PPP* ina utaratibu wake na imewekwa kwa mujibu wa sheria na kidogo inachukuwa muda si kwa Zanzibar lakini katika nchi zote zenye mfumo huu miradi hii inachukuwa muda. Nasema hivyo kwa sababu kunahitajika kwanza kufanyika *pre-feasibility study* kunahitajika kufanyika na *full feasibility study* lakini pia wende kutangaza tenda utoe tenda hiyo lakini vile vile na katika masuala ya kutayarisha *contract*. Kwa hivyo, hata ukienda Kenya, ukienda Ruwanda, ukienda Tanzania Bara hali iko hivi hivi.

Lakini iko miradi mingi ambayo tumeiseme hapa karibu miradi 11 ambayo imeshafanyiwa *feasibility study* na mengine imefanyiwa *pre-feasibility study* na miongoni mwa miradi hiyo ni ujenzi wa uendeshaji wa masoko yapo maeneo matano katika eneo hilo Soko la Mwanakwerekwe, soko la Mombasa, soko la Chake Chake, Soko la Kengeja, Soko la Mikunguni matano.

Lakini pia viwanda vya usarifu wa mazao ya kilimo Unguja na Pemba na kumefanyika *feasibility study*, viwanda vya michezo, Daladala *terminal* ambayo inatarajiwa kuweko pale Kariakoo nayo imefanyiwa *feasibility study* na nyumba za bei nafuu ambazo zinatarajiwa kujengwa katika eneo la Kwahani na eneo la Chumbuni. Hayo yote yameshafanyiwa *Pre-feasibility study* ama *feasibility study*. Kwa hiyo, si sahihi kusema kwamba miradi hii ipo muda mrefu sana na haijafanyiwa *feasibility study* ama hizi *Pre-feasibility study* kazi inafanyika kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala la Ajira kwa Vijana. Serikali imeona kwamba hili ni eneo muhimu na ndio maana katika kuelekeo wetu tumelileta kwenu kwamba serikali

imeliona tatizo la Ajira kwa Vijana ni kubwa na kwa mwaka huu wa Fedha na miaka inayokuja ya fedha juhudi maalum zitachukuliwa na serikali katika kuhakikisha tunaandaa programu na tunazisimamia utekelezaji wa programu hizo ili kuweza kupunguza tatizo la ajira kwa vijana wetu.

Kwa hiyo, kazi itafanyika na wale ambao wanasema kwa maelezo machache humu maelezo yatawekwa na zile fursa za ajira katika maeneo mbali mbali iwe Utalii, iwe Kilimo iwe ufugaji iwe katika maeneo ya ujenzi *real estate* yatawekwa vizuri. Lakini vile vile tutahakikisha kwamba bajeti itakuwa inaendana na utekelezaji na umuhimu wa Programu ya kukuza fursa za ajira kwa vijana.

Kuna suala la kupunguza utegemezi wa bajeti. Hapa Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe ningependa niseme kwamba kipimo cha utegemezi, ruzuku ndio inayotumika katika kupima utegemezi na sio mikopo. Kwa hivyo, mikopo hakuna nchi ambayo haikopi, hata hizo nchi zilizoendelea nazo zinakopa na kuna nchi zinakopa kwa wastani mkubwa zaidi kwa pato la taifa lao, kuna nchi zinakopa asilimi 43 ya pato ya taifa nyengine asilimia 50 ya pato la taifa. Sisi kima chetu bado iko chini asilimia 16.5. Kwa hiyo, fursa ya kukopa bado ipo kukopa zaidi na uhimili wetu wa deni hili ni mkubwa zaidi kwa sababu ni asilimia 16.5 ya pato letu, wengine wanachukuwa nusu nzima ya lile pato lao wanalikopea, kwa hiyo, sisi tuko vizuri zaidi. (*Makofi*)

Lazima nikiri kwamba ni muhimu kuongeza uwezo wetu wa ndani, hatutosita kuchukua mikopo kwa sababu bado tunahitaji kuendelea. Lakini mikopo hiyo lazima tuichukuwe pale inapohitajika na tuhakikishe kwamba mikopo hii inatumika kwa tija ili nchi yetu iweze kupiga hatua nzuri zaidi ya kimaendeleo na sio tukope kwa sababu ya kukopa tu. Kwa hiyo, tunakopa pale inapohitajika kukopa na tunakopa kwa shughuli muhimu ambazo tunajua zina mchango mkubwa sana katika kujenga uchumi wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, nirudie kusema kwamba utegemezi wetu unazidi kupungua kwa ile ruzuku niliyoizungumza pale. Mwaka 2016-17 tumeripoti katika kitabu utegemezi wetu ulikuwa asilimia 11.1, mwaka jana wa fedha ambao tunaendelea nao sasa utegemezi wetu ulikuwa ni asilimia 7.3. Lakini kwa bajeti hiyo 2018 utegemezi utashuka zaidi na kuwa wa asilimia 7.2. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe, walizungumzia suala la kutaka kwamba tuwe wabunifu zaidi na tusimamie vizuri zaidi ukusanyaji wa mapato ni jambo muhimu na tunashukuru sana kwa mchango huo na sisi tutazidi juhudi hiyo ya kuhakikisha tunakusanya mapato kuongeza wigo lakini vile vile kutizama vianzo vyengine vya mapato ambavyo vitaweza kutusaidia katika nchi yetu na katika kulitekeleza hili Mhe. Mwenyekiti, tuliwahi kutoa taarifa katika Baraza lako kwamba tayari *ZRB* imeshasaini makubaliano na Shirika la Ushirikiano, *Singapore Cooperation Enterprise* kwa ajili ya kutusaidia kujenga taaluma, kujenga uwezo wa watu wetu katika ukusanyaji wa mapato, lakini kufanya mapitio ya mifumo yetu ya kodi na kuona jinsi gani tunaweza tukaongeza wigo wa ukusanyaji wa kodi. Lakini vile vile kuweza kuimairisha watu uwelewa wao na waweze kulipa kodi kwa hiari baada ya kushurutishwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna Waheshimiwa Wajumbe walizungumzia suala la kuwa na vipaumbele vichache ni suala muhimu na nikiri ni kweli kwamba tunahitaji ku-*priorities* kuwa na maeneo machache ambayo tutayapa kipaumbele. Lakini kwa nchi changa zenye uchumi mchanga kama nchi zetu hizi suala hili sio rahisi kama hivyo tutakavyoweza kulisema, kwa sababu maeneo yote hayo ni maeneo ya kipaumbele huwezi ukasema uache elimu kwetu sisi elimu ni kipaumbele, afya bado kwetu ni kipaumbele, maji safi na salama bado ni kipaumbele. (*Makofi*)

Lakini ujenzi wa miundombinu barabara lazima tujenge uchumi wetu ni jambo la kipaumbele, suala la Utalii bado ni kipaumbele, ajira kwa vijana. Kwa hivyo, hayo yote ni vipaumbele na huwezi kulitoa hata moja katika hayo. Kwani muhimu sasa tuongeze ari ya kufanya kazi kwa bidii tuhamasishe watu wetu wafanye kazi kwa bidii, tuzalishe zaidi ili tuongeze uwezo wetu wa kuhudumia shughuli zetu za kiuchumi na kijamii katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, lilizungumzwa suala la athari la ongezeko la idadi ya watu. Ni suala muhimu tayari serikali imeshalitolea maelezo na hivi sasa tathmini inafanyika ya kuona hizi athari ni zipi lakini pia serikali imeshatoa maelekezo ya kuaandaliwa kwa sera ya idadi ya watu nchini. Kwa hivyo, hili suala linafanyiwa kazi. (*Makofi*)

Kamati ya Bajeti kupatiwa mafunzo hasa kuhusu MKUZA III, hili tunalichukuwa Mhe. Mwenyekiti, ni suala muhimu. Lakini suala la mafunzo na taaluma si kwa kamati ya Bajeti tu. Lakini nadhani lina umuhimu wake kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi lakini kwa watendaji wa serikali katika serikali yote nzima katika ngazi zote Serikali Kuu, Mikoa, Wilaya na hata Serikali za Mitaa. Ni suala muhimu ili sote kabisa ndani ya utendaji wa serikali tuwe na uwelewa mmoja kuhusiana na vipaumbele vilivyomo katika MKUZA III. Kwa hivyo, hili suala tunalichukuwa.

Lilikuwepo suala la idadi ya watalii na baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe walisema mbona hizi *figure* zinagongana katika taarifa mbali mbali. Hizi *figure* hazigongani kwenye taarifa hii tulikuwa tunazungumzia takwimu za kipindi cha miezi sita kuanzia Januari hadi Juni 2017 na ndio maana tukasema kwamba 2017 katika nusu mwaka hiyo ya 2016 watalii walioingia walikuwa laki moja arubaini na tatu elfu mia nane hamsini na moja. Lakini miezi sita ya mwaka 2017 yaani Januari-Juni waliingia laki moja sabini elfu mia tano thamanini na moja. Lakini kwa mwaka ndio hiyo hesabu ya sasa hivi tunayozungumzia laki nne thalathini na tano elfu. Kwa hivyo, hakuna mgongano wa takwimu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala lilizungumzwa hapa kwamba kuna *figure* zinagongana za mapato kwenye taarifa hii lakini na ile taarifa iliyotolewa na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Niliwahi kutoa maelezo mimi mwenyewe wakati nachangia taarifa ile ya kamati kwamba kweli kulikuwa na *figure* ambazo ziligongana lakini tayari kamati na wizara tumeshakaa na tumeshazisawazisha tayari. (*Makofi*)

Kwa hivyo, taarifa zilizomo humu ni sahihi na kwenye taarifa ile kule tumeshakubaliana kuweka sawa na *inshaallah* Mwenyezi Mungu akitujaalia huko mbele taarifa za takwimu sahihi zitatolewa katika Baraza hili. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kuwawezesha wananchi kuunga umeme, nafikiri utaratibu huu upo. Shirika la Umeme lina utaratibu wa kuruhusu wananchi kuomba kuungiwa

umeme kwa mkopo na malipo wanalipa taratibu, suala hili lipo na hii yote imewekwa kwa ajili ya kuwapa fursa wananchi kuweza kutumia huduma hii muhimu kwa maendeleo yao ya kiuchumi lakini vile vile kwa ustawi. Kwa hivyo, hii fursa ipo na serikali inajitahidi sasa hivi katika kuhakikisha visiwa vidogo vidogo katika kila bajeti nasi navyo vinafikishiwa huduma hii ya umeme.

Kuna suala lilizungumzwa je, hizi *instrument* zilizokuwa zikitumika huko nyuma za *OGL* na *STABEC* kwamba zinaendelea kutumika hadi sasa. Sasa hapa niseme tu Mhe. Mwenyekiti, kwamba ni kweli hizi *Instrument Open General Llicense (OGL).* Huko nyuma zilikuwa zikitumika, lakini zikuwa zikitumika wakati wa mageuzi ya kiuchumi katika miaka ya 80 na hizi zilililetwa na Benki ya Dunia wakati huo na watu wakati huo walikuwa na mkazo kwamba tuondokane na uchumi wa kuhodhi ambao unahodhiwa na serikali kwenda kwenye uchumi ambao unaendeshwa na soko, sasa hivi hazitumiki na kwa wakati ule walikuwa wanatilia mkazo maeneo makuu matatu, ubinafsishaji ikiwa ni moja ya *privatisation* wakati ule.

Lakini walikuwa wanazungumzia masuala ya *liberalization* ya soko wakati ule ndio yakaja hayo masuala ya *Stadex* kwa maana ya ku-*stabilize* uchumi ndio ikawa inatumika katika miaka hiyo ya 1980. Matokeo ya *instrument* hizi yanaweza yakazungumzwa kwa sababu mengine yalikuwepo mafanikio lakini mengine yalitokea changamoto kubwa sana katika uchumi wa nchi nyingi sana zilizofata ushauri huu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala la uchache wa maji katika nchi yetu ambalo nalo lilizungumzwa kwa hisia kubwa sana. Niombe kuwakikishia Waheshimiwa Wajumbe na wananchi wanaotusikiliza. Kwamba hili tatizo linafanyiwa kazi sana na serikali na apendapo Mwenyezi Mungu tatizo hili *inshaallah* ataliondoa. Sisemi muda gani lakini kwa jitihada za serikali zilizopo tuna matumaini makubwa kabisa kwamba tatizo hizi litapungua.

Nasema hivyo kwa sababu serikali imechimba karibu visima mia moja na hamsini kupitia msaada ule uliotolewa na Ras-al-Khaimah na sasa kazi inayofanyika kupitia *ZAWA* ni kuviwekea *pump* na kuweka viungo katika visima vile ili ziweze kumika na tayari serikali ilitenga karibu bajeti ya bilioni mbili kwa ajili ya ukamilishaji wa visima ishirini na sita katika mwaka wa fedha huu ambao tunaendelea nao. Tutenga fedha nyengine katika mwaka wa fedha ujao ili kuhakikisha kwamba baada ya miaka mitatu visima vyote mia moja na hamsini vinafanyakazi kama ilivyokusudiwa.

Lakini pamoja na juhudi hizo za serikali tulipata mkopo nafuu kutoka Benki ya *Exim* ya India kwa karibu dola milioni tisini na mbili nukta moja nane na sasa hivi mradi huu upo katika hatua za matayarisho ili uweze kutekelezwa. Lakini kuna mradi mwengine wa maji pia wa *ADB* kuna karibu dola ishirini na moja milioni, lakini pia mazunguzo baina ya Japan na wizara inayohusika yanaendelea hivi sasa kwa ajili ya mkopo mwengine wa dola za Kimarekani karibu milioni mia moja kwa ajili ya sekta ya maji. Sasa kubwa wananchi tunajua kabisa kwamba kuna maeneo ambayo yana upungufu wa maji tuzidi kustahamili lakini serikali inachukuwa juhudi kubwa sana ya kuhakikisha tatizo hili tunaweza kuondoka nalo kwa haraka iwezekano. (*Makofi*)

Serikali ijenge Ofisi na iachane na kukodi ndio jambo linalofanywa kila mwaka tunatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Serikali Unguja na Pemba, kuna jengo

la Afisi hivi karibuni limemalizika la Wizara ya Katiba na Sheria lakini kule Pemba kuna majengo ya wizara tatu yanajengwa kwa pahala pamoja, Katiba, Sheria, Wizara ya Fedha na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wanawake na Watoto. (*Makofi*)

Lakini nashukuru pia kwa Unguja ujenzi unaendelea katika jengo la Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Vijana, Wanawake na Watoto. Kwa hivyo, kazi hii ianfanyika Mashirika ya Serikali nayo yamehamasika nayo yamehamasika kujenga majengo yao ya Afisi na *ZURA* itajenga jengo lalke la Afisi hizi karibuni *PBZ* nayo itajenga majengo yake, Wizara ya Fedha nayo inakusudia kuanza ujenzi katika mwezi wa April. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba haya masuala yaliyochangiwa hapa yalikuwa na mengi nimejaribu kuyatolea ufafanuzi baadhi tu ya yale yaliyochangiwa kuna masuala kwa mfano ya Mhe. Hussein Ibrahim Makungu suala la uimarishaji wa Sekta ya Utalii na lilizungumzwa pia na Mhe. Miraji Khamis Mussa kwamba hawa *Singapore Cooperation Interpirse* tunashirikiana nao katika utayarishaji wa mkakati wa kuimarisha sekta ya utalii nchini.

Mkakati huo wameshafanya vikao mbali mbali na wadau mbali mbali na watendaji mbali mbali katika serikali katika serikali katika suala la kuimarisha mkakati huu, lakini vile vile na utayarishaji wa gharama ya utekelezaji wa mkakati huu. Utakapokamilika *inshaallah* utakuwa ni sehemu ya mazingatio katika utayaarishaji wa bajeti zetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa naomba niwahoji wale anaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mkono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yenu na utulivu wenu na mimi nichukuwe nafasi hii kuwashukuru sana Kamati ya Bajeti pamoja na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa hotuba yake ya Mkabala wa Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Muelekeo ya Bajeti 2018-19 na matumaini yangu mpango huu ni mzuri na tayari utafanyiwa kazi ili kuleta matumaini kwa wananchi pamoja na Wajumbe Wawakilishi wote kwa jumla. Nawashukuru sana. Sasa naomba niahirishe kikao hichi mpaka kesho tarehe 28/02/2018 saa 3:00 asubuhi.

(Saa 01:01 usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 28/02/2018 saa 3:00 asubuhi)